NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Thelathini – Tarehe 20 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli zetu za leo, katika kikao chetu cha Thelathini, tunao wachangiaji wetu tutaanza na Mheshimiwa Rashid Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucia Mlowe.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kusimama hapa. Mchango wangu wa leo si mkubwa nitazungumza mada fupi kwa sababu tayari nilishachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu kubwa ambalo naliona katika kilimo ni wakulima wadogo wadogo,

Wabunge wote wanawaona wanavyohangaika katika kilimo; mvua, jua, usiku na mchana na mazao yao tunayaona barabarani yanavyooza. Huu ni mtindo wa kila mwaka. Wakulima wanalima wanatumia nguvu zao jasho lao ni maskini kabisa, lakini hatimaye mazao yao yanapotea ovyo. Serikali wanaona, Mheshimiwa Magufuli Rais, alikuwa ni Mbunge alikuwa anapita barabarani anaona mazao yanavyooza lakini amechukua hatua gani? Soko liko wapi la wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri kama anataka kutumikia Taifa hili kwa kilimo tafadhali awajali wakulima wadogo wadogo. Wakulima wadogo wadogo ndio wanaoleta maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika Uvuvi wa Bahari Kuu. Uvuvi wa Bahari Kuu kwa taarifa za Waziri kwamba wanatoa leseni kwa dola elfu 50 kwa mwaka. Meli zinakwenda kuvua huko kwa samaki wanaotaka wenyewe na wale wa ziada wanawapoteza, kuna meli za uvuvi mia moja na tano kwa taarifa ya Waziri. Wanavua bahari kuu wanachukua samaki wanaowataka wa ziada wanawapoteza. Serikali ina utaratibu upi wa kuweza kulinda mazao haya ambayo yanaingiza fedha za kigeni kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetulia kimya Waziri mwenyewe anasema, anawaagiza, samaki wa ziada mlete juu kama vile ni kampuni yake. Kuna sheria ipi ya kuhakikisha samaki wale wa ziada wanaletwa huku katika nchi yenyewe. Kwa hiyo, wanakwenda katika vyombo vya habari anazungumza na Waandishi wa Habari, anawaambia samaki wa ziada leteni nchini huku. Hasa watu watoe meli zao huko *deep sea* walete huku nchini wapoteze mafuta yao bure, kuna utaratibu upi ulioweka Mheshimiwa Waziri kuweza *ku–save* mapato haya ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kuna masuala haya ya migogoro ya wakulima, migogoro hii inazidi kukua kwa Wakulima na Wafugaji. Tuna hekta milioni

88. Kati ya hekta milioni 88 kuna hekta milioni 60 ambazo zinafaa kwa wafugaji. Hata hivyo, *unit* tulizonazo za ufugaji ni *unit* bilioni 20 lakini mahitaji yetu ni *unit* 17.1 tuna tatizo gani la kuweza kuondoa mzozo huu wa wakulima na wafugaji. Kwa hiyo Serikali imetulia kimya tu. Mmechukua hatua gani watu wanauwana, mifugo inakufa, mizozo yao hii haishi. Uwezo wa kuweza kuyatatua tunao, kitakwimu tunafanya kazi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana dhima kubwa ya kuhakikisha kwamba mizozo hiyo ya wakulima na wafugaji wakishirikiana na Wizara nyingine inatatuliwa ili ku– *ave* maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mbolea, Serikali hii imekuja na dhana ile ya viwanda na kila ninavyoona ninavyopima tafsiri ya kilimo kwanza imeondoka. Kwa hiyo dhana iliyopo ni ya viwanda, sasa matokeo yake ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015/2016, Awamu iliyopita ilitoa mbole na pembejeoyenye dhamani ya bilioni 78, lakini mwaka 2016/2017, Awamu ya Mheshimiwa Rais Magufuli wametoa bilioni 10 hii inaonekana kama ni dharau hivi! Bilioni 78 ambapo wakulima wenyewe wamelalamika kwamba hazikutosha, leo Serikali hii imeweka bilioni 10, *is nothing*. Hii ni dharau kwa wakulima, kama hukutia mbolea basi mazao yatapungua. Mvua tumepata za kutosha lakini mvua pekee hazitoshi, lazima tuzi-*support* na mbolea na nina imani kwamba mazao kipindi yatapungua kwa sababu mbolea kipindi kilichopita haikutosha, wala haikufika kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya chakula; wakulima wamelima kipindi kilichopita na kwa bahati nzuri wakapata mazao mengi, wakazuiliwa kabisa kusafirisha mazao yao nje. *NFRA* wakanunua mazao tani milioni 13 *something* ambazo zina thamani ya bilioni sita. Zimekuwa *declared* kwamba zimeharibika kwa mvua kwenye maghala. Waziri mwenyewe anasema katika maelezo yake kwamba

zile tani hazikuharibika, ni watu wamefanya michakato yao tu. Waziri anajua, amechukua hatua gani kwa watu hawa?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya Serikali imepotea bilioni sita (6) na zaidi, mazao ya wakulima yamenunuliwa na yalizuiliwa kupelekwa nje, wakulima wamepewa fursa zote halafu wahuni wanasema yamenyeshewa na mvua lakini hadi sasa hakuna hatua iliyochukuliwa. Mheshimiwa Waziri nataka kujua fedha ya umma iliyoharibika kwa uzembe wa stoo hizi za *NFRA* na kupoteza bilioni sita, watu hawa wamechukuliwa hatua gani?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, kama tutakwenda hivi katika kila Wizara kama haipo *serious* na nguvu za wakulima haipo *serious* na kuwasaidia wakulima, haioni huruma, nataka Waziri hebu tumpe hekta moja tu au robo heka tu aende akalime, amwagilie maji avune mazao yake, halafu mazao yale yaharibike arudi tena mwaka wa pili alime tena na hakuna *support* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wafugaji, mara hii tumeona kwamba ng'ombe wengi wamekufa, lakini Mheshimiwa Rais Magufuli anawaambia nendeni mkauze ng'ombe akauze wapi ng'ombe? kwani ng'ombe wanauzwa vipi. Ng'ombe wanakufa kila maeneo hakuna malisho, lakini sasa hizi mvua zinavyonyesha utakuta majani yamezagaa tele, hakuna utaratibu wa ku-*process* majani yale. Kuna mashine nyingi unavuna majani unaweka katika stoo wakati wa kiangazi Serikali inapata mapato wanauzia wakulima ambao hawana majani, majani mashambani yanapotea bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine ya kuyasindika majani yale ziko tele na ni rahisi. Serikali imekaa tu, fedha ile pale na ng'ombe wanakufa, mifugo inakufa, watu wametulia hapa, wanakwenda huko na kurudi, tujenge raslimali yetu kwanza, tutunze rasilimali yetu, tutunze kilimo, tutunze mifugo, zile *initiative* tulizonazo tuzitumie hizo kwanza

usianzishe viwanda vikubwa lakini viwanda vidogo vya wakulima huku wanakufa, wewe unaanzisha viwanda vikubwa tu, *what for* ? Maana yake nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya kilimo ni asilimia 65.5 kwa mujibu wa taarifa zako, wengine wanasema asilimia 75 sijui *who is wrong* kama Waziri yuko sahihi au tuzungumze hapa, lakini vyovyote itakavyokuwa ni kwamba sekta ya kilimo inabeba Taifa. Kwa sababu inabeba Taifa Sekta hii ya kilimo nguvu za Awamu hii ya Tano ziko wapi, hatujaziona, tunasikia zimeagizwa matrekta lakini, hebu kwanza tuimarishe kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo wanasema, kilimo ndiyo maisha.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako, Mheshimiwa Lucia Mlowe atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla na Mheshimiwa Richard Ndassa ajiandae.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo, bila kilimo hatuwezi kufikia lengo letu la Tanzania ya Viwanda. Ukiangalia bajeti ya kilimo kama kweli kilimo ni uti wa mgongo bajeti ni ndogo sana, asilimia 4.9 ambayo inakwenda kuwasaidia Watanzania ambao ndiyo asimilia kubwa ya wakulima, asilimia 70. Bajeti hii ni ndogo naiomba Serikali iongeze bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushindani wa soko usio wa haki. Kuna ushindani wa soko usio wa haki. Kwa mfano, Mkoa wa Njombe wanazalisha viazi kwa wingi, viazi hivi hawaruhusiwi kuweka zaidi ya kilo mia moja wakati Wakenya wanaweka zaidi ya kilo mia moja na wanauza soko moja. Naiomba Serikali iliangalie suala hili kwa sababu Watanzania wanapata hasara, viazi vyao havitoki, Wakenya wanaweka vingi na viazi vyao vinatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama za upimaji wa udongo. Katika Mkoa wa Njombe wakulima wanachukua udongo ule kupeleka Mbeya kwa ajili ya kupima na udongo huu unapimwa kwa *unit* moja kwa Sh.75,000/=, kila shamba linatakiwa liwe na *unit* nane, kwa hivyo shamba moja linagharimiwa kwa shilingi laki sita na elfu saba. Kwa kweli wakulima hawataweza kuendelea na suala hili la upimaji wa udongo kwa sababu ya gharama hizo. Naiomba Serikali iwapunguzie au iwasaidie wakulima wa Njombe udongo huu upimwe kule kule Njombe badala ya kusafirishwa kwenda Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tozo. Ninaishukuru Serikali kwamba katika hotuba ya Waziri umeeleza kuondoa tozo mbalimbali, ninashauri kwamba tozo hizi zingeorodheshwa zote, halafu tuone ni tozo zipi zinatoka na tozo zipi zinabaki. Kwa sababu ukiangalia kwa mfano, wakulima ambao wana vyama vyao vya ushirika wametolewa ile tozo ya Sh.500/= isiwepo, nafikiri ni vema kuondoa zile tozo kubwa zinazotozwa na Serikali kuliko kuziondoa zile tozo ambazo ni za wakulima wadogowadogo, kwa sababu zile zitawasaidia kwenye vyama vyao vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaiomba Serikali iliangalie suala hilo tena kwa sababu ni kweli tozo hii imetolewa kulingana na hotuba yako lakini bado wakulima wadogo ambao wana vyama vyao vya ushirika watapata hasara, kwa sababu hawatapata kitu chochote cha kuendeshea vyama vyao vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu za viazi. Mwaka jana kulikuwa na tatizo katika Mkoa wa Njombe wa kuunguliwa viazi kutokana na hali ya hewa, hawakupata kabisa viazi na Serikali iliahidi kuwasaidia na wakawa wamesaidiwa kiasi fulani cha mbegu. Zile mbegu walizosaidiwa kwa kweli hazifai na siyo nzuri, hivyo wakulima hao wamepata hasara vile viazi haviuziki kwa sababu zile mbegu siyo kama mbegu ambazo walizoea kuzitumia miaka yote. Naiomba Serikali iwasaidie wakulima hawa kama

inawezekana kufika Njombe na kuona ni namna gani wanaweza kuwasaidia wapate mbegu ambazo ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Kilimo mpaka sasa hivi siielewi ni namna gani inawaisaidia wakulima. Mwaka jana tulipata maelezo mazuri tene ilikuwa semina nzuri sana ya Wabunge wote tulielekezwa kwamba benki hii itakwenda katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa hivi katika Mkoa wangu wa Njombe wakulima wanalalamika na wanahangaika sana kwa sababu benki hiyo ingeweza kuwasaidia sana wakulima kupata mikopo na kuweza kuboresha kilimo chao ili waweze kupata maao kwa wingi na iwasaidie angalau kupanda kwa uchumi wao na Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe ni kati ya Mikoa ambayo inazalisha chakula kwa wingi, tatizo kubwa ninaloliona ni kwamba hawana maghala ya kutosha. Kuna ghala moja Makambako. Naishauri Serikali kuhakikisha maeneo kama haya na hasa Nyanda za Juu Kusini na kila Mkoa unakuwa na ghala za kutosha kwa sababu vyakula wanavyozalisha vinaishia kuoza au kutawanya ovyo kwa sababu hawana ghala. Ghala zingesaidia sana angalau kuhifadhi chakula na kusaidia nchi nzima

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo; nashukuru kwamba Serikali imetamka sasa pembejeo na hasa mbolea zitawekwa madukani, ninachoomba na kusisitiza ni utekelezaji. Mbolea iwekwe madukani pamoja na pembejeo zingine ziwekwe madukani ili kusudi wananchi hawa waweze kununua kwa urahisi na kwa wakati wowote hasa kwa Mkoa wa Njombe karibu mwaka mzima wanalima. Kwa hivyo, kama watakuwa na mbolea hizi madukani maana yake watazalisha kwa wingi na muda wote hawatakuwa na shida na bei za pembejeo hizi zitakuwa zimeshuka kwa sababu zitakuwa madukani. Kwa hivyo, niiombe sana Serikali na nisisitize utekelezaji wa suala hili ambalo Serikali yenyewe imeahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mifugo, wafugaji na wakulima. Kuna maeneo yanayopakana na Mbeya ambalo ni eneo la Wilaya ya Makete, kuna tatizo la wakulima na wafugaji, wakulima wanalima vyakula vyao lakini wafugaji wanapeleka mifugo yao wanalisha mashambani. Naiomba Serikali kwa sababu nafikiri ni maeneo mengi ambapo tatizo hili lipo, suala hili lishughulikiwe kwa sababu linawakatisha tamaa sana hasa wakulima, kwa kuwa wanalima kwa bidii halafu ng'ombe wanakuja wanakula, kwa hivyo tunawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naiomba Serikali isaidie kutatua mgogoro huu wa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mlowe. Mheshimiwa Sigalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niungane na wachangiaji waliopita kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, nipongeze pia timu yake kwa pamoja kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura alizungumzia sana hasa katika suala zima la kuondoa tozo katika mazao mbalimbali na hili ameshaanza nalo, Mheshimiwa mchangiaji aliyepita anasema tozo, jamani ni hatua kwa hatua. Ameanza na tozo sasa baadaye itakwenda kwenye kutafuta masoko, ni hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitasema sana kuhusu pamba kwa sababu wewe Mtemi ni shahidi, tumezungumzia sana kuhusu zao la pamba, bei na mambo mengine. Najua Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, sasa yale ambayo tutakuwa tunayasema humu ni vizuri Serikali ikayachukua na

kuyafanyia kazi. Si jambo jema sana Waheshimiwa Wabunge wanasema jambo hilo hilo lakini tukumbuke zao la pamba kwa Kanda ya Ziwa ndiyo baba na ndiyo mama, ndiyo kila kitu. Uchumi wa Kanda ya Ziwa unategemea zao la pamba, bila pamba kwa kweli katika Kanda ya Ziwa sijui kama wengine tungekuwemo humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa sababu hata tukiulizana humu ndani ikifika pahali tunabeza pamba, sijaona humu Mbunge aliyevaa nguo ya ngozi ya ng'ombe au ya punda; wote tumevaa nguo zinazotokana na zao la pamba. Sasa kama mahitaji ya pamba ni makubwa, leo hatutaki kuzingatia na kuona kwamba zao hili ni zao la biashara na linasaidia nchi hii, kwa kweli tutakuwa hatujitendei haki. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ilione hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kuhusu kilimo cha kutumia matrekta. Mwaka jana kama unakumbuka wakati Waziri anawasilisha taarifa yake hapa alisema kwamba kuanzia sasa na kuendelea tunataka tuanze kununua matrekta ya kutosha ili kusudi jembe la mkono tukutane nalo makumbusho au sehemu nyingine. Sasa nimejaribu kuangalia kupitia Mfuko wa Pembejeo, wali-*project* kununua matrekta 79 lakini yaliyonunuliwa ni matrekta 43, matrekta ya mikono *power tiller* 10, hakuna hata moja lililonunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha wamekisia kununua matrekta mapya 71. Sasa sioni kwamba hivi kweli nia ni kununua matrekta nchi hii ipate matrekta ya kutosha. Hata hivyo, tukitaka kulima kisasa, kilimo kipana, mashamba makubwa ni lazima tutumie matrekta; hatuwezi tukaendelea kutumia jembe la mkono halafu ukawa na kilimo kikubwa. Lazima matrekta yatumike, kama hukumwezesha yule mtu mdogo kule chini kumkopesha kupitia huu Mfuko wa Pembejeo matrekta yatakuwa labda ni ya mjini tu lakini wakulima wakubwa wapo vijijini na bila kuwakopesha wakulima kule vijijini hawawezi kulima kwa kujitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Tizeba yeye ni mtoto wa mkulima pamoja na kwamba ametoka kwenye wafugaji, yeye ni mtoto wa mkulima anaifahamu Mwanza, hebu atusaidie hasa upande wa matrekta ili kusudi matrekta yaende yakafanye kazi yake kule yalime kwa kilimo siyo cha kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye mazao kujitosheleza hasa kwa chakula. Inashangaza kuona kwamba eti nchi hii, nitoe tu mfano Mkoa wa Morogoro tulikubaliana hapo mwanzo kwamba kuwe na ghala la chakula la Taifa, lakini sioni jitihada zozote zile kuonesha kwamba ni kweli pale ni ghala la chakula. Tulisafiri juzi kwenda Mlimba, mito tuliyokutana nayo, nikauliza hivi Mkoa wa Morogoro una jumla ya mito mingapi? Nikaambiwa Mkoa wa Morogoro una jumla ya mito zaidi ya 1000 na inafaa kwa umwagiliaji. Sasa unajiuliza hivi tatizo letu ni akili zetu au kutokutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mkoa huu una mito zaidi ya 1000 na inatiririsha maji mwaka mzima, hivi kilimo cha kumwagilia kinatushinda nini? Una mito zaidi ya 1000 huwezi kumwagilia, maji unayaacha tu yanatiririka yanakwenda baharini; kwa nini maji yale tusiyatumie kwa ajili ya umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hivi inawezekana kweli Tanzania tukawa tuna njaa? Hivi mwanzo wakati wa Baba wa Taifa, kuna mikoa minne ilichaguliwa, *the big four* ikawa inazalisha chakula cha kutosha kwa makusudi. Tukawa na siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona lakini hiki kilimo cha kufa na kupona sasa hivi sijui kimefia wapi, siasa ni kilimo nayo imefariki dunia, hakuna. Sasa hii mikoa mitano au minne, leo tukisema kwamba hebu tuiwezeshe hii mikoa iliyokuwa inazalisha kwa wingi chakula, chakula hicho kiweze kusaidia maeneo mengine yenye ukame lakini mikoa hiyo na yenyewe tumeiacha, hatupeleki mbolea na tukipeleka mbolea ni ya shida.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kwa

hii mikoa mitano au minne hebu turudi nyuma tuagalie ni wapi tumekosea na wapi sasa tufanye nini. Nashauri, siyo jambo jema sana kukaa tunalia hapa kwamba chakula hakuna, lakini lazima tulie kwa sababu inawezekana wenzetu wataalam mnataka kutusaidia lakini hamtaki kutusaidia. Ukitazama ile timu ya Mheshimiwa Waziri ina Maprofesa na Madaktari waliosomea mambo ya umwagiliaji lakini umwagiliaji sasa unaonekana na wenyewe hauna tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye suala la pembejeo kwa mfano upande wa zao la pamba inasikitisha tu, imesemwa jana hapa. Pembejeo zinaenda kwa wakati ambao haufanani na majira yanafahamika kwamba majira ya kulima pamba ni mwezi fulani, kupeleka dawa ya kupulizia wadudu ni mwezi fulani na kupeleka mbegu ni mwezi fulani lakini inapelekwa tofauti. Kwa utaratibu huu mazao yetu yanakwenda kufa. Tulikuwa tunaongoza kwa mazao mengi tu si katani, pamba, korosho wala kahawa lakini leo mazao yote haya yameshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji ukitazama kwenye majedwali huku unashuka, mfano zao la pamba mwaka jana ilikuwa tani 122; mmekisia tani laki moja na nusu, hamuwezi kufika pamba haipo msijidanganye. Hii tani laki moja na nusu hamuwezi kupata hata siku moja, mmetoka kwenye tani 122 mnataka kwenye 150 mtaipata wapi? Pia hawa wakulima wa pamba mnawasaidia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri na kumwomba sana Mheshimiwa Tizeba najua changamoto ziko nyingi kwenye Wizara yake, lakini hebu wakae na wataalam hasa kwenye suala la chakula kwa sababu hata Mheshimiwa Rais amesema jamani tunalia njaa, tunasema hatuna chakula, Masanja yeye analima anavuna, Athumani kwa sababu ni mvivu halimi, anakaa anasema kwamba tunaomba chakula cha njaa, lakini kama tuki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa. Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote naomba niunge mkono hoja hii. Pia napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna inavyojitahidi kufanya utafiti kuhusiana na zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imekuwa ikifanya utafiti wa aina mbalimbali hatimaye ulitoa mbegu aina ya manyoya kwenda kwenye mbegu ambayo haina manyoya. Pamoja na changamoto zilizopo katika mbegu hiyo, Serikali imejitahidi kutoa elimu kwa wakulima na hatimaye wakulima wameweza kufanya kama inavyotakiwa na hapa tunaona ongezeko la pamba mbegu kutoka tani 122,000 mpaka 150,000. Kwa hiyo, kuna kuwa na ongezeko la tani 28,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba zao hili ni zao la uchumi katika Mikoa yetu ya Magharibi. Ni zao ambalo linategemewa lakini limeonekana haliwezi kumnufaisha mkulima kama inavyotakiwa. Pamoja na elimu inayotolewa hii mbegu ambayo imetolewa manyoya ambayo ni *UK 91* imekaa muda mrefu sokoni na kupoteza ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango yangu iliyopita niliweza kuchangia kuhusu udhaifu wa mbegu hii, mbegu hii imekuwa ina matunda machache sana ukilinganisha na wakati ilivyokuwa inaanza. Kwa sasa inakuwa ina matunda kumi tu kwenye shina hadi ishirini kwenye shina moja, kwa hiyo inasababisha uvunaji wa kilo 300 katika heka. Kwa hiyo, pale bado hatujamsaidia vizuri mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali baada ya kusikia michango yetu iliyopita sasa imeweza kuja na mbegu mbya aina ya *UK M08.* Sisi Wabunge tunaotoka Mkoa wa Simiyu tunaelewa kwamba mbegu hii imefanyiwa majaribio katika Kata ya Mwabusalu na kuanzia inavyoota majani yanavyotoka mbegu hii imekuwa ikiweka matunda kuanzia chini mpaka juu na mpaka sasa takribani kuna wastani wa matunda 50 mpaka 100 katika shina moja na hivyo kutegemea katika msimu huu kilo zitaongezeka kwa heka moja kutoka kilo 300 mpaka 1000 au 1200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshangaa Mbunge mwenzangu wa Mkoa wa Simiyu ambaye bado anaongelea mbegu ya manyoya; Simiyu hatupo huko. Huyo haudhurii vikao vya *RCC,* hajui Simiyu tunaendaje, kwa hiyo asiturudishe nyuma kwenye mbegu za manyoya, sisi tupo na mbegu ya *UK M08.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kabla pamba hii haijaanza kuvunwa katika Kata ya Mwabusalu aende akaingalie kwa namna ilivyostawi ili walete sasa mbegu ya kutosha katika Mkoa wa Simiyu, hatutegemei tena kutumia mbegu ya *UK 91. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine la pembejeo; wakulima wa pamba walizoea dawa ya pembejeo ya mafuta, lakini nimefuatilia na kuona kwamba dawa hii imekataliwa kwa sababu ina sumu nyingi na kuletwa aina nyingine ya dawa ya maji aina ya *bametrim.* Dawa hii bado haiui wadudu vizuri, tunaomba pia utafiti uendelee kufanyika ili dawa hii iweze kuwaua wadudu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao hili pia linakaribiwa pia na kupungua kwa mbolea katika ardhi, tunaomba wakulima wahamasishwe kwa hiyari waweze kuweka samadi, tunao ng'ombe wengi hivyo waweke samadi ambayo itaweza kuiboresha ile rutuba ambayo muda mrefu mbolea yake imeonekana kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto zingine;

mzunguko dhaifu wa usambazaji wa pembejeo. Taasisi zenye msaada dhaifu kiufundi na kifedha kama Mfuko wa Uendelezaji Zao la Pamba *(CDTF)* pamoja na Bodi ya Pamba zimekuwa hazina msaada wa karibu kwa wakulima. Mkulima anakatwa Sh.15/= kwa kilo kwa ajili ya kuongeza uboreshaji wa zao hilo lakini matokeo pembejeo zimekuwa haziletwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aziangalie hizi taasisi, ziimarishwe au zifanyiwe kama kule kwenye Bodi za Korosho kulivyofanywa ili na sisi wananchi wa Simiyu wakulima wa pamba tunahitaji tija katika zao letu la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichangie tozo katika sekta ya mifugo; naipongeza Serikali kwa namna inavyoendelea kufuta tozo katika sekta hii ya mifugo. Kabla sijachangia naomba niweke kumbukumbu sahihi, siyo kweli kwamba mfugaji anapopeleka ng'ombe wake mnadani anatozwa ushuru wowote, mfugaji huyo ambaye kwa jina lingine anajulikana kama muuzaji. Serikali ilifuta ushuru wa aina yoyote kwa mfugaji anaepeleka mfugo wake mnadani toka mwaka 2003. Baadhi ya ushuru kama wa Halmashauri ulifidiwa na Serikali kuu kwa ile *general purpose. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, Mheshimiwa Mbunge naposema kwamba wananchi wa Simiyu wale wafugaji wanatozwa ushuru anapotosha. Ushuru unaotozwa ni kwa mnunuzi; kuna ushuru wa Halmashauri na ushuru wa kusafirisha mifugo nje ya Wilaya. Nashukuru Serikali imeazimia kuufuta ushuru huo nami naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono kwa sababu ushuru huu haukuwa na tija yoyote kwa Halmashauri au Serikali Kuu. Serikali iangalie vyanzo vya Serikali Kuu vinavyotozwa kule chini kwa kutumia *ERV* na stakabadhi yoyote inayotoka Serikali Kuu, fedha nyingi haiingii katika Mfuko wa Serikali, inaingia katika mifuko ya watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unataka kushuhudia hilo, tafuta wiki moja yoyote uangalie makusanyo ya ushuru yaliyotokana na mifugo kwa wiki katika Halmashauri moja ulinganishe na zile *permit* zilizokusanywa na Serikali Kuu kwa idadi ya ng'ombe. *Obviously,* ng'ombe waliokusanywa na halmasahuri wako juu kuliko waliokusanywa na Serikali Kuu, kwa hiyo fedha nyingi inaingia katika mifuko ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu mnada wa upili, Mnada wa Mhunze, mnada huu ni *secondary market.* Wafanyabiashara wengi wa mifugo...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** ...naomba itozwe ile tozo ya Sh.2,500/= kwa sababu Sh.5,000/=...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bashungwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii muhimu sana ambayo inabeba asilimia 65 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Tizeba na Naibu Waziri, Mheshimiwa Olenasha kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia hizi Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Pia nichukue nafasi hii kupongeza Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa kweli wamefanya kazi nzuri ya uchambuzi wa sekta hizi muhimu kwa Watanzania na nina imani kwamba Serikali itazingatia yale mapendekezo mazuri ambayo Kamati imetoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina machache ya kuchangia katika bajeti hii, naomba nianze na suala la kodi

kero 17 ambazo zimeondolewa. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutimiza ahadi ambayo aliahidi wakati wa uchaguzi na kodi kero hizi ziko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais tunakupongeza sana na tunakuombea ili uendelee kuchapa kazi tutimize zile ahadi ambazo tuliwaahidi Watanzania katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi nzuri, changamoto bado zipo, kwa sababu nia ya Serikali katika kuondoa kero hizi 17 kwenye kahawa ili kumsaidia mkulima wa kahawa bei ya kahawa iweze kupanda. Kuondoa kodi ni hatua muhimu katika kupandisha bei, lakini bei ni *factor* ya zaidi ya kodi, kuna thamani ya bidhaa yenyewe. Sasa ili zao la kahawa liweze kupanda bei sambamba na upunguzwaji wa hizi kodi kero, Wizara inawajibika kuwasaidia wakulima wa kahawa kuongeza thamani kwenye ile bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna Mfuko wa Kahawa ambao baadhi ya kodi zilikuwa zinaenda kwenye ule Mfuko ili uweze kumsaidia mkulima wa kahawa aweze kulima kahawa ambayo ina thamani. Mfuko huu sijui unasimamiwaje, umekaa kimya, nimefuatilia naambiwa Mfuko hauna hata shilingi moja. Naomba Wizara irudi kuhakikisha Mfuko huu wa Kahawa zile kodi zilizotakiwa ziingie katika Mfuko huu ili uweze kumsaidia mkulima wa kahawa, basi tumsaidie mkulima wa kahawa ili kahawa anayolima iwe na ubora. Kwa vile Serikali imeshaondoa kodi kero hizi 17, basi kahawa ikiwa na ubora ukaongeza hizi kodi ambazo zimetolewa, zitamsaidia mkulima wa kahawa kupata bei nzuri katika kahawa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kodi hizi ambazo zimeondolewa nyingi zimelenga kwenye zile kampuni ambazo zinasindika, sasa *trickle down effect* ya kodi lazima Serikali isimamie kuhakikisha hii *reduction* ya kodi ambayo imetolewa inaenda kwa mkulima kwa sababu ndiyo nia ya Serikali kumsaidia mkulima wa kahawa. Kwa hiyo, kupitia Bodi ya Kahawa, kupitia Vyama vya Ushirika Serikali iendelee

kufanya hizi *reforms* ili tuone mwisho wa siku mkulima wa kahawa ndiye anayenufaika *along the value chain.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hili, napenda kuiomba sana Wizara, mara nyingi tunaziachia Halmashauri ndizo zihangaike na kumsaidia mkulima wa kahawa, lakini suala la miche, kama nilivyosema ule Mfuko wa Kahawa, wekeni fedha za kutosha ili tuwasaidie wakulima wapande kahawa kwa wingi na kwa sababu sasa hivi tumeshawaondolea kodi kero ili uzalishaji upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Serikali sasa hivi hizi kodi kero ambazo zimeondolewa, ina maana imekosa mapato kwa upande mmoja, lakini tukimsaidia mkulima wa kahawa akapandisha uzalishaji kilimo cha kahawa Serikali itapata mapato kupitia Kodi ya Mapato na halmashauri pia kupitia zile tozo ambazo wanatoza na wenyewe mapato yatapanda. Kwa hiyo Serikali itakuwa imepoteza kwa upande mmoja lakini ime-*gain* kwa upande mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa. Naomba nitaje takwimu chache ili kuonesha picha ya hali ya Sekta ya Kilimo katika kuchangia Pato la Taifa. Nakumbuka sekta hii ndiyo inayogusa asilimia 65 ya Watanzania, kwa hiyo ni muhimu sana hizi takwimu zikai-*alarm* Serikali kwamba tujitahidi tufanye *reform* ambayo itapelekea jitihada nzuri ya Serikali ya kuweka miundombinu ili kutupeleka kwenye uchumi wa kati, jitihada nzuri za Serikali kuhakikisha tunakuwa na uchumi wa viwanda. Ili tuweze kuwa na hiyo *socio-economic transformation* ya kubeba asilimia kubwa ya Watanzania lazima takwimu hizi tusifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo kwa miaka sasa imegota kwenye asilimia 28 mpaka 29 kama mchango kwenye pato la Taifa. Hii inatuambia kwamba tukiweza ku-*double* ukuaji wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa tutakuwa tumewasaidia Watanzania asilimia 65. Kwa hiyo, tuna kila haja ya kuhakikisha tunaisaidia hii Wizara ipate

fedha za kutosha kufanya miradi ya maendeleo ili iweze kuinua asilimia kubwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sekta hii inakua kwa asilimia 1.7 takwimu za 2016, mwaka 2005 sekta hii ilikuwa inakua kwa asilimia 5.2, unaona *trend* inarudi chini, ni lazima Serikali ifanye kila jitihada ili tuweze kurudisha hii *trend* ianze kupanda, kwa sababu kukua kwa sekta hii ndiko kunamsaidia Mtanzania ajikwamue kutoka kwenye umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni sehemu ya Azimio la Maputo, hata Kamati ya Kilimo na Mifugo wamelitaja hili. Mwaka 2016 bajeti ya Serikali asilimia 4.9 tu ndiyo ilienda kwenye Sekta ya Kilimo; mwaka 2010 ilikuwa ni 7.8, kwa hiyo unaona *trend* nayo inashuka. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Kamati ya Bajeti, kaeni tuangalie hizi takwimu zinatupeleka wapi, lazima tuzi-*reverse* hizi *trends* tuanze kuelekea kwenye kuhakikisha asilimia 10 ya bajeti ya nchi inaenda kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *disbursement* ambayo inaenda kwenye sekta ya kilimo, haiendi yote. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Kamati, kilimo peke yake *disbursement* ilikuwa ni asilimia 3.3, hii ni kidogo mno. Naiomba Serikali kabla ya mwezi Juni kwisha jitahidini angalau tuende kwenye asilimia 50 mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye mifugo kiasi kilichoenda ni asilimia nane tu, hizi takwimu ni *alarm,* inabidi tufanye *u-turn* ili tuweze kwenda kwenye *trend* nzuri ambayo itawainua asilimia kubwa ya Watanzania. Kwa kufanya hivyo, tutahakikisha miundombinu ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inaijenga kukuza uchumi inasaidia Watanzania walio wengi. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kutengeneza malighafi ambazo zitaenda kwenye viwanda hivi ambavyo tunataka kuvitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hoja hiyo ya mchango wa kilimo kwenye Pato la Taifa, sasa niende

kuipongeza Serikali kwa kuleta utaratibu wa *Fertilizer Bulk Procurement.* Utaratibu huu ni mzuri sana, naipongeza Serikali kwa sababu inaonesha dhamira yake kutaka kumsaidia mkulima aweze kupata mbolea. Katika hili, pamoja na hii jitihada nzuri, Serikali zote duniani huwa kwenye *planning* na *coordination* kwa sababu Serikali ni kubwa… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Mwalongo atafuatiwa na Mheshimiwa Lubeleje Malima.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mpaji wa yote, ambaye yeye ndiye ametuwezesha wote tuwepo humu ndani siku hii ya leo, tukifurahia maisha ndani ya nchi yetu yenye amani ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Wamekuwa ni Viongozi ambao wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa sana kwa sisi wawakilishi wa wananchi na hasa sisi tunaotoka maeneo ambayo yanajishughulisha na kilimo. Kwa kweli nawapongeza sana na nawashukuru na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu waendelee kutoa ushirikiano kwetu, tuendelee kushauriana na kusaidiana ili kuboresha maisha ya wakulima na wafugaji wetu kwa kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na chakula cha kutosha na tunaweza kuendesha nchi vizuri kwa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwakilishi wa wananchi kutoka Jimbo la Njombe Mjini, jina hili mjini ni jina

tu lakini Jimbo langu mimi lina Halmashauri moja lakini lina Tarafa mbili. Tarafa moja ni ya mjini lakini Tarafa nyingine ni ya vijijini na ina kata kumi na tunajishughulisha na kilimo barabara. Moja ya mbinu za kilimo ambayo tunatumia ni vinyungu. Wiki iliyopita *headlines* nyingi sana za habari hapa nchini zilizungumzia vinyungu na leo naomba niongee habari ya vinyungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna Mbunge amesema yeye amekuzwa kwa pamba na samaki na mimi nasema nimekuzwa kwa vinyungu. Kila mwananchi anayetokea Mkoa wa Njombe na yeye amekuzwa kwa vinyungu. Vinyungu sisi kwetu ni kilimo muhimu sana. Hizi sheria zinavyotungwa ni vizuri sana zikafanyiwa utafiti wa kutosha, kwa sababu unapotuambia watu wa Njombe tusilime vinyungu, sisi tunasema na mpunga usilimwe, kwa sababu mpunga ndiyo unaolimwa mabondeni na mpunga ndiyo unatumia maeneo makubwa zaidi kuliko vinyungu. Kwa hiyo kwa kutuambia sisi tusilime vinyungu tu ni kutuonea na kutufanya sisi tuendelee kuwa maskini bila hata sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wataalam, sawa najua kuna Sheria ya Vinyungu inayosema tusilime mita sitini kutoka kwenye mtiririko wa maji, lakini maji hayahifadhiwi bondeni, maji yanahifadhiwa mlimani, ndiyo maana wote tunaokumbuka miaka ya nyuma baada tu ya uhuru na miaka mingine kidogo, kilimo chochote lazima mkulima alime makinga maji ndani ya shamba lake. Makingamaji ndiyo yanayohifadhi maji kwa sababu maji yale yatakuwa hayatiririki yote na kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wetu wa kilimo leo hawaelekezi wakulima juu ya makingamaji, watu wa mazingira na wenyewe wameng'ang'ana tu kuhusu mita sitini. Ninachosema, mita sitini itakuwa ni kuwanyanyasa wananchi na kuwafanya wafe na njaa, lakini kama ni kweli maji yanahifadhiwa bondeni basi na mpunga usilimwe kwa sababu wenyewe ndiyo unaotumia maeneo makubwa zaidi ya mabondeni. Nafikiri ujumbe huo umefika, Mheshimiwa Waziri, naamini hata huko Mwanza nina imani kutakuwa na

vinyungu tu, haiwezekani kusiwe na vinyungu, Tanzania nzima tunalima vinyungu wataalam waangalie upya utaratibu wa kuhifadhi maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya suala la vinyungu sasa niongelee suala la mifugo. Nilikuwa najaribu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuna mambo yamenisikitisha sana. Tuna tatizo kubwa sana la ng'ombe wa maziwa, ng'ombe hawa ndio ambao wanaweza wakawa na manufaa makubwa sana kwa wakulima walio wengi, lakini idadi ya ng'ombe wa maziwa ni wachache mno na uzalishaji wetu uko chini mno, sasa unajiuliza, mashamba yote haya kwa nini hayazalishi ng'ombe. Mheshimiwa Waziri mwenyewe katika hotuba yake amekiri kwamba maziwa yamepungua kwa asilimia 2.3 na anasema kwamba moja ya matatizo ni kukosekana kwa malisho, kuna ukame na malisho yamepungua, ukweli ni kwamba hata uzalishaji wetu wa malisho ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Watanzania lazima tuangalie kwamba tunataka kufanya nini kwenye kilimo, tunataka kufanya nini kwenye mifugo. Mifugo ina uwezo wa kuwaajiri vijana wengi sana. Leo hii kuna watu wanalima nyasi wanasafirisha nje ya nchi, hivi hatuwezi kweli kuanzisha ma-*block* makubwa ya kulima nyasi na tukaweka vifaa vya kutosha na vijana wakafanya hizo kazi. Tatizo kubwa tulilonalo ni kwamba tunawaambia vijana waende shamba, kijana wa leo ameelimika hawezi kwenda kushika jembe kwa mkono, ni lazima tuhakikishe kwamba tunaweka vifaa na mazingira wezeshi ili vijana wale wasimamie hayo mashamba kwa urahisi, lakini tunavyosema tu waende shamba hawataweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wangeweza kulima nyasi za kutosha, wakazifungasha na wakazisafirisha, lakini vilevile wakapeleka maeneo mbalimbali ambayo yana uhaba wa nyasi na mifugo ikapata nyasi. Sisi tunazalisha nyasi viroba 684,000, viroba 600,000 ni nyasi za ng'ombe 900 kwa mwaka, sasa ng'ombe 900 watatupeleka wapi? Kwa hiyo, niiombe sana Serikali ilione hilo, ianze kuweka mpango

maalum wa kuhakikisha tunakuwa na mashamba makubwa ya nyasi ambayo yatakuwa na vifaa vya kutosha kwa ajili ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watendaji wa Mheshimiwa Waziri kidogo nao wameteleza. Katika ukurasa wa 106 wanaeleza kwamba kuna kiambatanisho cha viwanda vya maziwa, naomba waangalie hapo kwenye kielelezo hicho kama kinaelezea maziwa, maana yake kielelezo kilichopo katika ukurasa huo kinaeleza habari ya mbegu mama. Sasa sisi wenye *interest* na viwanda vya maziwa tunapata taabu sana kujua. Kwa hiyo, kama taarifa hizo zipo tunaomba watuletee tuweze kuziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, kwanza tuongeze uzalishaji wa mitamba hii lakini pia tuongeze ukubwa wa mashamba kwa ajili ya malisho. Kwa sababu tunazalisha mitamba michache sana kwa mwaka, mwaka ambao ilizalishwa mitamba mingi ni kati ya mwaka 2011 na 2017 ambapo ilizalishwa mitamba 800 kwa nchi nzima, nchi kubwa namna hii hatuwezi kuzalisha mitamba kiasi kidogo namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye usindikaji wa maziwa lipo tatizo. Tatizo ambalo mimi naliona sasa hivi tumeingiza *VAT* kwenye mtindi. Sasa viwanda hivi, kwa mfano pale Njombe tuna Kiwanda cha maziwa kinaitwa *CEFA,* kiwanda kile ni cha wafugaji, ni kiwanda cha ushirika, tumeingiza *VAT* kwenye mtindi, matokeo yake wananchi wale hawapandishiwi bei ya maziwa kwa sababu kiwanda kinaingia gharama. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie sana hilo kama kweli tuna nia ya kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la kilimo, upimaji wa udongo; tunahangaika na mbolea sawa, mbolea ni muhimu sana kwa ajili ya kilimo na nini lakini lipo suala la msingi zaidi, ni lazima udongo wetu ujulikane, kwa sababu mbolea ni dawa, kwa hiyo tunatibu nini katika udongo wakati hatujui kwamba udongo unaumwa nini. Kwa hiyo, ni vizuri sana Serikali ikaona kwamba, ni kwa namna gani

sasa kila halmashauri lazima iwe na kifaa cha kupimia udongo, hata kifaa kile kidogo tu ili kusaidia kupima udongo. Wataalam wamesema chokaa ya kilimo ndiyo chokaa inayoweza kusaidia kurekebisha udongo, hapa Dodoma kuna mgodi lakini sijaona kama Serikali iko *serious* na ule Mgodi wa Chokaa ya Kilimo. Chokaa hii tuichukue tuisambaze kwa wakulima ili waweze kuongeza mapato yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana za kilimo; hatuwezi kwenda kwa jembe la mkono, hata siku moja, lakini hata haya matrekta yenyewe ambayo tunayapata, ubora wake ukoje. Leo hii ukienda hapo Kilimo Kwanza, ukiyaona yale matrekta labda yana miaka mitatu au minne jinsi yalivyomomonyoka yanatia huruma. Unaona kabisa kwamba hata kama kuna uzembe katika matumizi lakini hata ubora uko chini. Naomba sana, wanaoshughulika na matrekta wahakikishe kwamba matrekta yanakuwa bora na wananchi wanaweza wakayapata matrekta hayo wakayatumia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mikopo ya matrekta na yenyewe siyo rafiki kwa wakulima. Unamwambia mkulima alipe asilimia 50 halafu asilimia 50 iliyobakia ndani ya mwaka mmoja, ni mkulima gani atakayeweza namna hiyo, kwa hiyo hilo nalo ni jambo gumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu suala la mbolea. Naipongeza sana Serikali kwa mpango inayokuja nao. Angalizo ambalo naomba niiambie Serikali yangu ni kwamba, lipo tatizo, sasa hivi wenye mbolea (*importers* wa mbolea) tayari wana mbolea kwenye ma-*godown.* Serikali itakaposema mbolea kwa utaratibu huu ambao inaelekeza sasa watakwambia hiyo mbolea inayokuja Mheshimiwa Waziri tunaomba tuiuze mwakani kwa sababu sasa hivi *stock* imejaa. Kwa hiyo bei itabaki palepale na wananchi wataendelea kuumia. Kwa hiyo, niombe sana, kama kweli mchakato huu upo, umekaa vizuri, fanyeni haraka inavyowezekana ili wananchi waweze kupata mbolea kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tozo, Mheshimiwa Waziri ameondoa tozo nyingi sana, kweli zinaonekana zina manufaa, lakini nimwombe sana sisi tunaotoka maeneo yanayolima chai wameondoa tozo ya Vyama vya Msingi vya Wakulima ya Sh.500/= kwa kilo. Hii tozo aliyoondoa haimnufaishi mkulima na wala haitakaa irudi kwa mkulima, hii ni tozo ya majani makavu kiwandani. Ilikuwa ni tozo ambayo viwanda vilikuwa vinarudisha kwenye Vyama vya Msingi ili kusudi vyama vile viweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa unahitimisha hotuba yake atuambie hii Sh.5/= aliyotoa, je, Vyama hivi vya Msingi vitaendeleaje kufanya kazi kwa sababu hotuba ya Kamati imesisitiza kuimarisha ushirika, anapouondolea ushirika tozo hii anaufanya ushirika ukose uwezo wa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Wanafanya kazi nzuri lakini katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo matatu; kwanza. nitaanza na suala la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania *(TALIRI).* Taasisi hii ina vituo saba; kuna kituo cha Mpwapwa, Mabuki, Kongwa, Tanga, Naliendele na Uyole, lakini mimi nitazungumzia Kituo cha Utafiti wa Mifugo Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki kilianzishwa mwaka 1905, sasa hivi umri wake ni zaidi ya miaka 100. Hata hivyo,

Kituo hiki kinakabiliwa na changamoto nyingi sana, kituo hiki ndicho kinachohudumia wafugaji Kanda ya kati, Mikoa ya Singida na Dodoma kwa sababu wanakwenda kuchukua madume bora, wanakwenda kuchukua majike yale ambayo yana mimba kwa ajili ya kufunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 na 1993, Serikali ilipunguza watumishi, lakini bahati mbaya sana Serikali ilipunguza wahudumu wote. Kwa hiyo, hata wale wahudumu wachungaji wote waliondolewa, wakamuaji wa maziwa waliondolewa, kwa hiyo wakabaki watafiti tu. Sasa najiuliza, Mheshimiwa Waziri, kama wahudumu wote walipunguzwa kazi na kituo kile kina ng'ombe zaidi ya 800, kina Mbuzi zaidi ya 400, ni nani atakaechunga? Au watafiti watapanga zamu ya kuchunga na kwenda kukamua? Wasomi wenye *degree mbili, degree tatu;* kwa hiyo wapange ratiba nani leo aende akachunge, nani leo aende akakamue, ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapoamua mambo mengine kwa kweli wawe wanafikiria, wanaangalia uzito wa jambo. Sasa unapoondoa wahudumu; na namshukuru sana Mkurugenzi wa Taasisi, aliajiri vibarua 90, akawapanga wengine wanachunga, wengine ndiyo wanakumua na wengine wanafanya *bush clearing* yaani kusafisha mashamba yale ambayo mifugo wanachungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. Hawa vibarua wameanza kazi tangu mwaka 2015 mpaka leo hawajalipwa mishahara yao; wana familia, wanasomesha. Kwa hiyo naomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hawa vibarua wanafanya kazi nzuri, kwa sababu kama Mkurugenzi asingeajiri vibarua hii kazi ya uchungaji, ukamuaji ni nani angefanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna changamoto zingine; kuna upungufu wa magari, matrekta pamoja na pikipiki kwa ajili ya wale *Extension Officers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuhusu kuhamisha kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo na kukileta Dodoma. Mheshimiwa Waziri naomba anisikilize vizuri sana; Mawaziri wote wa mifugo waliopita akiwemo Mheshimiwa Rais Magufuli aliwahi kuwa Waziri wa Mifugo alikataa ile Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa isihamishiwe Dodoma. Sasa walipoona Mheshimiwa Lubeleje mwaka 2010, 2015 amepata likizo siyo Mbunge wakaihamishia haraka haraka Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Dodoma hakuna majengo ya Maabara. Pale Mpwapwa kuna jengo zuri, mwaka juzi wamejenga jengo zuri sana la Maabara, kwa hiyo wamehama vifaa vingine wamekuja navyo Dodoma, vingine wamefungia kwenye *stoo* pale Mpwapwa; yale majengo Mpwapwa yanaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na sababu gani ya kuhamisha kile kituo? Kwa sababu waliojenga kituo cha utafiti wa mifugo Mpwapwa ndio waliojenga Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa kwa sababu vinakwenda pamoja. Ng'ombe akiugua kwenye Taasisi ya utafiti analetwa pale *VIC* kwenye Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa wanamchunguza ana tatizo gani, lakini baadaye wamejenga chuo cha Maafisa wa Mifugo kwenye Chuo cha Mifugo ili *practicals* wawe wanachukua pale *VIC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale chuo cha mifugo wanasoma *theory* lakini *practicals* walikuwa wanafanya hapa Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa, maana hawa ni wataalam wa mifugo; wanasoma *anatomy physiology, animal deseases* pamoja na *meat inspection;* sasa *practicals* lazima wakafanyie pale Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa hata *meat inspection,* maana wale wanajifunza *ant-mortem inspection* na *post-mortem,* sasa *practicals* lazima wakafanyie kwenye Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapochukua yule ng'ombe wanaanza kumchunguza ana tatizo gani, amekufa kwa ugonjwa gani. Kuna vidudu vingine vya magonjwa ya

mifugo vinaonekana kama *liver flukes, Cysticercus bovis* vinaonekana, vile vile kama *anthracis bacillus* na *Tubercle bacilli* mpaka utumie darubini kali. Sasa ninyi wanahamisha kituo kile wanaleta Dodoma, hao wanafunzi wawe wanatoka Mpwapwa wanakuja kujifunza Dodoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri arudishe kituo kile haraka sana Mpwapwa la sivyo leo nashika shilingi. Kuna mtaalam mmoja pale ndiye aliyelazimisha kituo kihame, akasema Lubeleje ndiye Mbunge ambaye anazuia sasa ameondoka na bahati mbaya amestaafu, ndiye amelazimisha kituo kuhamia hapa. Sasa Waziri anieleze ametenga fedha kiasi gani, wanafunzi watoke Mpwapwa kuja kuchukua *practicals* huku Dodoma? Kwa hiyo, naomba anieleze Mheshimiwa Waziri mpango wa kuhamisha kituo hiki kirudi Mpwapwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni upungufu wa chakula katika Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma. Mheshimiwa Waziri alitoa kauli ya Serikali hapa Bungeni kwamba kuna Halmashauri 55 zina upungufu wa chakula, alikiri mwenyewe hapa na alisema kwenye maghala yetu ya hifadhi kuna chakula cha kutosha lakini nashangaa hawakugawa hata gunia moja kwenye vijiji ambavyo vimeathirika na chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tunasema majimbo yetu yana njaa, yana upungufu wa chakula tunaomba watusikilize. Sasa kama chakula kiko kwenye maghala na hapa tunapitisha, mwaka wa jana tumepitisha bajeti bilioni 18, zimetolewa bilioni tisa, hizo bilioni tisa ndizo zimenunua chakula kwahiyo kama chakula kidogo kipo, basi wasambaze kwa maeneo ambayo hakuna chakula ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje muda wetu ndio huo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Naomba nimalizie dakika moja, *one minute please!*

**MWENYEKITI:** Hapana, malizia tu hiyo sentensi yako

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba wagawe hicho chakula ili wananchi wasiweze kununua debe la mahindi kwa Sh.25,000/= na gunia la mahindi kwa Sh.120,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, wamekuelewa na wamejua *background* yako wewe ni nani. Tunaendelea, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na Mheshimiwa Salome Makamba wajiandae

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hii Wizara muhimu ya Kilimo. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa bajeti nzuri. Pia napongeza na uchambuzi wa Kamati, kwa kweli wamekuwa makini sana Kamati, wamekuja na *report* nzuri sana ambayo imetusaidia hata katika huu mchango nitakaoutoa mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kwa kipekee kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa juhudi ambazo wanazifanya kuondoa zile changamoto zilizopo kwenye mazao yetu na hasa zao la pareto kule Mbeya, naona sasa hivi kuna kiwanda kimeanzishwa pale Inyala ambacho kimeongeza ushindani lakini nina imani kuwa zile changamoto ndogo ndogo ambazo zimebaki wanaendelea kuzishughulikia ili tuondokane na zao la pareto kutoka leo chini ya tani 3,000 twende mpaka tani 8,000 ambazo ndiyo *potentials,* tunaweza kuzalisha Tanzania. Vile vile waendelee kuboresha bei ya pareto kutoka hii iliyopo sasa hivi ya

Sh.2,500/= ifike angalau Sh.4,000/= kwa kilo, ambayo nafikiri itamsaidia hata wale wauzaji wa nje wanaweza nao kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Waziri kwa *report* yake hii ambayo ameonyesha ni namna gani inalenga kuwasaidia wakulima kupata pambejeo kwa bei nafuu. Ni kweli kabisa pembejeo au mazao ya kilimo hata mashirika ya nje yanaangalia kwa karibu sana ni namna gani wamsaidie mkulima. Wenzetu ambao ni wanunuzi wakubwa kule nje na wazalishaji wakubwa wanaangalia ni namna gani mkulima wasimnyonye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nampongeza Waziri kwa vile umelisema mwenyewe katika ukurasa wa 51, ambapo ameelezea kuwa mwenendo wa bei za mbolea katika soko la dunia zipo kwenye viwanda vichache na zinauzwa kwa bei ya chini katika muda muafaka, hilo ni zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na hii *bulk procurement* ya *fertilizer.* Hata hivyo, inabidi tuangalie, je, ni peke yake Wizara ya Kilimo atafanikisha mkulima apate hii faida? Bila kuungana na wenzako hii haitafanikiwa kwa sababu *(value chain)* ya mbolea ni ndefu mno na hapa kwetu bei ya mbolea haitokani peke yake na bei ya kununulia *(CIF),* inatokana na gharama kubwa za usambazaji kuanzia Bandarini. Bei ya kununulia ni asilimia 53 tu lakini bei ya ukiritimba wa usambazaji kutoka Bandarini, tunatumia magari, barabara zetu mbovu inachangia hiyo asilimia nyingine 47. Sasa ukija kuchanganya na kwa vile mbolea tunanunua nje, kama hatutaweza kudhibiti mfumuko wa *exchange rate* ina maana vile vile hatutawasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi ambacho kinaweza kutusaidia ambacho naiomba Seriakli ijaribu kutusaidia, ni namna gani tupunguze gharama hii ya asilimia 47 ambayo ni mzigo mkubwa sana kwa mkulima. Kwa sababu ukilinganisha na wenzetu wa Ufilipino, ni asilimia chini ya 10,

ukienda kanchi kadogo kama Myanmar ni asilimia chini ya 20, sasa sisi kwanini mkulima achangie asilimia 47 ya bei ya *CIF?* Inamuumiza sana mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri na timu yake wakae chini na Wizara ya Miundombinu, mahali kama Mbeya huhitaji kusafirisha mbolea kwa magari, ni gharama kubwa. Tani moja inakwenda zaidi ya 100,000 na ikifika pale inabidi iende kijijini. Kwa nini hiyo mbolea ikija kwa *bulk* itoke kwenye meli iingie kwenye mabehewa ya *TAZARA*, tuwe na bandari kavu Mbeya ili tuweze kusambaza Ukanda mzima wa Nyanda za Juu na *packing* ifanyikie pale Mbeya na si Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo itasaidia vile vile na mazao mengine ambayo kahawa sasa hatutakuwa na sababu ya kuipeleka bandarini, tutaisafirisha kwenye Ulaya kutoka kwenye Bandari kavu pale Mbeya. Hii itapunguza gharama na mzigo mkubwa kwa mkulima. Kwa hiyo namwomba sana ndugu yangu, anafanya jitihada kubwa, zimeshaonekana na leo hii watu wanasifia hizo tozo ambazo zimepunguzwa, kama kwenye kahawa, ni lini zitaanza na nina imani kuwa zinaanza mara moja, wakulima wamefurahia na kweli hiyo itatupunguzia mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kilimo chetu tunakuwa maskini wakati mwingine kwa sababu wataalam hawatusaidii vizuri. Ukilima vizuri hekta moja ya mahindi unaweza kutumia mifuko kama mitano ya mbolea na huhitaji hata kulima kilimo cha hifadhi ardhi. Unachohitaji ni kuweka mbolea muafaka ambayo inalingana na udongo, na siyo lazima iwe *Urea* ama *DAP*. Hilo nalo Waziri ajaribu kuliangalia kwa vile sasa tumebadilika, hatulimi tena kwa kupandia na *DAP,* hatulimi tena kwa kukuzia na *Urea.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha sasa hivi tunachotumia, nikitumia mbolea labda *ya NPK 17-17-17 or NPK 15-15-15,* nina uwezo kwa hekta moja kupata kilo 13,000 ambazo zinaweza kuniletea milioni 12 kwa hekta. Kwa mkulima wa kawaida ambaye amelima, ametumia mifuko

mitatu mingine anauwezo wa kupata kilo 6,000 na akapata milioni tano. Vile vile mkulima atakayelima kwa hizi mbolea ambazo nazisema, atapata kilo 1,800 ambayo ni hela kidogo sana, inamwendeleza kuwa masikini. Kwa hiyo hapa suala siyo mbolea tu na mbolea ni tofauti na *petrol.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ni *product* kutokana na udongo. Tunahitaji hii *lime* inayozalisha hapa Dodoma iletwe Mbeya iboreshe ili wakulima waweze kupata kilo 13,000 kwa hekta. Ni zao zuri sana, limejaribiwa na uzuri wake hata kile Chuo cha Kilimo Uyole, waliwapeleka wakulima kwa mkulima mmoja Iringa, tumekuta yule halimi yeye ardhi ile; anapanda kisasa, anatumia mbolea kisasa na tumeangalia kwa macho yetu kulinganisha na mashamba ya jirani yake na hiyo ni Wizara iliyotupeleka pale. Sasa kwa nini tusielekee hiyo kwa ajili ya kumsadia mkulima? Hiyo ndio itakayotusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii bila kumsaidia mkulima umaskini utaendelea kututesa na kilimo tukifanye cha kijasiriamali mno, cha mahesabu. Tusiseme tu ya kwamba tutaleta *DAP* na *UREA*, tuseme ya kwamba kwenye eka moja utazalisha nini? Utaondoka vipi kwenye umaskini huu tulionao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani tukilifuatilia hilo kwa sisi tunaotoka kwenye majimbo ya kilimo, tunalima viazi; ukilima kisasa unakuwa tajiri, ukilima mahindi unakuwa tajiri, ukilima kahawa unakuwa tajiri na haya mazao yetu yana bei nzuri huko duniani kuliko kwingine. Ni *competitive* kwa sababu ukiangalia kahawa ya kwetu ni changamoto tu zinafanya bei inakuwa ndogo kuliko Kenya au Ethiopia. Ukiangalia mahindi ni changamoto tu zinafanya bei inakuwa ni ndogo kuliko ya Zambia. Tunaomba Serikali iwe na mkakati na iangalie ni namna gani itaondoa hilo ili tuweze kumsaidia mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine nitachangia kwa maandishi. Naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yake. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa hiyo naungana moja kwa moja na mapendekezo ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi takribani asilimia 67 mpaka 70 wameajiriwa kwenye sekta hii ya kilimo. Kwa hiyo, kama Serikali imedhamiria kweli kutupeleka kwenye Uchumi wa Viwanda tunatakiwa kuongeza bajeti kwenye sekta hii ya kilimo. Badala ya bajeti hi kukua bajeti hii inaendelea kupungua kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sikubaliana na kuendelea kuipunguza hii bajeti, naomba Serikali iliangalie kwa jicho la huruma, kwamba eneo hili ndio eneo pekee ambalo linatoa ajira ambayo haina shaka katika nchi hii. Kwa hiyo ni vyema tukaongeza bajeti kwenye eneo hili kusudi watu walioajiriwa kwenye eneo hili waendelee kupata *facilities* kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na pendekezo la Serikali la ununuzi wa pembejeo kwa pamoja *(bulk procurement)*. Tumeona kwenye mafuta tumefanikiwa sana na naamini kwenye pembejeo vile vile tutafanikiwa sana kwa ajili ya hii *bulk procurement*. Hii itatusaidia pembejeo itanunuliwa kwa wingi na naamini zitafika kwa wakati kwenye *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kule kwetu Mufindi, ukipeleka pembejeo baada ya mwezi wa Tisa, wakulima hawawezi kulima. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri ambaye amelileta pendekezo hili kwenye Kamati yetu na sisi tumelikubali na Waheshimiwa Wabunge

naamini tutalikubali kwamba hizi pembejeo zinunuliwe kwa wakati na zifike kwenye *site* kwa wakati. Pia tunaamini kwamba Serikali itakapopata kazi ya kununua hii, hakuna matatizo tena ya bei kwenye hizi pembejeo. Kwa sababu kuna watu walikuwa wanajipatia faida bila sababu. Kwa hiyo, nina hakika kabisa watu wetu wa Mufindi watalima wakiwa hawana shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni Benki ya Kilimo. Tuna benki ya kilimo na takribani ina miaka minne lakini benki hii haikui. Kwa hiyo, kusudi tuwasaidie wakulima walio wengi katika *site* kule ni vyema Serikali ikaongeza mtaji kwenye hii benki. Mtaji huu utawasaidia wakulima wadogo wadogo kukopa kwenye eneo ambalo halitakuwa lina *interest* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tunaiomba sana Serikali ifungue matawi kwenye *site.* Unakuta benki ya kilimo matawi yapo Dar es Salam, Arusha, yako wapi, kule *site* kwenye wakulima wadogo wadogo wa viazi, wakulima wadogo wadogo wa miwa, hatujafungua benki za kilimo. Wakulima wadogo wadogo wa nyanya kama vile ukienda kwenye majimbo ya wenzetu kama ya Kilolo, Ilula, Mufindi na Mdabulo. Tunaomba sana Serikali ifungue matawi kwenye maeneo haya na ihakikishe mikopo inaendelea kuwa kwa riba nafuu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo nyuma, azma ya Serikali ni kutupeleka kwenye uchumi wa viwanda. Ukitaka kuangalia kwa haraka haraka, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ni watoto pacha ambao wanakwenda *simultaneous*. Kwa hiyo, bado naendelea kusisitiza tu kwamba hatutapata mafanikio ya kutosha kama hatutawekeza kwa kiasi kikubwa kwenye eneo hili la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la *SAGCOT*, hawa wenzetu wa *SAGCOT* ambao wanawasaidia wakulima wadogo wadogo wamejielekeza kwenye maeneo machache, tunaomba

wafike kwenye maeneo mengine hata maeneo ya kule Mufindi. Wakifika kwenye maeneo haya, watasaidia sana kuhakikisha watu wanaboresha miundombinu na wanapata masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu katika Wilaya yetu ya Mufindi Jimbo la Kusini na Kaskazini ni wakulima wakubwa sana wa chai. Kwa masikitiko makubwa, chai imekuwa inaharibika, inapotea, kwa sababu hatuna miundombinu ya uhakika. Wananchi wameshaanza kukata tamaa kwenye maeneo haya, kwa sababu wamelima chai na chai ni kilimo cha muda mrefu hawajui wafanye nini. Kuna baadhi ya watu wameshaamua kwamba wakate ile miti ya chai wapande mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri; *last time* alikuwa mgeni rasmi kwenye mkutano mkubwa wa chai lakini hakufika. Namwomba Mheshimiwa Waziri afike kwenye *site* aone adha wanayoipata wakulima wa chai katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo tuliyokuwa nayo ya chai katika Wilaya ya Mufindi na Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa kwa ujumla, kwa maana ya Kilolo ni makubwa sana na kama yatahudumiwa vizuri tutalima chai nyingi kuliko wanavyolima wenzetu wa Kenya. Kwa hiyo, utaalam unatakiwa uongezwe katika maeneo haya. Ni aibu kuona chai ya Mufindi, Kilolo na Njombe soko lake linaenda kufanyiwa Mombasa kwenye Taasisi inaitwa *KATEPA*, wakati *TATEPA* hapa Tanzania haifanyi juhudi za kutosha. Hatuna sababu ya kuendelea kutumia masoko ya wenzetu, wakati sisi wenyewe tunatakiwa tujiangalie na tuimarishe masoko yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala ambalo limekuwa tatizo la muda mrefu, madai ya mawakala. Mawakala wanadai hela zao muda mrefu sana na kuna baadhi ya mawakala wengine wameshaanza kupata matatizo, wengine wameshaanza kufa na wengine wameshaanza kuuziwa *assets* zao ambazo

walizitumia kupata mikopo. Kwa hiyo, atakapokuja Mheshimiwa Waziri aje na majibu hapa. *Last time* waliambiwa wamwone Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini mpaka leo hii mawakala wapo hapa Dodoma wanataka wasadiwe kwenye hili eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni eneo la kilimo cha umwagiliaji pamoja na kilimo cha vinyungu. Wilaya ya Mufindi hekta 350,000 zimechukuliwa na Maliasili; kwa hiyo watu wengi katika Wilaya ya Mufindi wanalima katika vinyungu, hawana ardhi. Ukiwaambia wasilime kwenye vinyungu hawana sehemu yoyote ya kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri alione jambo hili. Hata siku zile wakati tunaomba kura tulikuwa na lengo, kwamba tuwasaidie na wapiga kura wengi ambao walitupa kura ni kutoka katika eneo hili la vinyungu. Sasa leo hii unawaambia watu kwenye vinyungu wasilime, wakalime wapi hawa watu? Leo unawaambia wasilime kwenye vinyungu wakalime wapi? Mbadala wake ni nini? Labda kuna lengo hapa hamtaki Kigola, Chumi na Mgimwa warudi kwenye majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri atakapokuja, kama kweli Serikali wameamua sisi tusilime kwenye vinyungu, watuambie mbadala wake tuujue hapa leo hii. Kwenye jambo hili tutashika shilingi. Kwenye jambo hili Mheshimiwa Tizeba ni rafiki yetu lakini hatutamwangalia kwa sababu tukiendelea kumbembeleza kwenye jambo hili sisi ndio tutakuwa si Wabunge tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili, ndiko tunategemea kupata viazi vya uhakika, kwenye eneo hili tunategemea kupata mpunga wa uhakika na kwa eneo hili tunategemea kupata miwa. Sasa badala ya kuongeza ajira

kwa watu, tunataka watu wengi wawe majambazi. Hoja ya kuwaambia leo hii watu waondoke kwenye vinyungu sisi hatukubaliani nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuna jambo sasa hivi linaendelea, naomba Mheshimiwa Waziri kwa mamlaka aliyonayo alizuie. Kule kwetu sasa hivi wameshaanza kufyeka mahindi kwenye vinyungu. Kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aseme na watu wanahitaji elimu. Namwomba sana Mheshimiwa Tizeba atuangalie sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda ndio huo Mheshimiwa, malizia.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nameomba sana Mheshimiwa Tizeba, atakapokuja kuhitimisha hotuba yake hapa atuambie mbadala wa vinyungu ni nini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Kuchauka ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuwawakilisha wananchi wangu wa Shinyanga katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyeki, napenda kuongea na Mheshimiwa Waziri na kumwomba atusaidie matatizo ya ushirika pale Kahama. Mheshimiwa Waziri wote tunafahamu Sheria ya Ushirika namba 20 ya mwaka 2003 inasema wazi kwamba Ushirika ukifilisika mali zake zitakwenda katika Ushirika mwingine. Hilo limekuwa likifanyika tangu mwaka 1984, mwaka 1986, lakini cha kushangaza hivi karibuni pale Kahama Chama cha Ushirika kimepewa Kampuni. Wamepewa Kampuni kinyume na utaratibu na Mahakama imetengua lakini mpaka leo Chama kile cha Ushirika

kimeng'ang'aniwa na Kampuni na wale wananchi ambao walijiunga pamoja, ambao ni wakulima wadogo wadogo wakatengeneza Ushirika, wakajenga vibanda, wamenyang'anywa maeneo yao. Suala hili nimeshalipigia kelele mara nyingi humu Bungeni na hakuna msaada wowote unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alitazame jambo hili kwa jicho la pekee. Wale wakulima ni watu ambao ni wanyonge, hawana pesa, hawawajui watu wakubwa, lakini kwa sababu walioko pale ni mapapa, ni mafisadi, wamewanyang'anya maeneo yao wale watu, vibanda zaidi ya 200 vimechukuliwa, soko lile limemilikishwa kwa mtu mmoja ambaye ndiye mwenye hisa nyingi kwenye Kampuni ile na wale watu wanakosa pa kukimbilia. Namfahamu vizuri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Tizeba ni mtetezi wa wanyonge. Namwomba sana aje kwetu pale atusaidie kutatua tatizo hili kwa sababu limekuwa ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wale watu wakihoji kuhusu Ushirika Mheshimiwa Waziri wanakamatwa, wanaenda kuwekwa ndani, wanaanza kuhojiwa, wanatishwa, vitisho hivyo ni unyanyasaji kwa raia wanyonge wa Tanzania hii. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie kutatua tatizo la ushirika kwa sababu limezidi, kwanza ni kinyume cha Sheria, Mahakama imeshatengua Kampuni ile kumiliki, ile hati iliyopo pale ya Kampuni imetenguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza wanatakatisha hati ile, wanafanya kui-*renew* ili ionekane kwamba ni hati halali. Kweli tatizo hili limezidi, limekuwa la muda mrefu lina miaka zaidi ya 27, tunaomba Mheshimiwa Waziri tafadhali aje atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo niongelee suala la upigaji chapa ng'ombe, tumezinduliwa mradi sasa hivi wa kupiga chapa ng'ombe. Wanasema ni kwa ajili ya sababu za kiusalama wanataka kutambua ng'ombe na wale

wanaokuja kutoka nchi za jirani. Hata hivyo, wanasema upigaji chapa hawa ng'ombe gharama yake ni Sh.3,000/= kwa kila ng'ombe. Sisi Wasukuma tunasifika kwa ufugaji. Familia za vijijini Sh.3000/=, Sh.1,000/= ya kula tunahangaika kutafuta hiyo Sh.3,000/= tutaitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndizo tozo za kero ambazo zilipigwa marufuku na Mheshimiwa Magufuli. Kama wanaleta mradi basi watafute namna ya kuutekeleza mradi ule bila kuwaumiza wananchi na Mheshimiwa Waziri anafahamu kabisa kwamba kupiga chapa ng'ombe kunashusha thamani ya ngozi ile inapotakiwa kuuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunasema tunakwenda kwenye Tanzania ya Viwanda, tunasema tuwakwamue wananchi kwenye umaskini, leo tunaenda kuwapiga chapa ng'ombe wao na tunawatoza Sh.3,000/=. Tunaomba majibu tunahitaji kujua ni njia gani itatumika kuwapiga chapa bila kuwabughudhi, bila kuwakera wakulima hawa ambao ufugaji kwao ni biashara, ufugaji ni maisha, lakini ufugaji kwao ndiyo chakula cha kila siku na ndio utamaduni wetu vile vile. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie sana majibu juu ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la punda. Usukumani punda wanatumika kwa ajili ya kubeba mizigo, maji, ndio usafiri kule kwetu. Hata hivyo, hivi leo nikikueleza punda wanauawa, punda wanauzwa, wamekuwa ndio biashara. Mheshimiwa Waziri, China wanabiashara ya ngozi, wananunua ngozi hizi za punda na wanatengeneza *anti aging*, dawa ambayo inayozuia kuzeeka na inaongeza nguvu za kiume pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri, biashara hii…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umesemaje? *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la punda lina dawa ambayo inatumika kule China kupunguza kuzeeka, lakini pia inaongeza nguvu za kiume. Kwa sababu hiyo thamani ya punda ni Sh.50,000/= mpaka Sh.190,000/=, lakini thamani ya ngozi ya punda ni *pound* 160, ngozi peke yake. Juzi Mheshimiwa Mwijage wakati anapitisha bajeti yake hapa alisema amepiga marufuku uuzaji wa punda. Hii haitoshi, tunatakiwa tuisimamie kama tunavyopiga marufuku mambo ya pembe za ndovu na biashara nyingine, kwa sababu hii itapelekea kupotea kwa hawa punda ambao ni mifugo tunayoitegemea sisi kama njia ya usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeamua kuingia kwenye biashara hiyo basi tuwe na *mechanism* ya kuongeza hawa punda wawepo wawe ni wanyama wa biashara, waongezeke tuwe na jinsi ya kuboresha, kwa sababu hii mifugo iko chini ya Wizara yako na hii mifugo sisi tunaitumia kama njia ya usafirishaji kule kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia wana mifugo milioni 7.5 hii ya aina ya punda, lakini kuna nchi ambazo zimepiga marufuku na wameweka sheria, nchi kama Burkina Faso, Niger na Pakistan wameshaweka Sheria. Kusema tu haitoshi, tunafungua mianya ya wale watu ambao watakuwa wanafanya ujangili wa mifugo hii. Tusifungue mianya kwa sababu hatimaye itatuathiri sisi wenyewe. Tuweke sheria ambazo zitazuia, lakini kama unataka kufanya biashara hiyo na wafanye kwa njia halali na kuwe na misingi ya kuzuia upotevu wa wanyama hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu kwa kweli Ushetu, Tarafa ya Mweli hakuna hata josho, tarafa nzima ina kata karibu sijui ngapi, hakuna hata josho la kuoshea ng'ombe. Sasa bajeti ya Kilimo na Mifugo haifiki hata trilioni moja na tunategemea eti huu uti wa mgongo wa Kilimo Kwanza; sijui hata hiyo sera iliishia wapi; tunategemea eti malighafi itokane na mazao wa kilimo na mifugo, eti uti wa mgongo wa nchi hii ni kilimo, wakati huo huo hata bajeti yenyewe haiakisi malengo ya nchi hii ya Tanzania ya kutokana na

malighafi za kilimo na mifugo. Hivi kwa nini tuendelee kuwadanganya Watanzania? Mimi sina wasiwasi na ukusanyaji wa kodi katika nchi hii, wasiwasi wangu ni *allocation* ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atueleze mkakati wake wa kuongeza kilimo na mifugo kwa nchi hii kuelekea ku-*connect* na wazo la Tanzania ya viwanda ukoje? Ukiangalia ni *theory* tu, utekelezaji wa *theory* hii mimi siuoni, naona tu ni maneno yanasemwa na mwakani wanatumia kitabu kile kile wanabadilisha mwaka wanabadilisha vitu vidogo wanarudisha kitu kile kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, anaakisi vipi, anashirikiana vipi na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutengeneza barabara ili atusaidie kule Ushetu, Kinamapula, Nyandele sijui Wandele sijui wapi, anatusaidia vipi kuleta barabara tuweze kulima kilimo cha tumbaku? Pamba imeshakufa, zao la biashara tulilonalo Shinyanga sasa hivi ambalo tunalitegemea ni tumbaku, lakini hakuna miundombinu iliyoboreshwa kila siku ni hadithi mtatekeleza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwanza naomba nitoe tu angalizo kwa wasomi wa nchi hii, kwa maana ya kwamba tunasisitizwa sana tusome sayansi, lakini jiografia nayo tuisome. Ukisoma sayansi usiposoma jiografia haina maana. Nasema hivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioghafia ya nchi yetu inatofautiana kutoka mkoa hadi mkoa, kanda hadi kanda, lakini wataalam wetu wanapotuhudumia wanashindwa kujua hizo jioghafia. Nitoe mfano, wanapogawa pembejeo

ile kalenda ya ugawaji wa pembejeo inakuwa ya nchi nzima na inakuwa ya tarehe zinazofanana wakati jiografia ya nchi yetu haifanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri sisi kanda ya Kusini tunapanda mahindi mwezi wa 12, lakini tumeletewa mbegu mwezi wa tatu. Juzi nimepigiwa simu tumeletewa mahindi ya msaada wa chakula, sisi sasa hivi tunavuna mahindi mwezi Januari sembe Wilaya ya Liwale ilifika kilo moja Sh.2,500/=, kilo hamsini ilikuwa ni Sh.100,000/=, mwone hiyo shida ya chakula. Leo tunavuna mahindi tunaletewa mahindi ya msaada hiyo yote ni kwa sababu hatuijui jiogafia ya nchi yetu. Hili jambo ni muhimu sana na ninyi mnaogawa pembejeo lazima mjue kwamba mkoa fulani unahitaji pembejeo aina fulani tarehe ipi na kwa msimu upi, hilo nilikuwa natoa angalizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile naomba nijielekeze kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Bodi ya Mazao Mchanganyiko ni tatizo, na bodi hii lengo lake lilikuwa ni kuimarisha hayo mazao lakini imekuwa kinyume chake. Nitoe mfano zao la ufuta; sisi Kusini sasa hivi zao la ufuta linakwenda sambamba na zao la korosho, lakini sasa hivi baada ya kuona zao la korosho limefanya vizuri kwenye stakabadhi ghalani tukafikiria ufuta sasa tuuingize kwenye stakabadhi ghalani. Sasa tunauingizaje wakati bodi yenyewe inayoshughulikia mazao mchanganyiko bado haijawa sawasawa? Hakuna sera yoyote ambayo inaelekeza namna ya kutafuta masoko ya hii zao la ufuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Lindi zao la ufuta ukiondoa korosho linashika nafasi ya pili kiuchumi, lakini tatizo letu kubwa la zao la ufuta ni soko. Hapo naomba nitoe angalizo lingine, kwamba hawa jamaa zetu wa vyama vya ushirika, nimeona kwenye *page* fulani hapa wamesema kwamba kazi mojawapo ni kufanya utafiti wa masoko. Vyama vya Ushirika hawawezi kufanya kazi ya utafiti wa masoko. Vyama vya Ushirika shida yao kwamba kwanza hawataki ushindani wanataka mtu mmoja *a-monoply* soko ili na wao wapate. Unapotokea ushindani wa kibiashara

kama vile ilivyotokea kwenye korosho mwaka huu wao kwa upande wao ni hasara kwa sababu hawakupata mnunuzi wa pamoja ambaye anaweza akawapa chochote. Kwa hiyo, tukiwaachia Vyama vya Msingi wafanye utafiti wa masoko hapa tutakuwa tunajidanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimesoma ukurasa wa 31 kwenye vipaumbele vya Wizara ya Kilimo. Wametaja vipaumbele kama tisa hivi pale na kimojawapo wamesema kwamba kuwawezesha vijana kushiriki kwenye kilimo, wanashiriki vipi? Nimejaribu kupitia sasa mikakati yenyewe iliyopo baada ya kuorodhesha vile vipaumbele, nikaangalia sasa mikati iliyopo kuiendea vipaumbele, maskini, sijaona chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba kuweka vipaumbele bila kuwekea mikakati kwamba tunataka tuingize vijana kwenye kilimo, kilimo cha aina gani? Hiki kilimo cha jembe la mkono ambalo Mheshimiwa Waziri wa kwanza wa Wizara hii alisema anataka kuliweka hili jembe la mkono makumbusho, lakini nalo hatuoni mikakati yake? Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hebu ajaribu kutuainishia hivi vipaumbele tisa alivyovirodhesha hapa mikakati yako ni ipi kuviendea hivi vipaumbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye kuongeza thamani ya mazao. Hapa kwenye uongezaji thamani ya mazao nimeona kwenye ukurasa wa 37 amesema sijui bodi inakusudia kuleta mashine 14. Hata hivyo, Mikoa ya Lindi na Mtwara sifuri, sasa sielewi sisi kule Mikoa ya Lindi na Mtwara hatutakiwi kuongeza thamani ya mazao yetu au ndio kwa sababu sisi tuko Kusini kama inavyosemwa siku zote? Mimi sijaelewa, kwa sababu hata mashine za kuongeza thamani zilizotajwa hapa kwetu majanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kwenye hii sekta ya kuongeza thamani wamesema tutashirikisha watu binafsi, lakini kwenye kushirikisha watu binafsi kuna matatizo huko; hatupati wawekezaji kwenye watu binafsi kwa sababu tumeongeza kodi zimekuwa nyingi mno. Ukianzisha hiyo

kampuni *OSHA* atakuja hapo *BRELA*, sijui nani sijui *TBS* sijui *TFDA,* wote wanafanya kazi moja hiyo hiyo. Sasa huyu mwekezaji atakayekuja kuwekeza hiyo faida anaipata wapi? Ndiyo maana hata hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wanachangia kwa kusema kwamba, bidhaa zetu zinashindwa kuuzika, zinashindwa kuingia kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa zetu zinashindwa kuingia kwenye soko kwa sababu bidhaa zake ziko juu, gharama ya uzalishaji iko juu. Ndiyo maana utakuta dawa ya mswaki leo ikitoka Nairobi inauzwa bei rahisi kuliko inayozalishwa hapa kwa sababu hapa kodi zimekuwa nyingi mno. Hebu jaribu kama Serikali kuna ile wanaita *collective responsibility,* nafikiri Wizara zote wakae pamoja waangalie tatizo letu liko wapi? Kwa nini bidhaa zetu zinashindwa kuingia kwenye soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba niongelee suala la maghala. Ukiingia ukurasa 36 pametajwa maghala pale panatakiwa kujengwa maghala. Hata hivyo, ukiangalia kwenye Mkoa wa Lindi na Mtwara hakuna ghala hata moja. Yaani Mikoa ya Lindi na Mtwara ni kama vile haipo nchi hii, maana kila sekta wanayoitaja nikipekua hivyo vitabu sioni wapi wameandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la zao la ufuta. Ununuzi wa zao la ufuta naomba, mwaka huu ilikuwa tuuingize kwenye stakabadhi ghalani lakini tumekwama kwa sababu ya bodi kama nilivyosema. Kwa hiyo, naomba ikiwezekana zao la ufuta mtengenezee bodi yake kwa sababu ni zao ambalo sasa hivi limeshapata umaarufu mkubwa linaiingizia pesa nyingi nchi hii. Kwa hiyo kama ambavyo kuna Bodi ya Korosho basi hilo zao la ufuta waliondoe kwenye mazao mchanganyiko na walitengenezee bodi yake ili na sisi tunaweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee zao la ngano. Tanzania tunasindika ngano inayofika tani kama 1,500,000 hivi kwa mwaka, lakini katika hizi tani 1,500,000 Tanzania tuna kama 0.05 *percent,* ndiyo ngano ya

kwetu. Sielewi sera ya nchi yetu hii ni nini? Kwa sababu sasa hivi ukiondoa mchele na mahindi, ngano inaongoza kwa ulaji lakini sioni mkakati wa Wizara wa kuimarisha hili zao ukiondoa tu kwamba linazidi tu kutupotezea pesa zetu za nje. Kwa hiyo, naomba tuone mkakati wa kufufua mashamba ya *NAFCO* ili na sisi tuweze kunufaika na sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna ukurasa 37 kupitia mradi wa *policy* and *human resource development.* Nimeona hapa wamesema kwamba watajenga maghala lakini kama nilivyotangulia kusema, kwamba na sisi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na sisi tunazalisha mazao na tunaomba maghala hayo nasi kule tuwe nayo. Mwaka wa jana tumepata shida sana ya maghala ya korosho, matokeo yake tukapata shida na usafirishaji nao ambapo barabara zetu kama mnavyofahamu ni mbovu. Kwa hiyo, nawaomba sana wanapopanga mikakati yenu, wanaopanga vipaumbele vyenu wajue kwamba Mkoa wa Lindi na Mtwara nako kuna watu nako kuna uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano wa zao la viazi. Viazi Mkoa wa Lindi tunapeleka mpaka nchi za nje lakini viazi Mkoa wa Lindi mimi kule kwetu Liwale kiroba kimoja cha viazi ni Sh.10,000/= lakini ukifika Dar es Salaam kiroba kile kile unakuta kinauzwa zaidi ya Sh.100,000/=; hivi hamwoni hii hasara wanayoipata wakulima wa Mkoa wa Lindi na Mtwara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kabisa, hii yote ni kutokana na shida ya usafiri tuliyonayo katika Mkoa wa Lindi na Mtwara hasa Wilaya ya Liwale, ndiyo maana nikasema kwa umoja wenu kama Serikali kwa *collective responsibility* wakae kwa pamoja waangalie ni wapi kunapatikana mazao gani na yatafikaje kwenye soko, hatimaye waone kwamba watu wale wananufaika na nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nilikuwa sina mengi, naomba tuu nishie hapo ujumbe umefika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge wacha ninyooshe miguu kidogo. Matangazo wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni, karibuni sana mliopo hapa. *(Makofi)*

Tunakumbushwa kwamba kesho Jumapili tarehe 21 Mei, kutakuwa na semina ya Waheshimiwa Wabunge wote kuhusu faida za utalii na umuhimu wa kuhifadhi mapori nchini. Semina hiyo itaratibiwa na Wizara ya Maliasili na utalii na itafanyika katika ukumbi huu wa Bunge kuanzia saa 4.30 asubuhi na taratibu zote za kibunge zitazingatiwa.

Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo Jumamosi tarehe 20 Mei, kwenye uwanja wa Jamhuri kutakuwa na michezo ya kirafiki ya mpira wa miguu (*football)* na mpira wa pete (*netball)* kati ya Bunge *Sports Club* na timu za *NSSF* saa kumi jioni, Waheshimiwa na wananchi wote wa Dodoma mnakaribishwa.

Hayo ndio matangazo tuliyonayo. Sasa tuendelee na kazi yetu niwatambue wafuatao: Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Mheshimiwa Alex Gashaza na Mheshimiwa Azza Hamad, ajiandae. Mheshimiwa Sigalla.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kabla sijaendelea nichukue nafasi hii angalau kwa dakika moja kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayofanya ya kuiendeleza Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie mambo machache kwa haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Waziri afahamu kwamba ili uendeleze kilimo na ufugaji ni vizuri Hazina (*treasurers)* za Serikali na hasa mashamba maalumu yaliyotengwa kwa ajil ya ufugaji ya Serikali yatumike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu mstaafu baba wa Taifa hili Mwalimu Nyerere pamoja na mzee Karume mwaka 1965 walikaa kutafakari na kuona ni jinsi gani wataondoa ugomvi kati ya wakulima na wafugaji, ndipo wakaja na wazo la kusema ni lazima mashamba ya mifugo yaanzishwe ili wanaochunga ngo'mbe wajifunze kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana hawa wazee, wameshalala wametangulia mbele za haki, lakini bado hekima zao na akili zao zinaonekana ziko juu sana ya upeo wetu leo. Kwa mfano Shamba la Kitulo ambalo liko Makete uwezo wake ni kuchukua ng'ombe 4,500 sasa hivi wako ng'ombe 750 tutawezaje, tutawezeshaje wananchi wa Tanzania kufuga ng'ombe na kupata maziwa? (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Mifugo aliyepita Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alitembelea Wilaya ya Makete akabaini hazina kubwa iliyopo pale, akaridhika kwamba ni muhimu sana zitafutwe bilioni 7.6 ili shamba lile liweze kufufuliwa ili Watanzania kutoka kaskazini na pande zote za Tanzania waweze kujifunza namna ya kufuga, tuondoe ugomvi wa kuswaga ng'ombe. Mpaka leo hivi ninavyoongea Waziri hajaenda tena kuweza kujibu hoja hii ya wananchi wa Makete kwamba ni lini hao ng'ombe watakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji aliposimama hapa kwenye mada yake alisisitiza kwamba ng'ombe 3,000 wameagizwa kutoka nje, mpaka leo hao ng'ombe hawajaenda Kitulo. Kwa hiyo hazina ile inapotea wakati ingeweza kujibu haja ya migogoro ya wakulima lakini pia ingeweza kuboresha uchumi wa Watanzania wala si Makate peke yake, ni Watanzania wote; maana wangejifunza kule namna ya

kufuga wangepata maziwa, wangepata ajira, afya zingeboreshwa na uchumi ungeboreshwa pia. Ni muhimu sana Wizara izingatie hili ili kuendeleza uchumi wetu lakini pia kuboresha mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko shida ya kufasili namna bora ya kuboresha kilimo chetu. Soko limeachwa kwa wakulima ambao weledi wao uko kwenye kulima na hauko kwenye masoko. Niiombe sana Wizara, Mheshimiwa Waziri Wizara yake ni muhimu kabisa ijikite kwenye kutafuta, la kwanza masoko, ili mkulima anapolima awe na uhakika wa bei atakayouza, siyo ilimradi kuuza lakini bei atakayouza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, ni vizuri Mheshimiwa Waziri ajikite kwenye kutafuta mbegu bora. Pale Makete na Njombe nzima tunalima sana viazi, lakini leo viazi tunavyolima havina soko kwa sababu viazi vinavyozalishwa nchi jirani ya Kenya vinauzwa kwa bei ndogo Sh.50,000/=, wakati sisi uzalishaji bei ya chini ya uzalishaji ni Sh.80,000/=. Kwa sababu hiyo kwa vyote vile tukitaka kuuza hivyo lazima tuuze kwa bei ya hasara. Tatizo haliko Kenya, tatizo liko kwetu, kwamba Wizara inafanya nini kutoa majibu ya mbegu bora ili wakulima wetu wa viazi, watumie mbegu bora hatimaye wapate viazi vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifurahi sana rafiki yangu Mhandisi Tizeba alipoteuliwa kushika Wizara hii. Nilifurahi kwa sababu kwanza yeye ni mkulima, hata kama yeye ana fani ya uhandisi lakini ni mkulima, naamini ataitendea haki Wizara hii; kwa sababu hatusemi vitu ambavyo ni vya nadharia kwake yeye anavi-*practice,* analima, anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana rafiki yangu Mheshimiwa Tizeba apeleke nguvu kwenye kutafuta mbegu bora za viazi, pareto na mazao mengineyo, tukifanya hivi tutaharakisha maendeleo ya nchi yetu na hasa kwenye eneo la ukulima bora; vinginevyo wakulima wetu wataendelea kulaumu sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, watadhani kwamba tunazembea. Sasa mtu mmoja akizembea ni vizuri sana ajue kwamba ni yeye aliyezembea. Nami naamini

Mheshimiwa Waziri si mzembe, kwa vyovyote vile atafanya jitihada ili kuhakikisha kwamba analigeuza hili jambo ili kwamba mbegu bora zipatikane na wakulima wapate kulima vizuri na twende mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pareto ni moja ya mazao ambayo miaka ya 80 Wilaya ya Makete ilikuwa inaongoza kwa zao la pareto. Likapoteza mwelekeo kwa hiyo bei yake ikashuka. Sasa hivi angalau bei ya pareto inarudi, niombe sana Wizara, kama nilivyosema awali isipuuze soko kuachia wakulima, hawa ni wakulima wa kawaida weledi wao ni wa kawaida, hawana weledi wa kutafuta masoko. Niombe sana Mheshimiwa Waziri aichungulie Makete ili aweze kuona ni jinsi gani ataharakisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe mchango wangu mfupi kwa kusema kwamba kama Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hatasema neno kuhusu jinsi ya kulifufua shamba la Kitulo ili wananchi wale waone faida ya kuachia hekta 12,000, kama asipokuja na majibu hakika nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anafahamu rafiki yangu, sina jinsi ya kushawishika isipokuwa atoe majibu jinsi ya kuwafanya wananchi wa Makete ambao wamenituma kwenye Bunge hili waone faida ya kutunza eneo hilo na waone faida ya ng'ombe hao kuwa wamesambaa kwenye kata zote 23 za Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mungu Ibariki sana Serikali ya CCM, siungi mkono hoja mpaka atakapotoa majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. tunaendelea Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Alex Gashaza na Mheshimiwa Azza Hamadi ajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kunipa nafasi ili niweze kuchangia mada hii ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwanza kuipongeza Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sekta hii ambaYo ni sekta muhimu inapiga hatua na kuweza ku-*support* sekta zingine ambazo zinategemea kilimo kama Sekta ya Viwanda, Mazingira na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia vitabu hivi viwili, kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, na kitabu cha Kamati ya Kudumu ya Bunge, ya Kilimo, Mifugo na Maji, nimefarijika kutokana na malengo ambayo yapo katika bajeti hii. Pia nimefarijika zaidi baada ya kuona kwamba utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais, zinaendelea kudhihirika kwa vitendo hususani pale ambapo wameendelea kuondoa zile kodi za kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka Mkoa wa Kagera Wilaya ya Ngara, sisi ni wakulima wa zao la kahawa, kwa muda mrefu sana zao la kahawa limekuwa na bei chini kutokana na tozo nyingi. Zilikuwepo kodi 26 sasa zimeondolewa kodi 17; naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais na Wizara ya Kilimo kwa kazi hii nzuri. Vile vile nipongeze hata kwa kodi ambazo zimepunguzwa kwenye Sekta ya Mifugo, kodi saba zilizoondolewa zitafanya maboresho katika sekta hii ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango mizuri ambayo imeainishwa katika kitabu hiki cha bajeti katika kuboresha sekta hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, lakini kutokana na bajeti hii kuwa ndogo napata mashaka kidogo katika utekelezaji wa baadhi ya malengo ambayo yamewekwa katika mpango huu wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunapokuwepo na ufinyu wa bajeti na inapotokea kwamba sasa hata pesa hazipelekwi kwenye miradi ya maendeleo inavyotakiwa, athari ni kubwa na zinaonekana katika maeneo mengi. Kwa mfano tumeshuhudia kwamba upo upungufu kwa mfano wa watumishi hususan Wagani katika maeneo mbalimbali, tumeshuhudia upungufu wa bajeti katika vituo vya utafiti,

tumeshuhudia kuwepo na upungufu wa fedha hususan katika kuboresha miundombinu katika sekta ya mifugo kwa mfano ujenzi wa malambo, ujenzi wa majosho na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe kwamba katika utekelezaji sasa wa bajeti hii, pamoja na kwamba kuna ufinyu huu, kuna upungufu huu, nina uhakika kama tutaweza kusimamia vizuri na tukaenda kulingana na jinsi ambavyo tumeweka vipaumbele, tunaweza tukapiga hatua, sina mashaka kwa sababu dalili naziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ambazo nimezisema, kwa mfano kwenye vituo vya utafiti kuna mahali ambapo mpaka sasa hivi kwenye vituo vya utafiti kama kituo cha Naliendele, baadhi ya watumishi ambao wamestaafu hawajaweza kupata stahiki zao hususani kama pesa kwa ajili ya kusafirisha mizigo yao, lakini bado pia, watumishi wanapostaafu *replacement* ya watumishi wengine inakuwa ni tatizo kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo niwaombe katika maeneo haya ambayo ni muhimu Serikali iweze kuyaangalia na kujikita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua jitihada za Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri, na watendaji wao. Binafsi upande wangu katika Jimbo langu la Ngara, wamekuwa wakinipa ushirikiano mkubwa na ndiyo maana nasema kwamba, ili tuweze kuinua sekta hii ya kilimo pamoja na kuzalisha mazao ya chakula lakini ni lazima pia tuangalie uzalishaji wa mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu kubwa tunaangalia mazao ya chakula kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na chakula cha kutosha, lakini tunapokuja katika suala la kuinua kipato cha mwananchi na kuinua uchumi wa nchi hii kupitia sekta ya kilimo, lazima tuangalie uboreshaji katika mazao ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mazao ambayo tumeyazoea korosho, kahawa, pareto, pamba na kadhalika; lakini yapo mazao mengine ambayo hatujayazoea Tanzania

lakini ni mazao ambayo yamefanya vizuri katika nchi zingine na ambayo yameweza kuinua uchumi mkubwa katika Mataifa hayo. Ndiyo maana katika jitihada zangu binafsi kama Mbunge wa Jimbo la Ngara za kuangalia fursa zilizopo, na kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, tumeamua kuanzisha zao jipya la *Stevia*, ambalo ni zao linalofanya vizuri duniani sasa. Naishukuru Wizara kwa ushirikiano wanaonipa kwamba tayari sasa tunaingia kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii kama nilivyoomba wakati ule kwenye swali langu la nyongeza, kwamba kituo cha Maruku ambacho kitafanya utafiti kwa kushirikiana na Kampuni ya *East Africa* Stevia *and agro investment* kwenye zao hili la *Stevia* basi bajeti iweze kutengwa kwa ajili ya kituo hiki cha Maluku na utafiti huu uweze kufanyika katka Jimbo la Ngara. Ni pesa kidogo tu ambazo haziwezi kuzidi milioni 20 kwa kuanzia kwa ajili ya utafiti huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo. Sekta hii ni sekta muhimu, lakini ni sekta ambayo imekumbana na changamoto nyingi. Katika Wilaya yangu ya Ngara tuna mifugo mingi, tuna ng'ombe takribani 70,000, mbuzi wasiopungua 190,640, nguruwe takribani 20,000 na kondoo zaidi ya 75,000 lakini hatuna lambo hata moja, yaani bwawa la kunyweshea mifugo. Kwa hiyo hii inakuwa ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ambayo ilikuwa inachungiwa kwenye hifadhi za Burigi na Kimisi sasa mifugo hiyo inaingia vijijini ambako hakuna huduma hizi za mabwawa na malambo, kwa maana hiyo vyanzo vya maji ambavyo ndivyo vinavyotumiwa na wananchi kwa ajili ya matumizi ya kawaida vinazidi kuharibiwa kutokana na mifugo hii, ambayo ni mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ya bajeti yake aweze kuangalia ni namna gani ambavyo

wanaweza wakatenga kiasi fedha kwa ajili angalau ya kuweza kuchimba hata malambo manne basi kwa sababu tuna tarafa nne basi kwa kuanza angalau Malambo manne ili kila tarafa iweze kupata lambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Ngara naweza nikasema ni lango la kuingilia na kutoka kwenye Nchi za Maziwa Makuu, lakini pia ni Jimbo ambalo lina fursa nyingi. Kama nilivyotangulia kusema na ambavyo nimesema wakati nachangia kwenye Wizara ya Maji, niipongeze Wizara kwamba baada ya mchango wangu wameangalia kwa makini na tayari bonde la Murongo limetengewa fedha kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu, ambalo liko katika Kata ya Bukililo. Pia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Maji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante. Mheshimiwa Azza Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Jumaa Aweso na Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na hatimaye kusimama katika ukumbi wako wa Bunge kuweza kuchangia Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakumbuka mwaka 2015 wakati wa uchaguzi alisema kodi kero zimezidi na hatimaye leo ndani ya mwaka mmoja na

nusu tunakwenda kuona kodi kero zimenakwenda kuondolewa. Mheshimiwa Rais hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Naibu wake pamoja na timu yake yote. Niwaombe basi haya waliyoyaandika kwenye vitabu hivi waende wakayafanyie kazi. Tunawaamini, tunaamini watatekeleza yale ambayo wametuletea leo ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo bila afya hakiwezi kwenda na natambua kabisa mchango mkubwa wa wanawake katika sekta ya kilimo. Naomba uniruhusu nitumie fursa hii kuwashukuru sana Ubalozi wa China nchini Tanzania kwa kuweza kunisaidia kwa wanawake wa Mkoa wa Shinyanga, msaada wa vifaa vya kujifungulia akinamama, nawashukuru sana Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nijielekeze sasa katika bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Maeneo yetu yanatofautiana kwa kiasi kikubwa. Ninaposema yanatofautiana nina maana gani? Mkoa wa Shinyanga kwa miaka mfululizo sasa tumekuwa hatupati mvua za kutosha na Mkoa wa Shinyanga huwezi kuwaambia wananchi waende wakalime. Yuko tayari kulima kimeungua analima, kinaungua analima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kusema kwa mwaka huu tukaouanza ambao msimu wake wa mvua umekwisha tuna upungufu mkubwa wa chakula. Mkoa wa Shinyanga ni Wilaya moja angalau inakuwa inafanya vizuri kwenye suala la chakula, lakini nayo kwa mwaka huu kidogo hapako vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Kwandikwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Jimbo lake ndio kidogo ndio kidogo linakuwa linaupatia Mkoa wa Shinyanga chakula, lakini kwa mwaka huu, Jimbo la Ushetu hawakuweza kufanya vizuri kwa sababu ya ukosefu wa

pembejeo. Kwa hiyo, nikiuchukua Mkoa mzima wa Shinyanga hali ya chakula tuna upungufu kwa kipindi hiki tunachokwenda naomba Mheshimiwa Waziri atuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa haifanani na maeneo hayafanani, Mheshimiwa Waziri ananitazama naomba hili alichukue alifanyie kazi. Hatupendi Waheshimiwa Wabunge wa Shinyanga kusimama humu tukasema haya, Wasukuma si watu wa kuwaambia kwenda shambani watu wote humu ndani ni mashahidi, Msukuma ni mtu ambaye anainuka mwenyewe anakwenda shambani, hakuna mtu wa kumwambia aende shambani, lakini hali ya hewa ilivyo, ndiyo inatulazimu kufikia hatua ya kusema tuna upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda sasa hivi mfuko wa sembe, wa kilo 50 unauzwa Sh70,000/=. Ninaposema tuna upungufu wa chakula naomba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi waangalie. Ghala la chakula tunalo pale karibu, hatuhitaji chakula cha bure, tunahitaji wananchi wetu wapate chakula chenye bei nafuu. Niwaombe wafanyabiashara, niwaombe mikoa ambayo wanajinasibu wana chakula cha kutosha, watuletee chakula Mkoa wa Shinyanga watuuzie kwa bei ambayo ni nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba Serikali ya Mkoa wa Shinyanga mwaka 2010/2011 ilikaa na kubaini maeneo ya kuweza kuwa na kilimo cha uhakika katika Mkoa wa Shinyanga ili kuuondoa Mkoa wetu katika kilimo cha kutegemea mvua za juu. Ilibaini eneo la bonde la Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na wataalam kutoka Wizara ya Kilimo walitembelea eneo hili, sijui hayo yaliishia wapi? Tangu mwaka 2010/2011 mpaka leo kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bonde zuri kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, matokeo yake ni nini. Hata mwaka huu ninavyoongea mvua zimenyesha za mwisho mwisho,

bonde lile limejaa maji, lakini hayana kazi tena, yanapotea kwa sababu hatuna sehemu ya kuyahifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara ituangalie Mkoa wa Shinyanga kwa sababu hata aliyekuwa Waziri Mkuu kipindi kilichopita, Mheshimiwa Mizengo Pinda, alikuja Shinyanga na akaiona hali ya Shinyanga akaahidi kulisimamia bonde hili na kuhakikisha Shinyanga tunakuwa na kilimo cha umwagiliaji. Tukikimbilia kusema kule kwenye milima na maporomoko ya maji ndio wapewa kilimo cha umwagiliaji, wanakuwa hawatutendei haki wale ambao hatuna maporomoko ya maji na milima inayoporomosha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itutazame Mkoa wa Shinyanga kwa jicho la huruma, watutazame waweze kutuwekea miundombinu na kamwe hawatatuona tunasimama na kusema tuna upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo cha umwagiliaji nasikitika sana, najua kilimo na umwagiliaji ni vitu ambavyo vinaendana kwa pamoja, nina hakika Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji yuko hapa; suala hili lilitekelezwa kwenye umwagiliaji kipindi kilichopita. Mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Isholololo, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Mradi huu umetumia fedha nyingi, mamilioni ya fedha, lakini ukifika kwenye mradi ule unaweza ukalia. Tumeachiwa mashimo tu. Tuta lile baada ya mwaka mmoja limebomoka na maji yanapita, hakuna kinachohifadhika kwenye bwawa lile la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, Mheshimiwa Waziri akisimama hapa aniambie. Nataka kujua waliokwenda kutekeleza mradi ule wa Kijiji cha Isholololo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga wamechukuliwa hatua gani kwa sababu mradi ule ulikuwa umelenga kuwafaidisha na kuwanufaisha wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, lakini mradi ule tena hauna tija kwetu kwa sababu tumeachiwa mashimo na tuta lile limekatika na maji yanapita yanapitiliza hayana sehemu ya kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba majibu ya Serikali, Mradi ule wana mpango gani nao ili tuweze kuwa na tija nao, bila ya hilo Mheshimiwa Waziri kwa kweli sitamwelewa. Naomba awasiliane na watu wa Maji na Umwagiliaji wamweleze mradi huu wa Isholo lo hatima yake ni nini? Yale mashimo yaliyoko pale hatuhitaji kuyaona, tunahitaji kuona mradi unafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la mbegu. Tunapokwenda kwenye maeneo ya ukame kama Mkoa wa Shinyanga, tunawaambia wananchi wetu wabadilike wapande mbegu ambazo zinastawi kwa muda mfupi. Hata hivyo, kinachonisikitisha sana mbegu hizi zinauzwa bei kubwa sana. Unapomwambia mwananchi akanunue Stuka sijui akanunue Pama sijui akanunue kitu gani, kile kimfuko cha kilo moja kinauzwa mpaka 12,000, mwananchi wa kawaida hawezi kumudu kununua mbegu hizi na kwenda kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewashawishi wananchi kwa kipindi hiki tutoke kwenye zao la mahindi twende tukalime mtama. Mbegu yenyewe ya mtama kwa mwaka huu ilikuwa ni adimu mno, haipatikani. Niiombe Wizara itufanyie mpango mkakati wa kuweza kutuletea mbegu hizi ili na sisi tuweze kuwa tunavuna kwa muda unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye soko la mazao. Miaka ya 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iliweka mpango mkakati wa kuwa na soko la mazao, soko la mchele. Tunaposema mchele wa Shinyanga maana yake kweli Shinyanga kuna mchele, mchele wa Dodoma, mchele wa Arusha, unatoka Shinyanga. Tulipenda Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tuwe na soko la mchele pale katika Kata ya Didia na mipango hii ilitoka Halmashauri ikaenda mkoani ikaja Wizarani, sijui ilifia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba mchele sasa unakuwa na soko lake katika Mkoa wa

Shinyanga na kuweza kununuliwa? Kuna watu wengi wanaokuja kununua mchele lakini hatuna soko la uhakika, tunahitaji na sisi kuwa na soko ili mchele wetu uweze kununuliwa sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye mifugo. Mkoa wa Shinyanga ni miongoni mwa mikoa ambayo ina mifugo ya kutosha. Kwa nini wafugaji wetu wanaondoka? Ni kwa sababu ya hali kama hii ninayoisema ya ukame, marlsho hayapo, maji hayapo, ni kwa nini Wizara haifikirii kwenda kwenye maeneo kama Mkoa wa Shinyanga ambapo wafugaji wanahangaika kuhama na mifugo, wakawapa utaalam wa kupanda zile nyasi ambazo zinapandwa Mwabuki, zinapandwa pale Mpwapwa na maeneo mengine ili wafugaji wetu wasiendelee kuhama na mifugo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika mfugaji ukimwelisha na ukamwonesha hizo nyasi zinapandwa vipi, na zinapatikana wapi, hakuna mfugaji atakayehama kwenye eneo lake na kwenda kutafuta malisho sehemu nyingine. Naomba Wizara watuambie mna...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba, naomba pia Wizara iongee na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili ule mradi wa umwagiliaji... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wetu ndio huo.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jumaa Aweso.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba muhimu katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wangu, Mhshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wa Tanzania. Imani huzaa imani, kwa namna anavyofanya kazi tutaendelea kumuunga mkono; na hata kama uchaguzi ungekuwa mwaka 2020, mimi kura yangu ningempigia tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aendelee kuwa Rais wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda niwapongeze Mawaziri pamoja na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa namna wanavyofanya kazi. Nawaona ni namna gani wanavyoweza kushiriki na wakulima, wafugaji na wavuvi katika matatizo yao. Kikubwa nawaombea Mwenyezi Mungu awabariki waendelee kufanya kazi, lakini kubwa lililonifurahisha ni namna gani walivyoweza kuondoa tozo ambazo zilizua kero, ambazo zilikuwa zinadumaza maendeleo ya wavuvi, wakulima na wafugaji. Hongereni sana, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa, nilikuwa nataka nizungumzie kuhusu suala zima la zao la nazi. Pamoja na kwamba kilimo ni uti wa mgongo, lakini kila kilimo kinategemeana na mazingira yake. Ukienda Shinyanga wanategemea suala la pamba, Tabora wanategemea tumbaku na sisi wananchi wa Pangani tunategemea zao la nazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia nazi, ninazungumzia uchumi na maisha ya wananchi wangu wa Jimbo la Pangani. Wananchi wa Pangani wamekuwa maskini kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Minazi ile imekufa, imekauka, hali ya maisha imekuwa duni sana. Naiomba Wizara hii ifanye tafiti ya dhati kabisa ili kulifufua zao hili la mnazi. Kwa sababu tunapozungumzia suala la zao

la mnazi, ni moja ya kitega uchumi. Sisi binafsi tulikuwa tukichangia pato kubwa la Taifa kipindi cha nyuma; tulikuwa tukizalisha nazi kiasi cha 500,000 kwa mwezi lakini sasa hivi imeshuka tunazalisha chini ya 100,000. Kwa hiyo, tafiti zifanyike kwa haraka ili tuweze kujua ni namna gani tunaenda kulifufua zao hili la mnazi ili na sisi Wilaya yetu ya Pangani tuweze kuchangia pato la Taifa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia juzi nilihudhuria kongamano la kuhusu suala zima la zao la korosho. Kwanza nampongeza Mkurugenzi wa Bodi hii ya Korosho kwa mkutano mzuri unaonipa matumaini. Na sisi katika Wilaya yetu ya Pangani tuna mazingira mazuri kabisa ya kufufua zao hili la korosho. Naiomba Wizara hii ituhakikishie kwamba inatupatia mbegu kwa haraka na bora ili kuhakikisha kwamba tunaenda sambamba, badala ya mnazi tunaenda sasa na zao hili la korosho kwa sababu tunaona kabisa Korosho ni zao la kijani. Kwa hiyo, tunapopanda korosho na tafiti zinafanyika kwa ajili ya kuinua zao la mnazi, nina imani uchumi wa Pangani utakuwa kwa kasi na maendeleo yatakuwa kwa kasi nasi tutaweza kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nizungumzie, tunaona kabisa nchi yetu inaelekea katika suala zima la viwanda. Kama tunahitaji suala zima la viwanda, lazima tuwekeze kwa dhati kabisa katika suala zima la kilimo. Ukiangalia kilimo tunacholima sasa, tunategemea kudra za Mwenyezi Mungu. Leo mvua ikinyesha kwa wingi, kilimo kinakuwa na athari kubwa, mvua isiponyesha, pia kuna athari kubwa. Ili tuweze kuingia katika uchumi wa viwanda na tupate maendeleo makubwa ya viwanda ni lazima tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa kuwa na mito mingi mbalimbali. Sisi katika Jimbo letu la Pangani tumekuwa na Mto Pangani, lakini tunashindwa kunufaika nao, leo mto unamwaga maji baharini kwa kukosa miundombinu mizuri ya maji. Namuomba Mheshimiwa Waziri akae na Waziri wa Maji ili watuhakikishie kwamba

wanatutengenezea miundombinu ya maji ili sisi wananchi wa Pangani tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji. Tukiwekeza katika kilimo cha umwagiliaji, leo tunaweza tukaulisha Mkoa wa Tanga, lakini tunaweza tukailisha Zanzibar na kanda ya Kaskazini kupitia mto huu wa Pangani.

Kwa hiyo, naomba tusiishie Pangani, lakini hii iwe ajenda ya nchi ili kuhakikisha kwamba tunawekeza katika kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kupata manufaa makubwa na malighafi ambayo itatumika katika suala zima la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie hapa ni kuhusu suala zima la wavuvi. Wilaya yetu ya Pangani ina bahari ya Hindi, lakini wavuvi wale wanashindwa kunufaika kwa sababu ya kukosa uwezeshwaji wa nyenzo. Leo mvuvi wa Pangani anatumia ndoano na chambo. Hivi leo ikitokea samaki ameshamla samaki mwenzake kashiba, hivi kweli anaweza akamvua huyo samaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara sasa tuangalie namna gani tunaweza tukawawezesha wavuvi hawa wadogo ili kuhakikisha kwamba wanapata nyenzo za kisasa ambazo zitaweza kuwasaidia ili waweze kunufaika na rasilimali bahari iliyokuwepo katika Jimbo langu la Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri ambalo nataka nilizungumze ni kwamba, pamoja na kuwekeza katika bahari lakini pia tuna wafugaji katika Wilaya yetu ya Pangani. Ni sekta muhimu na ambayo inachangia mapato ya Halmashauri lakini ukiangalia wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi sana; hawana majosho wala hawana malambo.

Naiomba Wizara hii na Mheshimiwa Waziri aangalie namna anavyoweza kutusaidia. Wanasema unapozuru wengine, naomba na sisi utukumbuke, usitupite kwa kuhakikisha kwamba unatupatia majosho na malambo ili

wale wafugaji wa Pangani waweze kunufaika na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maneno mengi sana, ila kubwa naomba niwapongeze sana Mawaziri hawa kwa namna wanavyofanya kazi. Naiomba Serikali itoe fedha kwa dhati na kwa haraka ili iweze kutekelezeka bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mdee kwanza, halafu Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba tu meza ya Katibu ziwe dakika kumi, maana huwa mnapunja muda sana. Kwa hiyo, mnipigie kengele kwa dakika kumi zangu za kawaida.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, wewe ndio unatumia vibaya sasa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisema kwamba kwanza nasikitika na ninawashauri tu Wabunge wapya na vijana, jukumu letu sisi ni kuisaidia Serikali na kuisaidia nchi. Anasimama Mbunge anatoa pongezi kwa Wizara ya Kilimo kwa sababu ya hoja moja ya tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake anatumia robo tatu ya muda kusema tozo mbalimbali alizozikata badala ya kutuambia pamoja na hiyo tozo kukatwa tuna mikakati gani mipana ya kusaidia 75% ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tungewekeza kwenye kilimo ipasavyo kama ambavyo mipango ya miaka mitano mitano kwa miaka zaidi ya 30 iliyopita, kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikisema kwa miaka zaidi ya 30 iliyopita, ajenda isingekuwa tozo yaani tungeongeza

kodi Serikali ingepata mapato kwa sababu tumewekeza vizuri. Ni muhimu Wabunge wapya wakajua Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi iliahidi kuongeza...

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mdee keti tu, tusikilize taarifa, ingawa mnanijua mimi msimamo wangu wa taarifa. Keti tu Mheshimiwa Mdee.

**T A A R I F A**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji aliyekuwa anaendelea kuzungumza kwamba Wabunge wote humu ndani ni wapya, kwa sababu uchanguzi umefanyika 2015, wote tukaja hapa tukaapa. Kwa hiyo, Wabunge wote ni wapya kwa mujibu wa uchaguzi tuliofanya 2015. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ananipotezea muda. Ninachotaka kumshauri, mimi unajua natoka Jimbo la mjini, *alright!* Asilimia 85 mnatoka majimbo ya vijijini. Tukichukulia mzaha bajeti ya kilimo, mimi kwangu naathirika kwa sababu tu ya mfumuko wa bei.

Kwa hiyo, ni lazima nizungumze hapa kwa sababu mwaka 2016 mfumuko wa bei ulikuwa 5.4% sasa hivi ni 6.4% kwa mujibu wa ripoti ya *BOT* iliyotoka juzi. Kwa sababu chakula, mahindi, sukari, mihogo imepanda bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumza hapa, tunataka wenzetu wasikie. Hivi unapongezaje bajeti ambayo mlituahidi kilimo kitakua kwa 10% mwaka 2010; kikashuka, sasa hivi kilimo kinakua kwa asilimia 1.7%? Mwaka 2016 kilimo kilikuwa kinakua kwa 2.7%; mwaka 2015 kilimo kilikuwa kinakua kwa 4%! Kwa hiyo, kwa kadiri ambavyo siku zinakwenda, kilimo kinazidi kushuka chini; na tafsiri yake 75%

wa Watanzania wako hoi bin taabani! Hatuoni? Hivi tunapongeza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo inaniuma! Bajeti ya maendeleo, eti kati ya shilingi bilioni 101, zimepatikana shilingi bilioni 3.3, sawa na 3.31%. Hivi tunapongeza nini? Hivi Mheshimiwa Waziri huyu...

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima keti tu.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa kwa mujibu wa kifungu cha 68(8) kwa misingi kwamba malalamiko yake kuhusu Wabunge waliochangia kupongeza juu ya kuondolewa kwa tozo mbalimbali nadhani hazina mashiko kwa sababu yeye ni Mbunge wa Mjini kama alivyosema. Kwa wale Wabunge wanaotoka vijijini wanafahamu adha kubwa walizokuwa wanapata wananchi wa vijijini.

Kwa hiyo, wanayo haki ya kuzungumza kero zilizokuwa zinahusu wananchi wao, asiwaingilie katika hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, taarifa unaikubali?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Aah! Mheshimiwa Zitto, wewe unajua kanuni, acha akae. Kaa kwanza. Mheshimiwa Mdee, unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia mama yangu pale, ufukara mliowasababishia wakulima wa nchi hii...

**MWENYEKITI:** Aah! Mheshimiwa Mdee, tumia neno la…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Siwezi kupokea taarifa hiyo ya hovyo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, sikia basi! Nisikie kwanza, usimwite mama, muite tu Mheshimiwa…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa *Chief Whip* Kivuli! Aah, Mheshimiwa *Chief Whip. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi, labda nirudie, niweke vizuri. Kwa sababu sisi ni rahisi ku-*propagate* mambo. Nasema hivi 75% ya Watanzania ambao wanafanya kazi ya kilimo, ambao 80% ndani yake ni wanawake, wamefukarishwa na Serikali ya CCM kwa sababu ya mipango ambayo hawana mikakati ya kuitekeleza. Ndiyo maana…

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Mdee. Unaikubali taarifa au unaikataa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeikataa kwa sababu haina *issue*. Sasa ndiyo nataka ni…

**MWENYEKITI:** Sasa muda, muda! Endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema ni nini Wabunge? Nasema kwa nia njema kwamba kama leo bajeti ya maendeleo ya kilimo tumetoa 3%; mwaka 2016 tukasema utekelezaji, ndugu yetu ni mpya 15% tena kwenye shilingi bilioni 32 ikatoka shilingi bilioni tano, asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji, wakati anasoma Waziri wa Maji imepatikana 8% tu. Tume ya Umwagiliaji ina wajibu wa kuhakikisha kwamba Sera ya Umwagiliaji inatekelezwa ili miundombinu ya umwagiliaji iwekwe kule kwenye mashamba, halafu eti mtu anakaa

anapongeza, unapongeza nini? Hatuisaidii Serikali! Hatuisaidii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba tutasimama hapa kwa sababu wengi tunawakilisha wakulima, tuweke mguu chini, tuiambie Serikali… *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee zima tu hiyo *microphone*. Taarifa Mheshimiwa *Engineer* Isack.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mbunge anayeongea, Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na 8% iliyotolewa na Serikali kwenye umwagiliaji, lakini bado tumekuwa na shilingi bilioni 20 zilizotolewa na wafadhili na Mradi wa Dakawa unaendelea; lakini pia imetolewa shilingi bilioni 23 na Serikali ya Japan na imesambazwa kwenye maeneo mbalimbali katika Halmashauri na kazi ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji bado inaendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unasemaje Mheshimiwa hiyo taarifa? Unaikubali au unaikata?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kaa kwanza, utanipa ya kwako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasoma taarifa za Serikali tulizoletewa Bungeni.

**MWENYEKITI:** unaikubali au unaikataa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kukubali, yaani haina mashiko. Siwezi kukubali hiyo taarifa, kwa sababu sisi tunasoma nyaraka ya Serikali. Tunasoma Taarifa za Kamati za Bunge. Sasa kama hizo taarifa

zinatuambia hivyo, hayo makandokando mengine ya kuombaomba huko, sisi hayatuhusu. Sisi tunazungumzia bajeti ya Serikali na tuko kwenye bajeti hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wasiniingilie. Mheshimiwa mh! Jana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, hebu kaa. Kuna taarifa. Mheshimiwa Zitto unataka kumpatia Mheshimiwa Mdee?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *speaker's guidance.*

## MWONGOZO

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waheshimiwa Wabunge wanapochangia na kupongeza, wanazungumza, Waheshimiwa Wabunge ambao wanaona kwamba bajeti ina upungufu, walikaa kimya na kuwasikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba utupe mwongozo wako kwamba kipindi ambacho Mbunge anayeona kwamba bajeti ina upungufu akichangia, pia upande wa pili uweze kukaa kimya. Kwa sababu takwimu ambazo Mheshimiwa Mdee anazizungumza, hazitoi hewani, anazitoa kwenye nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge hapa amezungumza kuhusiana na tozo ambazo zimetangazwa na Serikali jana. *Majority* ya tozo ambazo zimetangazwa...

**MWENYEKITI:** Tumekuelewa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasherehesha. Mwafrika hawezi kuzungumza bila kusherehesha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapana, muda! Mheshimiwa Zitto!

**MBUNGE FULANI:** Tunaomba Kanuni Mheshimiwa!

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uvumilivu ndani ya nyumba.

**MWENYEKITI:** Nimeshakulewa. Muda wangu ni finyu sana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie dakika moja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana kwa mujibu wa kanuni zetu, suala la taarifa ni sehemu yake, lakini tatizo ambalo huwa tunaliona hapa; taarifa hata ile ambayo ina lengo la kutoa hali halisi ya kile kilichosemwa, tumeanza kujenga tabia tu ya kusema siikubali taarifa. Ndiyo maana mara nyingi mnanielewa msimamo wangu wa masuala ya taarifa.

Nilitegemea mambo mengine kama ni taarifa ambayo inatokana na hotuba au hoja ya Mheshimiwa Waziri, yeye mwenye hoja ana nafasi atakapokuja ku-*wind up,* kuja kuyasahihisha hayo. *(Makofi)*

Eeeh, sasa ndiyo mara nyingi huwa nasema, tusifanye kazi ambayo siyo yetu. Unamwachia mwenye hoja na ndiyo maana wako hapa na wataalamu hawa wapo kwa shughuli hizi. Wanakuja kuyasema vizuri tu ili Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote waielewe *position* ya suala hilo. Tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika, unafahamu...

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufahamu wangu ndani ya Bunge hili,

Waheshimiwa Wabunge wote sisi tuko sawa. Hakuna Mbunge wa Mjini wala wa shamba, Wabunge wote sisi tuko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaoomba kutoka kwako ni huu kwamba kila mtu ana uhuru wa kusema lile analoliamini ndani ya Bunge. Wale wanaopongeza ndivyo wanavyoamini; wale wanaokosoa ndivyo wanavyoamini. Nilidhani kwamba ni ustaarabu wa Bunge hili anayepongeza aendelee kupongeza, anayekosoa aendelee kukosoa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hana nidhamu huyo. Ni mwalimu wa nidhamu na ni Mwenyekiti wa Nidhamu, lakini hana nidhamu!

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo mtu anasimama, anamdhalilisha mwenzake kwa kusema amesema ya hovyo, amesema ya hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wewe ulisema ni mwanajeshi!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maana sasa mnaanza kuchomoka tu! Hapa Mheshimiwa Mdee ndiye anayechangia hoja hii. Alipewa taarifa nikairuhusu kwa shingo upande, lakini nikasema hivi, hiyo ni sehemu ya kanuni zetu. Nimeona tu kwamba imekuwa ni kawaida sasa, mtindo tu kwamba taarifa yoyote hata kama imesheheni suala zuri la kushibisha, tunasema siikubali.

Ndiyo nikasema kama ni suala ambalo linatokana na mtoa hoja, ndiyo maana mtoa hoja yeye anayachukua haya na wataalamu wake wapo, watakuja kuyajibu. Yale ya lugha ambayo siyo ya Kibunge, nategemea Wabunge hatutasita mara moja kusimama na kusema kuhusu utaratibu. Maana lugha ambayo siyo ya Kibunge, hairuhusiwi humu. Eeh, twende kwa misingi hiyo Waheshimiwa Wabunge.

Maadam nikiwa nimesimama, nitangaze wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro; Naibu Waziri wetu wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Olenasha. Tuna wanafunzi wa *UDOM* wanaotoka Wilaya ya Ngorongoro, wamekuja kwa hotuba hii. Karibuni sana vijana wetu. Hebu simameni. Eeh, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mdee, sasa tumekulindia muda wako ila dakika zkao meza inajua. Tunaendelea Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri Waheshimiwa Wabunge wa CCM wapya wasome Ilani...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, hebu endelea na hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Naendelea!

**MWENYEKITI:** Endelea na mchango wako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Naendelea! *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mimi ni *term* yangu ya tatu Bungeni.

**MWENYEKITI:** Ongea na Kiti Mheshimiwa Mdee!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wabunge wa CCM, vijana na watu wazima ambao wameingia, wametukuta sisi tukiwemo, mkasome vizuri Ilani ya CCM. Mimi huwa naipitia, kwa manufaa tu ya kujenga, kwa sababu mwisho wa siku, mafanikio ya Ilani yenu, ni mafanikio yenu na ni mafanikio ya Taifa. Kwa hiyo, hapa hatutafuti mchawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawashauri wakasome Mipango ya Maendeleo mbalimbali. Yaani usije ukawa umekuja mwaka 2010, basi unachukua ule Mpango wa Maendeleo wa 2010 ama 2015; unakuja 15 kwenda mbele. Lazima tujue tumetoka wapi, tunakwenda wapi ili tuweze kushauri vizuri. Kwa hiyo, tusichukiane, dhamira ni njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kwa sababu watu wamezungumza suala la utafiti hapa, ni kweli! Tuliazimia na Serikali ikakubali kwamba 1% ya pato la Taifa itaenda kwenye utafiti kwa sababu dunia ya sasa hivi bila kufanya tafiti ili uweze kujua unataka nini, huwezi kupanga mipango yako. Isipokuwa mpaka sasa fedha zinazotolewa kwa tafiti zinatia aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mwijage amekuja hapa, kwa sababu tu ameandika kwenye hotuba yake viwanda ambavyo vimekuwa *registered,* yaani watu wameenda kusajili tu pale *TIC!* Kwa sababu ameandika kwenye hotuba yake viwanda 224. Kila Mbunge anapongeza anajua viwanda vimeshafanyaje? Vimeshajengwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimepitia hivi viwanda 224, si tuko kwenye hotuba ya kilimo! Sasa wamezungumza watu, hakuna kilimo bila *raw materials,* viwanda gani hivyo? Nimeangalia hapa viwanda 224, robo tatu viko mjini Dar es Salaam. Halafu viwanda vyenyewe basi ukienda kuangalia *deep into details* unaweza ukacheka, ufe mbavu, uzimie na ufe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wamezungumza watu hapa suala la pamba, nikasema hebu ngonja niangalie, kwenye hivi viwanda 224 hivi kwenye hiyo mikoa, kwenye robo hiyo chache basi, hivi viwanda vya kuiongezea hadhi Pamba vipo? Hakuna hata kimoja!

Sasa unajiuliza hivi wale ndugu zetu wa Kanda ya Ziwa hususan mikoa ambayo inalima pamba, pamba

ambayo ni zao muhimu, akiwemo Mheshimiwa Mtemi Chenge, hamko kwenye mipango ya Serikali, halafu anasimama mtu hapa anapongeza, eti tozo. Yaani tozo isingekuwa *issue* kama wakulima wetu hawa tungewapa mitaji; kama tungeweza kuweka miundombinu na tungetoa fursa za kilimo! Tozo siyo *issue! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hiki kitabu, mlisema juzi hapa kwamba hii Serikali ni moja, siyo kwamba Wizara ni ya huyu, ni wa huku, Serikali ni moja! Hivi iweje leo ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Kilimo…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hivi vitabu viwili, moja ni mbingu, nyingine ni dunia. Hivi vitabu havikutani. Kwa hiyo, sasa sisi tunaiomba Serikali jamani, tuache kutumia, sijui tuliwanyima Watanzania elimu! Tuna-*take advantage* ya kuwanyima elimu, maana tumeambiwa 31% ya watu ambao hawajui kusoma na kuandika. Sijui tunafanya makusudi ili ukienda na hoja nyepesi unaijengea maghorofa kama vile hiyo hoja ndiyo ulikuwa umeahidi, kumbe ulikuwa umeahidi kitabu kinene hivi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa dhamira nzuri kabisa, tuisaidie nchi! Yaani naomba kwa nia njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo alituambia mwaka 2013 kulikuwa kuna sera mpya ya kilimo. Hivi ni vitu gani ambavyo viko kwenye Sera ya Kilimo ya 2013 ambavyo vimekuwa *reflected* huku, yaani inauma! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia masuala ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Mwaka 2011 tulileta hoja binafsi hapa, miaka saba kama siyo sita iliyopita, tukaiambia Serikali tufanye *land auditing* nchi nzima ili tuweze

kujua kila kipande cha ardhi cha nchi yetu anayo nani? Kama ni mwekezaji, kama ni mkulima, kama ni mfugaji ili tuweze kupanga matumizi bora ya ardhi, Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka sita iliyopita nilitoa hiyo hoja, Bunge likaunga mkono, likawa Azimio la Bunge na aliyekuwa Waziri wa Ardhi akafanya mabadiliko kidogo. Tukasema tukifanya hivi, tutaweza kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji, tutaweza kujua mashamba makubwa ambayo yako chini ya wawekezaji ni mangapi. Tutaweza kujua wakulima wetu wadogo na wafugaji wakoje, ili tuweze kupanga mipango kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka sita baadaye Azimio la Bunge ambalo nadhani lilikuwa ni la kihistoria kwa pande zote; Waheshimiwa Wabunge wa Chama Tawala na Upinzani tuliungana tukasema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Muda wetu ndiyo huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Willy Qambalo ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hii Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba aliyetangulia amesema hatupaswi kupongeza, lakini wanasema usiposhukuru kwa kidogo, hata kwa kikubwa hutashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambayo imefanywa na Wizara hasa ya kuondoa hizo tozo ambazo ndizo kero kubwa kwa wananchi wetu, ni kazi nzuri ambayo inahitaji

kupongezwa. Vilevile naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa nzuri. Taarifa nzuri kwa maana gani? Wizara imeendelea kuzungumza aidha madhaifu au mafanikio, yote wameendelea kuyaweka bayana. Hii siyo kwa sababu nyingine; wamefanya hivyo ili waweze kupata ushauri. Mheshimiwa Waziri, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninachohitaji tu kusema, mfano ukisoma kwenye ukurasa wetu wa nne unasema, kilimo kinachangia asilimia 65 ya ajira; lakini ameendelea kusema, kwenye upande wa chakula kilimo kinachangia asilimia 100 na kwenye pato la Taifa kinachangia asilimia 29. Hii ameisema kwa sababu ya kuonesha hali halisi na umuhimu wa kilimo. Tunapokuja kwenye ukweli ni kwamba kwa kweli Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni Wizara ambayo haikupewa fedha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kupitia kwenye hiki kitabu, ukiangalia pale *page number* 27 na 28, kwenye miradi ya maendeleo ya mwaka 2016/2017, zile fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa, shilingi bilioni 800, zilizotolewa ni 4% peke yake, kwa maana ya shilingi milioni 280. Fedha za wafadhili ndiyo zimetoka kidogo kama shilingi milioni 900 ambayo ni asilimia 12. Kwa hiyo, hii tu inaonesha kwamba ni kweli tuna changamoto kubwa kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia, leo sisi hasa watu wa Kanda ya Ziwa tunalia sana tatizo la kilimo kwa maana hatuna chakula. Siyo kwamba ni wavivu lakini ni kwamba tunalima, tukishalima kwa sababu ya kukosa maji, kile chakula kinakufa. Bahati nzuri ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba, ukipita tu pale Magu utawaona wako pale vijana wa Kisukuma wanahangaika na vi-*pump* vya maji, tena vile vya petrol, vi-*pump* vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe kinachopaswa kufanyika pale ni kwamba, ukiangalia kwenye mabonde kama haya tuliyonayo mengi, ni kwa nini basi tusianzishe zile *irrigation scheme* tena kwa utaratibu rahisi tu, tunatangaza

*tender* kama tunavyotangaza *tender* za barabara? Nani anataka hizi hapa ekari 3,000 aje afanye *irrigation! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kuwalipa, ule mpunga wenyewe kama ni mpunga ambao ukiangalia mchele una soko kubwa Kenya, Uganda, Rwanda na tuna soko kubwa la ndani. Kwa hiyo, ni kwamba wale wakulima wenyewe wataweza kulipa zile gharama za kuendesha shamba lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya maeneo tuliyonayo yako mengi. Nilidhani tu kwamba kupitia ile Benki ya Kilimo ni vizuri basi tukaweka mkakati mahsusi kwa ajili ya kilimo cha *irrigation* na hii itatupunguzia adha ya chakula; hii ambayo kila leo tunaipigia Serikali kelele kusema Serikali ilete chakula. Tunaamini kwamba Serikali kwa majukumu iliyonayo na kwa shughuli ilizonazo, fedha za kuweza kutuletea chakula hazipo. Kwa hiyo, nilidhani kama Mheshimiwa Waziri atauchukua huo ushauri, atakuwa ametusaidia katika upande huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumze kidogo kuhusu uvuvi. Sisi pale kwetu Musoma Mjini tunavyo viwanda visivyopungua vitano vya samaki. Kwa taarifa yako na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri anafahamu, vile viwanda vyote vimekufa. Vile viwanda vimekufa siyo kwa sababu nyingine, ni kwa sababu ya uvuvi haramu, wale samaki wameisha, vile viwanda kwa Musoma Mjini vilikuwa vinachangia uchumi kwa kiasi kikubwa sana, lakini siyo Musoma tu, hata Mwanza vile viwanda vya samaki vimekufa, hata kule Bukoba vile viwanda vya samaki vimekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi nini kifanyike? Njia pekee ni kwamba lazima uvuvi haramu uendelee kupigwa vita. Mheshimiwa Waziri yeye anao ushahidi, pale kwetu Musoma Mjini bahati nzuri tunaye *DC* mmoja anaitwa Anney Vincent. Ni *DC* ambaye hata Mheshimiwa Waziri anajua amefanya kazi nzuri sana. Kwa Musoma Mjini, uvuvi haramu haupo; lakini sasa cha ajabu ni kwamba ukiondoka tu pale

Mjini, ukianzia Bunda na kuelekea kwenye maeneo mengine, ule uvuvi haramu unaendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ndio hivyo, maana yake ni kwamba hata ile juhudi anayoifanya ya kuhakikisha kwamba huu uvuvi haramu unaisha, maadamu anafanya katika eneo moja, tafsiri yake ni kwamba hao samaki watakuwa wanaenda maeneo mengine na wataendelea kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa kazi ile iliyofanyika, mpaka hivi sasa, angalau kwa pale mjini samaki tunaokula ni wale wazuri. Sasa kinachotakiwa kufanyika ni kumwangalia mtu kama huyu tukampa *overall* ya Ziwa Victoria akahakikisha kwamba anapata *resources.* Naamini wale wenye viwanda watachangia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanazuia uvuvi haramu. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo, tunadhani kwamba itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine dogo, hebu tuanzishe vile vikundi vinavyofuga samaki kwa njia ya *caging* ambapo wakifuga vile wale wenyewe watakuwa walinzi wakubwa wa wale wanaovua uvuvi haramu. Kwa kufanya hivyo, itatusaidia sana kuhakikisha kwamba hilo tatizo la uvuvi haramu linaisha, viwanda vyetu vinafufuka na uchumi wetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niguse kwenye upande wa ufugaji. Kwa kweli kwenye ufugaji bado hatujafanya kitu. Hatujafanya kitu kwa sababu gani? Tunazo *ranch* nyingi, nimeangalia hapa kwa haraka haraka, tuna *Sao Hill,* Mabuki, Kitulo mpaka *ranch* yetu ya *NARCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisoma kwenye ukurasa wa 110 pale, Mheshimiwa Waziri mwenyewe anasema kwamba kwa mwaka 2016 tumeweza kuzalisha mitamba 634. Sasa hizi *ranch* zote zina uwezo wa kuzalisha mitamba 634 peke yake? Tafsiri yake ni kwamba zile *ranch* tumewapa watu wachache wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenyewe bahati nzuri ni mfugaji, unapozungumza mitamba 634 hiyo, ukienda kwenye zizi langu pale kwenye wale ng'ombe nilionao, unawapata hao mitamba 634, tena mitamba wazuri na wa kisasa. Hata siku moja niliweza kuleta ng'ombe wangu hapa Dodoma machinjioni, bahati nzuri nikamwalika Mheshimiwa Naibu Waziri, alifika akawaona. Ng'ombe mmoja nilikuwa nauza siyo chini ya shilingi 1,200,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumbe tunachohitaji kufanya katika kusaidia mifugo, ushauri wangu ni kwamba hizi *ranch* nyingi tulizonazo, hebu tuwachukue wale wafugaji wanaofanya kazi ya kunenepesha. Hata ukipita pale Mwanza baada ya Coca Cola hapo njiani utakuta Wasukuma wapo pale wanahangaika, wanalisha mashudu, hakuna eneo la malisho. Ukiangalia hizi *ranch* nyingi tulizonazo hizi, zimekaa tu. Hivi kwa nini tusiwapangishe waka-*lease,* halafu wakaweza kufuga mifugo ya kutosha, mingi tukaweza kuendelea?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wetu.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fatma Toufiq, atafuatwa na Mheshimiwa Qambalo na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hii hotuba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika kuandaa bajeti hii. Napenda tu nimtaarifu mwanangu Mheshimiwa Halima Mdee kwamba

unapokuwa unatoa pongezi ni kwamba unathamini muda na kazi ya mtu ambaye amefanya shughuli hiyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tuna kila sababu ya kukupongeza; na kweli katika kuandaa *document* kama hii siyo kitu cha mchezo. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba kutoa mawazo, kukubali au kukataa kitu, ni haki ya mtu yeyote. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kukusoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelichangia hilo. Sambamba na hilo, bila kilimo, viwanda haviwezi kupata malighafi. Hivyo basi, maisha ya Watanzania hayawezi kuwa na tija bila kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee, Mkutano wa Maputo ambao ulikutana kuanzia tarehe 10 Julai hadi Disemba, 2003 ambapo viongozi wa Afrika walikutana kwa pamoja na walikubaliana kwamba asilimia 10 za Bajeti za Serikali katika nchi za Afrika ziende katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana, naona kwamba Serikali yetu bado haijafikia lengo hilo na hali kadhalika haijafikia nusu ya lengo hilo; kwamba hadi sasa hivi bajeti yetu ya kilimo ni 4.2% lengo ambalo kwa kweli bado lina hatihati sana. Kwa hiyo, naishauri Serikali yangu sikivu kwamba ione umuhimu wa kuweza kuongeza bajeti ya kilimo kama kweli tunataka kufika katika viwanda vya kati au uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ili wananchi waweze kufaidika kwa kilimo, waweze kujitosheleza kwa chakula na kupata ziada ya kilimo ili wawe na maisha ambayo ni bora, lazima kilimo kitiliwe mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa tisa wa hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri, amebainisha kuwa Halmashauri za Wilaya 55 zina upungufu wa chakula kutokana na uhaba wa mvua, lakini hapa hali halisi ni kwamba kwa sababu zinategemea zaidi mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa sana ya wakulima wengi kutegemea mvua kwa ajili ya kilimo ndiyo imesababisha ukosefu wa chakula, mvua ambazo mtawanyiko wake hauridhishi na pengine mvua hizo huzidi na kuleta madhara makubwa ambayo hayana tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wamezungumza na wamebainisha kwamba suluhisho pekee ili tuweze kupata mazao ya kutosha pamoja na usalama wa chakula katika nchi yetu, ni budi tujikite kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo basi, Serikali ina kila sababu ya kuandaa miundombinu rafiki zaidi katika kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo kutumia mito ya kudumu, ambayo ninaamini tunayo, mito ya msimu, chemchemi za asili, mabwawa ya kuvuna maji ya mvua na miradi inayotumia visima virefu na vifupi. Naamini kabisa ikiwa Serikali itakuwa na nia ya dhati, tukitumia utaratibu wa umwagiliaji, basi suala la upungufu wa chakula litakuwa ni historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuongelea ni suala la mbegu na pembejeo. Wenzangu wengi wamelizungumzia, taarifa zilizopo ni kwamba nchi yetu ina uwezo wa kuzalisha mbegu kwa asilimia 35 tu, kiasi ambacho ni kidogo sana. Kwa hiyo, inabidi sasa Serikali ikabuni mkakati mbadala. Hapa nchini tuna vyuo mbalimbali vya *MATI*, mfano tuna Chuo cha Mlingano - Tanga, tuna Chuo KT - Kilimanjaro, tuna Ukiriguru - Mwanza, Igurusi, Muhongo - Kigoma, *MATI* - Ifakara na vinginevyo kwa kuvitaja. Hebu Serikali ione jinsi gani itakavyovitumia vyuo hivi kwa kuzalisha mbegu ili mwisho wa siku tatizo la upungufu wa mbegu liweze kupungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Halmashauri za Wilaya pia zinaweza zikaanda mashamba darasa ya kutosha na hatimaye hili suala la kuagiza mbegu kutoka nje likapungua badala yake mbegu zikawa zinazalishwa humu humu nchini. Wenzetu katika Kamati walishauri kwamba uwepo utaratibu wa kulima kufuata Kanda maalum.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hata pia katika mbegu, basi ingefanyika utaratibu huo ili kusudi nazo mbegu ziweze kuzalishwa kikanda, nikiamini kabisa na hiyo pia inaweza ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Kuzalisha Mbegu, hawa *ASA,* inabidi nao wajitahidi, waweke malengo makubwa zaidi ili kusudi mbegu ziweze kupatikana kwa wakati na hatimaye suala la kupunguza ukosefu wa mbegu liwe ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu upungufu baadhi ya wataalam, Mabibi na Mabwana Shamba ambao pia imekuwa ni tatizo au kikwazo katika suala zima la kilimo; na hawa wamekuwa na tatizo kubwa sana kwa sababu hawana vitendea kazi vya kutosha. Kukosekana kwa vitendea kazi hivi kunawafanya washindwe kufanya kazi zao kwa ufanisi, hivyo hata kule vijijini ambako wangeweza kwenda kuwasimamia wale wananchi kwa kuwapa utaalamu inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, Serikali ione jinsi gani ya kuwapatia magari, pikipiki, mafuta na vile vifaa ambavyo vinastahiki ili kusudi waweze kufanya kazi zao kwa utaratibu unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililotaka kulizungumzia ni suala la masoko, wenzangu wamelizungumza pia. Pamoja na kwamba baadhi ya wakulima wengi sana wanajitahidi kulima, lakini suala la masoko imekuwa ni tatizo, kwa mfano, katika Mkoa wa Dodoma tunalima sana zabibu, lakini bado soko la zabibu ni dogo. Kwa kweli inabidi tuone Serikali inafanya utaratibu gani kuhakikisha kwamba soko la zabibu tunapata watu wengi zaidi au wawekezaji wengi zaidi ili wawekeze kuweza kusindika mazao ambayo yanatokana na zabibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia, najua muda unanitupa mkono, ni suala la utumiaji wa teknolojia duni. Kwa kweli bado tuna kila sababu ya kuona tunapata wataalam wengi zaidi kwa ajili ya kuwa na teknolojia ambazo ni za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ukosefu wa zana stadi za kilimo bado wananchi hawajaacha jembe la mkono. Kwa kweli bado jembe la mkono linaturudisha nyuma sana katika kilimo, wananchi wengi hawana uwezo wa kukopa hizi zana za kilimo. Kwa hiyo, bado tuna kila sababu na Serikali ina kila sababu ya kuhakikisha kwamba wananchi wake wana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Willy Qambalo, atafutiwa na Mheshimiwa Bupe na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia katika sekta hii muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi, lakini pia kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaongea juu ya sekta inayoajiri zaidi ya asilimia 65.5 ya wananchi wetu. Suala la ajira nchi hii limekuwa ni jambo ambalo halijawahi kupata suluhu; lakini hapa tunayo sekta ambayo inaajiri asilimia 65 ya watu wetu, lakini ni sekta ambayo pia tunaipa fedha kidogo kiasi hicho. Takwimu zimetuambia Sekta ya Kilimo mwaka 2015 na mwaka 2016 imechangia asilimia 29 ya pato la Taifa. Nadhani tuna kila sababu ya kuitizama sekta hii ili iweze kuchangia pato la Taifa kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea asilimia 65 ya Watanzania, Watanzania waadilifu, watiifu ambao wamebaki vijijini wanazalisha, siyo wale waliokimbilia mijini, lakini Watanzania hawa ni wale ambao wanakumbana na

changamoto mbalimbali za kimaendeleo. Ukija ukame ni wao; wadudu waharibifu ni wao, kwelea kwelea ni wao, tatizo la maji linaandama kundi hili, lakini bado ni kundi ambalo mimi kwa mtazamo wangu naona hatujalitendea haki kikweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tumeanza kujadili bajeti za Wizara ni kama tumefika nusu ya safari. Sasa mimi sijui hizi fedha pengine hizo Wizara zinazokuja ndiyo zitapewa asilimia hizo nyingi 70%, 80% na 90%, lakini tangu tumeanza ni 3%; sana sana tumekwenda mbele asilimia 50 na kitu. Hizi fedha zinasubiri kupangiwa Wizara ipi, kama Wizara nyeti kama hii inapewa fedha kidogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kilimo cha zao la mahindi. Zao la mahindi ni zao la biashara lakini pia ni zao kuu la chakula kwa maeneo mengi ya nchi yetu. Zao hili kwa takwimu za kitabu cha Waziri linachangia karibu tani milioni sita kwa mwaka. Tukiwa *serious* tunaweza kuzalisha zaidi ya mara tatu au nne ya kiasi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa kwenye kilimo cha zao la mahindi ni suala la mbegu. Utafiti unaonesha kabisa ukilima mahindi ukatumia zile mbegu zetu za asili, zile za kuchukua tu, utavuna kidogo, lakini ukipanda mbegu zile zilizoboreshwa, utapata angalau kiasi cha kutosha kwa heka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wamesema, mbegu za mahindi ambazo zimeboreshwa ni ghali sana na sehemu kubwa inatoka nje ya nchi. Sasa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, mimi sijui wataacha *legacy* gani mtakapoondoka katika eneo hili la kilimo cha mahindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tunaomba ili tuwakumbuke mtuambie Kampuni ya *TANSEED* iliyokuwa inazalisha mbegu nchini miaka ya nyuma, imekwenda wapi? Mtuoneshe hilo kaburi mahali lilipo tukafufue ili tuzalishe mbegu ndani ya nchi yetu ili bei ya mbegu iwe rahisi.

Wakulima wengi wanajitahidi sana, wanalima kwa muda, lakini linapokuja suala la kupanda, kwa kweli mbegu inawakwaza. Mwisho wa siku wanaishia kwenye kupanda kile chochote ambacho ama amenunua dukani au amepewa chakula cha msaada na matokeo yake kwa heka anaishia kupata gunia mbili au tatu. Tunao uwezo wa kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kama tutazingatia suala la mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye zao la mbaazi. Kwa miaka ya karibuni, zao la mbaazi limekuwa ni mkombozi kwa wakulima wengi kwenye zile kanda ambazo zao hili linalimwa. Msimu wa mwaka 2015 zao hili lilikwenda kwa kilo karibu shilingi 3,000, msimu wa mwaka 2016 zao hili likashuka hadi shilingi 900; wakulima wamechanganyikiwa, wamekosa hamu ya kulima zao hili kwa sababu bei hailipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu mliopo kwenye dawati la Wizara...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea na mchango wangu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara hebu itusaidie kutuunganisha na masoko ya zao hili yalioko ndani au nje ya nchi ili wakulima wetu waweze kupata bei nzuri.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ambayo ni ya muhimu kidogo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwenye eneo hili ni suala la wanunuzi wa zao hili. Wapo wanunuzi ambao hadi leo tunapoongea, bado hawajawalipa wakulima fedha zao baada ya kuchukua mbaazi zao. Tunaomba Mawaziri mtakapokuwa mnahitimisha mtuambie, wanunuzi wa mazao kama hawa, ambao wanawakopa wakulima mwaka mzima, wachukuliwe hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye eneo la pembejeo. Wenzangu pia wamelisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejaa wataalamu wa kila aina na wa kila rangi, hivi inawezekanaje pembejeo zinachelewa kwenda kwenye maeneo yanayohusika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnajua watu hawa wanahitaji mbegu kwa ajili ya kupanda; msimu wa kupanda ni Januari, lakini mbegu zinaenda mwezi wa tatu za kazi gani? Kwa hiyo, nadhani kuna vitu vingine tunapopiga kelele, sijui tatizo lipo wapi? Kwa nini hayo marekebisho yasifanyike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hata kabla sijaingia Bungeni, suala la ucheleweshaji wa pembejeo limekuwa ni jambo ambalo halijapata ufumbuzi. Nadhani ni vitu vidogo sana. Suala la kalenda ya kilimo kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu inafahamika; na pembejeo hizi kwa bahati nzuri au mbaya inawalenga watu wachache. Hivi inashindikana nini kupeleka tani tano au kumi kwenye Wilaya X kwa muda ili wananchi wale waliolengwa walime pia na kupanda kwa muda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili jambo linawezekana. Hebu mzizi huu sasa ukateni, fitina kwenye eneo la ucheleweshaji iishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani ni watu muhimu sana kuwasaidia wakulima wetu, lakini tunao wachache sana.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani katika Wizara hii kama kuna eneo ambalo mnaweza kuwatendea haki wananchi wetu ni kuwapeleka Maafisa Ugani wa kutosha. Wale wachache walioko vijijini, sasa hivi ndiyo wamekuwa *Acting WEOs* na *Acting VEOs* hawafanyi zile kazi zao ambazo zimewapeleka kule. Kwa hiyo, naomba Maafisa Ugani pia wapewe uwezeshwaji wa vifaa vya usafiri ili waweze kuwafikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amechelewa kupiga marufuku uchinjwaji wa punda. Amechelewa kabisa! Nilitegemea angesema kesho. Wanyama hawa wanaisha na wanyama hawa wanazaliana kidogo kidogo sana. Kule vijijini wanyama hawa ambao walikuwa wanatusaidia kusafirisha vitu, kuchota maji na kupeleka vitu sokoni, sasa hivi wanaibiwa hovyo.

Kwa hiyo, naomba suala la kupiga marufuku ikiwezekana punguza huo muda. Siku 45 zinatosha kumaliza punda katika nchi hii. Hao wanaofanya biashara ya punda, sasa hivi wamebadilisha mbinu nyingine, wanawachinja huko huko na ngozi wanazichukua na wanapeleka huko wanakopeleka. Wanyama hawa ili wasiishe, hiyo marufuku naomba ipunguze muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya suala la kilimo cha umwagiliaji. Kilimo chetu kwa muda mrefu kimekuwa ni kilimo kinachotegemea mvua. Hebu tuchukue jitihada za makusudi za kuelekea kwenye kilimo cha umwagiliaji. Nchi hii, leo mvua inanyesha, baada ya wiki mbili, tuna shida ya maji. Tuwekeze kwenye miradi mikubwa mikubwa ambayo itachochea kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Olenasha jirani yangu, anafahamu kwamba sisi Mang'ola ni wakulima wazuri sana wa vitunguu na tunazo chemchemi zenye uwezo mkubwa wa kumwagilia mwaka mzima, lakini tatizo letu mifereji ile ya kumwagilia haijajengewa. Hebu wekeni mpango tusaidieni wananchi wa Mang'ola waweze kumwagilia vizuri baada ya ile mifereji kujengewa ili maji yafike kwa wakulima walioko upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee juu ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro hii imekuwa ni ya muda mrefu. Jitihada mbalimbali zimefanyika, lakini jambo hili naishauri Serikali, hebu lifike mwisho. Hawa watu wawili wote ni Watanzania; hebu tuwekeni pamoja kwenye meza moja tuongee, tusiwe tunagomba kila siku. Nchi hii imetawaliwa na migogoro ambayo haiishi. Kila mmoja hapa anachangia

kwenye pato la Taifa. Huyu mfugaji kwa sehemu ni kama alikuwa ameachwa achwa, ni kama hakulindwa. Ifike mahali tutambue kwamba hata ndugu zetu wafugaji wana mchango kwenye pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kuchungia hayapo. Serikali sasa hivi inasema tutenge maeneo, hivi tutatenga kutoka wapi? Hivi ukisema Wilaya ya Karatu tutenge maeneo ya kufugia, yako wapi? Hebu mje mtembee mwone, hakuna eneo la kufugia! Pia mje na mpango ambao utatusaidia hata yule ng'ombe moja au wawili tuwafuge kwa ubora ili watupe kile ambacho tunataka. Mkisema tuuze ng'ombe, hivi mnadhani wafugaji hawajui mahali minada ilipo? Tunajua mahali minada ilipo, lakini hatuuzi kwa sababu ng'ombe ni benki yetu. Sasa ukiniambia niuze, wewe mbona *accounts* zako za *NBC* na *CRDB* hufungi? Kwa hiyo, suala siyo kuuza mifugo, suala ni kumsaidia mkulima ili afuge kwa kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwenye eneo la hifadhi ya chakula. Tunapoteza chakula kingi kwa sababu ya uharibifu unaofanywa na wadudu. Takwimu zinasema, karibu asilimia 40 ya tunachokivuna, kinapotea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Balozi Kamala ajiandae.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, hatimaye kuwawakilisha wananchi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote kwa uchapakazi wao mzuri na uwajibikaji. Hakika hawa Mawaziri hawajakaa maofisini kama tunavyojua Maofisa wanavyokaa maofisini kusubiri changamoto. Wamekuwa wakizunguka Mikoa kwa Mikoa, Majimbo kwa Majimbo kuhakikisha wanajua changamoto za wananchi. Mheshimiwa Rais hakukosea kuwateua, hakika Mungu awasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pamoja na changamoto wanazozipata za hali ya hewa, lakini wamekuwa wakichapa kazi kuhakikisha wanaendeleza Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uchapakazi wake mzuri, kwa uwajibikaji, hatimaye kuliletea Taifa nidhamu. Rais huyu amekuwa akifanya kazi usiku na mchana japokuwa kuna watu wamekuwa wakimbeza wakisema Rais huyu ni wa ajabu, siyo kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais huyu ametenda maajabu ambayo hawakuyategemea. Rais huyu kwa muda mfupi tu ameweza kufanya mambo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ameweza kuhakikisha kwamba watoto wanasoma bure, pili, ametengeneza barabara zote, sasa hivi zinapitika kwa kiwango cha lami, tatu, ameweza kununua ndege, mmeziona, mmeshuhudia na nyingine bado zinakuja, Rais huyu amefanya mambo mengi sana. Amerekebisha mambo mengi sana! Ni mtambo wa kurekebisha tabia za mafisadi! Mungu amjalie huko aliko, nasi tupo nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye suala la pembejeo. Mkoa wa Rukwa umekuwa ni mkoa ambao unalima mazao mengi yanayokubali. Mkoa huu umekuwa ulikilisha mikoa mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi iangalie mikoa hii ambayo mvua ni za uhakika ipeleke pembejeo kwa wakati. Huu mpango ambao umeanza kutumia mawakala, naomba mawakala wapeleke pembejeo kwa wakati hatimaye wananchi wa mikoa hii wapate kulima kilimo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la Benki ya Kilimo. Benki hii tunaisikia Dar es Salaam na Arusha. Nilikuwa naiomba Serikali, kwa sababu kuna mikoa ambayo mvua ni za uhakika na kilimo ni cha uhakika, ipelekwe benki hii ianzishe mabenki mikoa yote, ikiwezekana wilaya zote, wakulima waweze kukopa pesa za kulima na kukopa matrekta, itasaidia sana kuongeza kiwango cha kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la Soko la Samaki la Kimataifa. Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Kalambo lilianzishwa Soko la Samaki la Kimataifa, lakini mpaka sasa hivi soko hili linaonekana kama limetelekezwa. Kule Kalambo Ziwani kunapatikana samaki wengi sana ambao ni migebuka, sangara na samaki wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo inaonekana kwamba kwa sababu ya kukosa lile soko, kwamba halifanyi kazi, wanakuja Wakongo na Wazambia wanavua samaki mle tani na tani, wanapeleka huko. Serikali na Halmashauri zinashindwa kupata mapato na wananchi pia hawapati mapato, hilo soko haliwasaidii. Naomba Serikali ilifufue hilo Soko la Samaki la Kimataifa ili wananchi waweze kufaidiaka na Serikali pia iweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kututunzia muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Balozi Kamala ajiandae.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa na nzuri inayofanyika katika kufanya mabadiliko kwenye maeneo mbalimbali ambayo tumekuwa tukiyalalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa baadhi ya Wabunge ambao nimesikia hapa wakijaribu kutuelekeza namna ya kusema; nawaomba wasifanye hivyo, kwa sababu Wabunge hapa tuko wengi, nchi yetu ni kubwa na mazingira yanatofautiana sana. Kwa hiyo, mawazo ambayo nitayatoa kutokana na mazingira yangu ya Msalala ni tofauti sana na mawazo ya Mbunge mwingine. Kazi ya Serikali ku-*coordinate* na kuweza kuchukua hatua za kurekebisha pale ambapo pana marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mambo yaliyofanyika ni makubwa. Changamoto zilizoko kwenye kilimo ni kubwa sana, lakini hatua zinazofanyika zinaonekana. Tumelalamikia sana kwa mfano suala la tozo mbalimbali, kwamba linaumiza wakulima. Hatua zimechukuliwa, tumeona, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi kumekuwa na tatizo kubwa sana la uratibu na usambazaji wa mbolea. Mpango na utaratibu uliokuwepo kwa miaka yote ulikuwa unasababisha matatizo makubwa ya upotevu wa fedha za Serikali, lakini kubwa zaidi hata usambazaji wenyewe ulikuwa unafika wakati mbolea inasambazwa kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa hatua iliyochukuliwa ya sasa ya kufanya uratibu na

usimamizi wa ununuzi wa mbolea kwa kutumia huu mtindo wa *bulk procurement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono wazo hili, naamini litatusaidia. Tumekuwa na matatizo, hii ni hatua mojawapo ya kupata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushauri wangu kwenye hili eneo la mbolea ni kwamba ni lazima sasa kwa sababu mbolea itaagizwa na sekta binafsi ni lazima Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuthibiti bei; kama ilivyo kwenye mafuta kwamba wanaagiza na wanaelekezwa bei ya kuuzia kwenye maeneo mbalimbali watakayosambaza, pia bei elekezi ya mbolea itakayosambazwa iweze kutolewa na hao wasambazaji na mawakala wao kwenye hayo maeneo, waweze kutangazwa na wajulikane kwamba Wakala wa Mbolea kwa eneo kwa mfano kwangu Kahama ajulikane ni fulani na bei yake itakuwa ni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nishauri hivyo kwenye eneo la mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika utangulizi, mimi natoka Mkoa wa Shinyanga. Mkoa huu kwa miaka yote tumekuwa tukilalamikia tatizo la njaa. Naomba nifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba hata sasa hivi Mkoa wa Shinyanga hali ya chakula hairidhishi. Tumetoka kwenye kipindi chenye changamoto za mvua za vuli mwezi, Novemba, Disemba, zimenyesha kweli. Kufika mwezi Januari, mvua zilikata kabisa na sehemu kubwa waliokuwa wamelima mahindi, hasa Wilaya ya Kahama, mahindi yote yalinyauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa mvua za masika zimeanza kunyesha tena mwezi wa Pili, wakulima wakajaribu tena kulima kwa mara nyingine, lakini cha ajabu kukatokea funza! Siyo viwavijeshi, lakini ni aina fulani ya funza wa ajabu sana ambao wameharibu mazao yote. Mheshimiwa Waziri tuliongea kwamba moja ya tatizo kubwa

tulilolipata kama wananchi na wakulima ni kutokupata mwongozo wowote kutoka kwa Maafisa Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walikuwa wanahangaika kukabiliana na hawa funza bila kujua watumie dawa gani? Wapo waliokuwa wakishauriwa watumie sabuni na kuchanganya na majivu, haikusaidia; wapo walioelekezwa kutumia dawa za mifugo, haikusaidia; na mwisho mazao hayajapatikana. Kwa hiyo, naomba katika msimu ujao wa kilimo ni muhimu Serikali kuwa imeshajua tatizo la hawa wadudu ni nini? Au hao wadudu ni wa aina gani? Dawa gani itumike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba Serikali hapa, siyo lazima itununulie dawa, ielekeze tu kwamba wadudu hawa wanauawa kwa dawa hii, wakulima tumieni dawa hiyo. Itawasaidia sana wakulima. Watu wa Shinyanga ni wakulima wazuri, wala hawahitaji kusukumwa kwenda shambani. Kwa mazingira tuliyonayo kwa sasa, kabla ya kufika msimu ujao wa kilimo, tutakuwa na tatizo la njaa. Nilikuwa naiomba sana Serikali, kumekuwepo na utaratibu wa Serikali kusaidia mbolea kwa miaka ya nyuma na kusaidia kuwezesha maeneo mengine ambayo mvua zinanyesha, wazalishe kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtizamo ni kwamba huko wanakozalisha, mikoa ile ya *G5* Iringa, Morogoro, Rukwa na kadhalika, wazalishe kwa wingi. Halafu baada ya kuwa wamezalisha chakula kile kiweze kuuzwa kwa bei nafuu kwenye mikoa ambayo ina shida kama Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kwa hiki kipindi isaidie kuratibu zoezi hili. Wafanyabiashara ukiwaelekeza tu bila kuwasaidia namna yoyote ya kuwapa *incentive,* bado hawawezi wakafanya biashara na hawawezi wakapunguza tatizo la bei. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kwa hiki kipindi kabla ya msimu ujao wa mvua, ifahamu kwamba Mkoa wa Shinyanga tuna tatizo la uhaba wa chakula na isaidie kuratibu upatikanaji wa chakula cha bei nafuu kabla ya kufika msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu ujao utakapofika, naimba sana Serikali isaidie jitihahada za Serikali ya Mkoa wa Shinyanga kuanzisha kilimo cha umwagiliaji. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge Azza kwamba mwaka 2010/2011 Serikali ya Mkoa wa Shinyanga iliandaa mpango kabambe wa kupambana na njaa katika mkoa na iliweka mkoa katika kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda mojawapo iliyobuniwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ni Halmashauri ya Wilaya Shinyanga Vijijini kwa maana ya Jimbo la Solwa pamoja na Jimbo la Msalala ambalo lina bonde zuri sana linalotoka maeneo ya Mwakitolyo kuungana kule kutoka mkondo wa Ziwa Victoria hadi kuja kwenye Kata za Mwanase, Kashishi, Bulige, Isaka pamoja na Isakajana kwa jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji na taarifa zilishafika Wizarani. Naomba sana, jitihada hizi zilizoanzishwa na mkoa ziungwe mkono na Serikali ili badala ya kuomba chakula kila wakati, badala ya kuomba Serikali iingilie kati kupunguza bei ya chakula katika eneo hili, wananchi hawa waweze kulima na mvua zinanyesha, pamoja na kwamba zinanyesha kwa muda mfupi, maji yanapatikana, basi waweze kulima kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu tulipendekeza kuanzisha Soko la Kimataifa la mchele kwenye eneo la Bulige na mradi ukawa umekwishaanza kwa maana ya kuanza kujenga soko. Kwa bahati mbaya uendelezaji wa mradi huo mwaka 2013/2014 ukawa umesuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara isikume mradi huu utekelezwe ili kama mkoa tulivyopanga na Halmashauri na Jimbo kwamba mpunga uzalishwe kwa wingi kwenye eneo hili la Solo na Msalala na soko kubwa la mchele liweze kuwepo pale Bulige; na kwa kufanya hivyo umasikini utapungua na wananchi wataweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kwa dakika chache zilizobaki, nataka kuishauri Serikali kwa upande wa uvuvi, ielekeze nguvu katika ufugaji wa samaki. Uvuvi wa samaki kutoka kwenye mabwawa na maziwa ambayo tayari yapo, hauna tija sana. Tujifunze kutoka nchi kama Vietnam ambayo zaidi ya asilimia 80 ya samaki wanaouzwa kwenye soko ni wale wanaofugwa kwenye vidimbwi vidogo vidogo. Jambo hili linawezekana na linaweza kikaongeza sana tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa migogoro ya wakulima na wafugaji, naomba sana Serikali iongeze juhudi katika kusaidia wafugaji kupata malisho. Ukisikiliza chanzo cha migogoro, ni malisho *versus* maeneo ya kulima. Sehemu kubwa ya maeneo makubwa ambayo yamekuwa malisho miaka ya nyuma kwa mfano Mkoa wa Shinyanga ambao unalima na kufuga, maeneo mengi ambayo yamekuwa ni ya mifugo, sasa wanalima. Kwa hiyo, wafugaji wanajikuta hawana maeneo ya kufugia, wanaendelea kuhama kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mjadala kuhusu suala hili kwamba yatapatikana maeneo ya kuwasaidia wafugaji wawe na maeneo yao watakayoyamiliki na kufuga bila kuhama. Naomba Serikali iharakishe kukamilisha zoezi hili ili maeneo ya wafugaji yajulikane, maeneo ya wakulima yawepo ili migogoro iweze kwisha. Siyo jambo zuri kukaa tunalalamikia jambo hilo miaka nenda, rudi na mwisho wa siku tunashuhudia mauaji ya wakulima au wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, mpango wa Serikali ni mzuri, pamoja na kwamba kuna maeneo ambayo naiomba Serikali iongeze nguvu. Naiunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Tizeba na rafiki yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Olenasha, ongezeni juhudi, sisi Wabunge tunaelewa mnachokifanya, tunajua mnafanya kazi kubwa na tutaendelea kuwaunga mkono. Tusaidieni katika hayo

ambayo nimeyasema na Wabunge wenzangu wameyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashidi Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala na Mheshimiwa Dunstan Kitandula jiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja iliyoko katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naanza kwa kuwapongeza Mawaziri wenye dhamana; Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Hili suala la tozo kwa kweli ni jambo ambalo lilikuwa linawarudisha nyuma wakulima wetu, kwa sababu hizi tozo zote zilikuwa zinakwenda kwa mkulima. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba kwa kuondoa hizi tozo zitaongeza tija pia zitaongeza uzalishaji pamoja na ari kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la utafiti hasa kwenye vyuo vyetu vile kikiwemo kile cha *MATI* - Mlingano. Kwa dhati kabisa tunaiomba Wizara itafute namna ya kuboresha tafiti mbalimbali za mazao ya kilimo. Sasa hivi kutokana na mabadiliko ya tabianchi, mazao mengi yameanza kukataa katika baadhi ya maeneo. Kule Lushoto sisi tulikuwa ni wakulima wazuri sana wa Kahawa, lakini sasa hivi kutokana na mabadiliko ya tabianchi, Kahawa imeanza kupotea. Hali kadhalika na Kilimanjaro hali pia siyo nzuri kama ilivyokuwa mwanzo. Kwa hiyo, tuombe hivi vyuo vifanye tafiti kuona namna gani wanaweza wakabadilisha mbegu ambayo itakuwa inaendana na mazingira ya wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kule katika Jimbo la Mlalo kuna *scheme* ya kilimo cha mpunga, kinaitwa *Mng'aro Irrigation Scheme. Scheme* hii imeanzishwa

mwaka 1985, wakati huo ilikuwa chini ya ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani *(FAO).* Linafanya vizuri sana kwa sababu tunalima mpunga lakini pia tunalima mahindi. *Scheme* hii ina uwezo wa kuzalisha mahindi mara tatu ndani ya msimu mmoja wa mwaka. Kwa hiyo, inasaidia sana kupunguza tatizo la upungufu wa chakula katika maeneo ya Mkoa wa Tanga, lakini na Mkoa wa Kilimanjaro kwa baadhi ya maeneo, hasa Wilaya ya Same na Mwanga. Tatizo kubwa ni mpunga. Mpunga unaolimwa katika bonde lile hauna thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukaamini hivi ninavyozungumza, gunia moja la mpunga kutoka Mng'aro ni shilingi 42,000. Kwa hiyo, unakuta mwananchi anatumia gharama kubwa sana wakati wa kulima, lakini wakati anauza mpunga huu hauna thamani. Kwa hiyo, naomba Wizara itusaidie kufanya utafiti ili tupate mbegu bora zaidi ambayo inaweza ikasaidia wakulima hawa waweze kupata soko zuri la kuweza kushindana na mpunga kutoka Kyela, Shinyanga, Ifakara na maeneo mengineyo. Kwa hiyo, tunaomba sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la malambo na majosho ya kuosha mifugo. Katika Halmashauri ya Lushoto tuna kata tatu ni tambarare; na hizi kata ndizo ambazo zina jamii ya wafugaji. Mwaka 1954 kabla ya Tanganyika huru, wakoloni wa Kijerumani walikuwa wamejenga lambo na josho mahali fulani na mpaka sasa hivi lipo. Pamoja na tatizo hili la kuchakata vyuma chakavu, lakini lile lambo bado lipo. Kwa hiyo, naiomba Wizara, na sisi katika Halmashauri tumeshaandika mpango wa kulifufua lile lambo ili tuwasaidie wafugaji hawa wasiingize mifugo katika Hifadhi ya Mkomazi, kwa sababu wakati mwingine hii migogoro ya wafugaji na hifadhi tunaisababisha sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwamba tusiweke huu mzigo moja kwa moja kwake, tumeanza katika ngazi ya Halmashauri. Kwa hiyo, tunaomba mtuunge mkono ili josho lile liweze kutumika, tuwapunguzie

wafugaji hawa adha ya kuingiza mifugo kwenye hifadhi na kupigwa faini ambazo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Pia nataka nimwelekeze Mheshimiwa Waziri kwamba katika Kata hizi nazozingumza ambazo zina wafugaji, pia tumeanzisha kilimo cha mazao ya mchaichai. Sasa hivi mchaichai una thamani kubwa sana duniani. Tumeanza majiribio katika ekari kama nne hivi na tumepata soko zuri, lakini soko lenye liko Pemba. Baada ya kuona kwamba zao hili linaweza likawa na tija, mwekezaji mmoja wa ndani ameagiza mtambo kutoka India na sasa hivi tunaweza tukakamua mchaichai katika Tarafa hii ya Umba ambayo ina Kata karibia nne ambazo zinalima mchaichai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwako kwamba unaweza ukaja ukajifunza huu ubunifu ambao tumeupata kule tukausambaza maeneo mengine ya nchi kwa sababu mchaichai hahutaji *sulpher,* hauhitaji pembejeo mbalimbali. Ni suala tu la kupanda, kunyweshea, baada ya muda unakata. Tani moja ya mchaichai ni shilingi 250,000. Kwa hiyo, naomba aje alichukue hilo kama shamba darasa la kueneza hiki kilimo maeneo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Suala ambalo lingine ambalo nilikuwa nalizungumzia ni suala *bulk procurement* ya mbolea. Hili ni jambo ambalo linakuja kutibu tatizo sugu ambalo tulikuwa tunakumbana nalo. Sisi kule Lushoto ni wakulima wa mboga mboga na matunda, lakini mara nyingi tulikuwa tunaulizwa mbona sisi wakulima wa mboga mboga hatupati ruzuku ya kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa kwamba ruzuku hii ilikuwa inaenda katika maeneo yale ya uzalishaji wa chakula. Sasa kwa kuanzisha *bulk procurement,* maana yake ni kwamba mbolea itapatikana kwa bei ya chini na nadhani kwenye bajeti ya mwaka 2016 Waziri aliyekuwa na dhamana wakati huo alituahidi kwamba lengo ni kuhakikisha kwamba mbolea inapatikana kama vocha ya simu; au akatumia lugha nyingine kwamba ipatikane kama ambavyo unanunua *CocaCola* dukani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwa utaratibu huu wa kununua kwa pamoja kama ambavyo tumejifunza kwenye mafuta, utaleta tija kwa sababu kutakuwa na bei maalum, lakini pia itasaidia kuhakikisha kwamba hata wale wafanyabiashara wa ndani wanaweza sasa wakaingia kwenye *fair competition.* Sasa hivi siyo rahisi sana kwa mwekezaji mdogo wa ndani ku-*compete* na makampuni yale makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia *bulk procurement* maana yake ni kwamba hata hawa wafanyabishara wadogo wadogo ambao ni wazawa wa ndani wanaweza sasa na wao wakaingia katika mfumo huu, wakaagiza kiasi cha tani wanazohitaji katika maeneo yao na itawasaidia pia kukuza mitaji lakini pia kukuza dhana nzima ya uchumi kwa maana ya upande wa wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu tangawizi. Halmashauri ya Lushoto tunalima tangawizi, Halmashauri ya Same wanalima tangawizi, kule Njombe na Madaba wanalima tangawizi na Kigoma na Rukwa nadhani pia wameanza, lakini changamoto ipo kwenye bei. Kwa sababu mara nyingi sana tangawizi inavunwa katika muda ambao unafanana bei yake huwa inashuka kutokana na suala la *demand* na *supply.* Kwa hiyo, nimsihi Mheshimiwa Waziri tuone namna ya kuwasiliana na Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji kupitia *TIRDO* na *SIDO* tupate mashine ndogo ndogo za kuweza kui-*process* na kuikausha kwa sababu tunauza ikiwa mbichi, hatuwezi tukaitunza muda mrefu. Hii itasaidia kuongeza tija lakini pia tukifanya hizi *processing* pamoja na *packaging* nzuri tunaweza tukaanza kuvuka kwenye masoko ya kimataifa na kuweza kuwasaidia hawa wakulima waweze kuona tija katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa ni huo, nitoe tu rai kwamba Wizara hii inafanya kazi kubwa, ina ma-*Extension Officer* mpaka kule kwenye vijiji, tunawaomba muwatumie vizuri. Hii ndiyo Wizara pekee ambayo ukifika katika ngazi ya kijiji unaikuta lakini nadhani kuna tatizo la *connection* kutoka kwenye Halmashauri na

kuja kwenye Wizara. Hebu tuitumie nafasi hii vizuri ku-*coordinate* na kuhakikisha kwamba ikitokea agizo la kitaifa basi huku chini wote wanawajibika. Tunapopita katika maeneo yetu tunagundua wakati mwingine hawa Maafisa Ugani hata hajui kwa nini yuko mahali pale. Kwa hiyo, nitoe sana wito kwamba kwa sababu mnayo hii rasilimali watu ya kutosha tuitumie vizuri kuhakikisha kwamba Wizara hii tunaitendea haki kama ambavyo tunaizungumza kwamba ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Kamala atafuatiwa na Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Rose Kamil Sukum ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jambo la kwanza, mpaka wa Tanzania na Uganda uko Mtukula, Minziro, Kakunyu na hauko Bunazi. Kwa hiyo, wale wote wenye mawazo ya kufikiri kwamba ukifika Bunazi umemaliza Tanzania na hivyo wanazuia mchele, mahindi na sukari kufika Mtukula. Naomba kuanzia leo ninapozungumza hapa wakome mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inaeleza na kubainisha kwamba kuna nia ya dhati ya kuanzisha masoko ya mpakani, masoko ya kimkakati. Huwezi ukaanzisha masoko haya na huwezi ukatekeleza mkakati huu kama una watu ambao wanafikiria mpaka wa Tanzania ni Bunazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuondoa tozo kama tulivyoziondoa ni jambo jema, lakini itakuwa na maana tu kama faida itamfikia mkulima moja kwa moja. Lengo pia liwe kuhakikisha sasa tunaongeza fedha anazozipata mwananchi kutoka asilimia 88 ya sasa walau tupandishe hadi asilimia 90 ya bei ya soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, makato ya 0.75% yaliyopunguzwa mpaka 0.375% ni jambo jema. Hata hivyo,

lengo na *best practice* ni kufuta kabisa mwisho wa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kinachoitwa mifuko ya mazao ambapo kuna fedha zinakatwa na kupelekwa kusaidia mifuko hiyo ni makosa kwa sababu tulipoamua kuondoa gharama za kuendesha bodi mbalimbali hatukumaanisha kuleta makato mengine tukayaita makato ya mifuko ya mazao. Jambo hilo likome mara moja kwa sababu ni kumbebesha mkulima gharama ambazo tulishaziondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, *cess* 5% ambayo tunamtoza mkulima wa kahawa kupitia kwenye vyama vya msingi si jambo jema. Nchi zilizoendelea duniani kama vile Vietnam, Mexico na India, hivi sasa hutoza 1% tu kwenye *border* na si vinginevyo. Huu utaratibu tunaweza kuufuata na ukatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, kumkata mkulima wa kahawa kilo mbili kila gunia kwamba hiyo ndiyo gharama ya gunia si jambo jema na ni wizi wa mchana. Ukienda maeneo mengi vijijini unakuta mizani haikaguliwi na matokeo yake unaweza ukapeleka kilo 50 ukaambiwa hizo ni kilo 45, huo ni wizi wa mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Kigarama, kuna mtawala mmoja anaitwa Pastory Kabeba, mtawala huyu amekuwa akisababisha hasara kubwa kwa kupima mwenyewe kwa kufikiria anachoona kinafaa na kumbebesha hasara mkulima. Jambo hilo likome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, soko la kahawa katika Afrika Mashariki tulikuwa tukifikiria sehemu tatu, tunazungumzia Jumuiya ya Ulaya, Sudan na Honduras lakini sasa *South Sudan* imeshajiunga na Afrika Mashariki. Kwa hiyo, badala ya kuzungumzia soko la Ulaya ambalo kwa maamuzi yetu tumeanza kujiondoa na kwa kuwa hatuwezi kuzungumzia Honduras, basi Mheshimiwa Tizeba peleka tume

ya wataalam hapo *South Sudan* na tujiunge na Sudan tukauze kahawa yetu kwa sababu kuna soko kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kyakakera Wizara ilitumia shilingi milioni 497 kwa ajili ya maji ya umwagiliaji, maji hayo hata ukitaka kikombe kimoja hauwezi kukipata. Naomba hilo jambo ahangaike nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Balozi. Nadhani wamekoma wengi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Sukum. Hawa sasa dakika tano tano, Mheshimiwa Saumu Sakala na Mheshimiwa Juma Kombo.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na uhai na kwamba naendelea kuwatumikia wananchi wa Mkinga, lakini vilevile kutoa mchango kwa Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Kamati inayohusika na Wizara hii. Kamati imefanya kazi kubwa, Kamati imetufumbua macho juu ya hali mbaya iliyopo katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoambiwa ukuaji wa sekta hii ni 1.7%, lakini unapoambiwa kwamba 65% ya Watanzania nguvu kazi hiyo inafanya kazi kwenye sekta hii halafu unapoambiwa kwamba mikopo inayokwenda kwenye sekta hii *is only 2%* na unapoambiwa kwamba fedha za maendeleo zilizotoka ni 3% tu, unachanganyikiwa. Kama nchi lazima tujitazame upya, lazima tujitafakari, tukishindwa

kufanya hivyo tutaendelea kuwa soko la nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii usindikaji wa maziwa yetu *is only 3%* ya tunachozalisha. Tunaagiza 62% ya maziwa kutoka Kenya, tunaagiza *twenty something percent* kutoka *South Africa,* tunaagiza 4% ya maziwa kutoka Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa hapa ni mashahidi leo hii Tanzania imekuwa jalala la matunda kutoka *South Africa.* Tunaagiza *apples,* machungwa na kadhalika. Hatuwezi kwenda namna hii lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anapoambiwa kwamba usindikaji wa maziwa katika nchi yake ni 3% tu, hili lazima limuumize kichwa. Nawasihi sana tuongeze nguvu katika kurekebsha mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye korosho halikadhalika. Korosho yetu yote tunaipeleka ikiwa ghafi kwa kiasi kikubwa. Nilisema juzi hapa na wapo baadhi ya Wabunge wenzangu waliniunga mkono kwamba tutumie fedha zile za *export levy,* twendeni tukajipange tuseme walau tuanze kwa kuhakikisha 50% ya korosho yetu inabanguliwa hapa ndani, tutumie fedha zile kujenga viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wizara wamekuja na *initiative* ile ya kugawa bure dawa zile za kunyunyiza. Vilevile mnaangalia uwezekano wa kutoa hata magunia, ni hatua nzuri. Hata hivyo, ili twende haraka zaidi hebu twende kule kwenye kujenga viwanda vya kubangua korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, tuliwahi kuambiwa hapa ndani ya Bunge, wakati watu wa Tanga tunapiga kelele kuhusu viwanda vya matunda, tukaambiwa Tanga machungwa yenu hayafai kwa kutengeneza *juice.* Sasa Serikali mkishasema hivyo halafu mnaishia hapo, kwa nini hamji na utaratibu wa kuhakikisha mnabadilisha mbegu ile ili tuwe na mbegu zinazofaa kwa wakulima wetu? Kwa

nini hatuipi nguvu Mlingano iweze kufanya utafiti au tukaingiza mbegu kutoka nje ili kubadilisha machungwa katika nchi yetu tuwe na machungwa hayo yanayofaa kwa kutengeneza *juice?* Nawasihi sana liangalieni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tanga tunalima mazao ya viungo, Muheza, Korogwe na Mkinga, lakini tuna tatizo kubwa la utafiti wa mbegu bora katika maeneo hayo. Mbegu inayotumika ni ya tangu Adam na Hawa. Tunaomba mfanye kazi katika eneo hilo. Najua huko mbele ya safari mtasema tumieni *ASDP* na kadhalika lakini toeni maelekezo ili kutumia *ASDP II* mambo haya yaweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine. Hivi Serikali mmeshindwa kutusaidia watu tunaolima zao la minazi kuweza kuondokana na tatizo lile kwa zaidi ya miaka 20 sasa? Kweli mmeshindwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Philipines walipopata tatizo la janga lile la mafuriko na minazi yao ikaondolewa walikimbilia kwa watu wa *FAO,* walipata fedha dola milioni 35. Leo hii Philipines imerudi kwenye *chart* yake ya kuwa nchi ya pili kwa uzalishaji wa zao la nazi duniani. Tunaomba mtusaidie tuondokane na umasikini kwa watu wetu. Zao la minazi ndani yake unapata bidhaa karibu 11 lakini zao la minazi ukilienzi maana yake hata mazingira unayatunza. Hebu tujielekeze kwenye eneo hili tuondoe tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nisipolisema nitakuwa sijatenda haki ni kuhusu uvuvi. Nimekuwa nikisema hapa sekta ya ufugaji wa samaki ndiyo sekta inayokua katika ulimwengu kwa kasi kuliko sekta yoyote ndani ya sekta za kilimo. Hapa nimeona taarifa kwamba kwa mwaka jana mazao ya samaki kutokana na ufugaji wa samaki yameongezeka kutoka tani 3,000 mpaka tani 11,000. Nina uhakika hizi ni jitihada binafsi za watu kwa sababu jedwali hili linatuonesha kwamba hatukuwa na fedha za maendeleo kwa mwaka uliopita lakini hii ni sekta ambayo tukiwekeza tunaweza kuvuna zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya miaka sita iliyopita waliwekeza takribani bilioni 35. Mwaka huu wa fedha wametenga bilioni saba kwa sekta ya ufugaji wa samaki peke yake. Jirani zetu Zambia wameanzisha mradi mkubwa, wamewekeza bilioni 112 kwa ajili ya sekta ya ufugaji wa samaki peke yake, halikadhalika Uganda. Hii maana yake nini? Maana yake wenzetu wameiona hii *opportunity* wanawekeza, sisi hatuwekezi maana yake tutakuwa soko la samaki watakaowazalisha. Nawasihi sana twendeni tukawezeke kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni bandari ya uvuvi. Hivi tunapata kigugumizi gani kwenye jambo hili? Mimi niliwahi kusema hapa hebu tujiongeze...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Rose Sukum Kamil.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipatia fursa hii niweze kuchangia Wizara hii ya Kilimo ambayo ni muhimu kwa jamii nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kuona kwamba Serikali haitambui umuhimu wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kinachonisikitisha zaidi ni kwamba mhimili huu una maisha ya Watanzania wote. Ukiangalia kwa ndani kabisa karibu 98% wanategemea chakula kwenye Wizara hii ya Kilimo na pia 80% wanategemea ajira na 95% *raw material.* Ina maana kwamba hii Wizara ndiyo Wizara mama kwa sababu wategemezi wake ni wengi mno, lakini bado inaonekana kwamba hii Wizara haifai kwa kupewa 3% ya miradi ya maendeleo. Sababu ni nini, nashindwa kuelewa.

Waziri hebu atuambie, wamepigwa sindano gani ya ganzi hampati hata kufumuka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kwenda Wizara ya Viwanda kama hukutumia Wizara ya Kilimo. Juzi Waziri wa Mambo ya Ndani amesema kiatu chake kinang'ara kwa ajili ya ngozi, kwa hiyo, wanategemea mifugo, mimi sijui kwa nini hatuoni hali halisi ya Wizara hii. Tumeona kabisa mawazo yaliyotolewa na Kamati, mawazo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani Bungeni, yanawaelekeza ni nini cha kufanya. Naomba sana muiangalie sana Wizara hii kwa sababu ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo linanitia wasiwasi nalo ni uwekezaji usio na tija. Sijui kama ametembelea maeneo yote ya uwekezaji, Serikali hii hii ya Awamu ya Tatu ilibinafsisha mashamba mengi sana, ikiwemo Wilaya ya Hanang mashamba ya *NAFCO,* naomba niyatolee mfano, yalibinafsishwa na Serikali hii lakini hakuna tija. Mashamba ya ngano, leo tunazungumza habari ya ngano inaagizwa nje, wakati kuna mashamba ya *NAFCO* yalikuwepo kule wamepewa wawekezaji. Matokeo yake mwekezaji huyo amepewa shamba la Gidagamowd amelima ekari 4,000 kati ya ekari 16,300. Shamba la Setchet amepewa ekari 16,330 amelima ekari 3,800. Shamba la Murujanda amepewa ekari 12,455 amelima ekari 6,000. Maana yake ekari zaidi ya 30,585 hazijalimwa, nayo ni mgogoro kwa sababu maeneo ambayo hayajalimwa wananchi wanaingia kulima, wengine wanaingia kufuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza hawa wawekezaji ambao hawana tija kwa nini msiondoe yale mashamba kutoka kwenye mikono yao mkayarejesha kwa wananchi? Kwa nini yabaki kwao yana faida gani? Wakati wewe ndiyo Waziri wa Kilimo kwa nini asitoe kauli hiyo ya kurudisha mashamba hayo kwa wananchi? Kwa nini Waziri hakutembelea muda wote haya mashamba ya Hanang kwa ajili ya kutoa kauli? Mimi napenda kujua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni vibaya sana kama mashamba yanakuwepo pale, Halmashauri haina tija, haipati hela ya mapato ya ndani, lakini Serikali nayo haipati kitu chochote, mmebinafsisha kila kitu, hakuna chochote tunachopata. Yale mashamba yalikuwa ni maeneo ya wafugaji waliyonyang'anywa na Serikali hii hii. Naomba hili liangaliwe sana kwa undani na nataka majibu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji, pamoja na maliasili, hii ni kero kubwa. Mheshimiwa Waziri nafikiri pia naye yupo kwenye ufugaji kama sijakosea lakini Naibu Waziri alikuwa Mkurugenzi wa Pingos na mwanasheria wetu, alikuwa anatufundisha ni jinsi gani tutapata haki kwa wafugaji, mbona amejisahau au huko ndani kuna nini? Kama yeye ndiye alikuwa mwalimu wetu leo tena hakuna kinachofanyika wafugaji wanakufa, wakulima wanakufa kutokana na migogoro ya ardhi, ni nini mnachotakiwa kufanya? *(Makofi)*

Napenda kujua na wewe Mwenyekiti ulikuwepo Bunge la Kumi, mwezi Novemba ilitolewa hoja Bungeni Kamati ikaundwa wakaleta taarifa yao Februari, 2015 ya kwamba kuna migogoro na inatakiwa itatuliwe. Kwenye taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri nzuri sana kwamba tayari wameunda timu inafanya kazi, sasa hiyo timu tangu 2015 na 2016 haijafanya kazi halafu imetengeneza sera itawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri, itawasilishwa lini. Kama mwaka jana haikufanyiwa kazi na mgogoro uko watu wanakufa, hivi hiyo timu yenu ya wataalam au wanatoka nje kwamba hawakufika ndiyo wamefanya kazi sasa hivi.

Mimi naomba tuelewe, kama ni wataalam wa Tanzania muda wote huo kwa nini hawakufanya hiyo kazi na watu wanaendelea kufa. Huu mgogoro ni mkubwa sana na mnasaobabisha ni nyie Serikali kwa kweli kwa sababu watu wengine wanauawa na polisi, watu wengine wanauwawa na askari wa wanyamapori, ni mateso makubwa sana. Tunataka ardhi tengefu iwepo haraka iwezekanavyo kuondoa migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ardhi hii inatakiwa nini? Mnasema kwamba Halmshauri wakatenge watatenga wapi? Wilaya ya Hanang mmechukua heka zaidi ya laki moja, watatenga sehemu gani ili wafugaji wao wabaki pale, ni ngumu sana. Kwa hiyo, lazima muangalie ninyi wenyewe na Waziri tembea, hebu kaangalieni ninyi wenyewe siyo kutuma wataalam pekee yao, wafanye kazi kwenye eneo husika siyo kufanya kazi ya mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni taarifa inayotolewa hapa Bungeni kuhusu idadi ya mifugo waliopo Tanzania. Naomba kujua hii sensa ilifanyika lini? Mimi ni mfugaji ukiniambia ng'ombe milioni 28.4 ndiyo wako Tanzania ni kweli yaani unakubaliana na hilo? Mbuzi milioni 16, kondoo milioni tano, kuku wa asili milioni 37, hii ni taarifa ya hapa Dodoma au ni ya Tanzania nzima? Mimi sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe sijaona sensa imefanyika nyumbani kwangu. Mimi ni mfugaji, sijaona aliyekuja nyumbani kwangu kufanya sensa ya ng'ombe. Sasa mtuambie hii taarifa yenu mliitoa wapi au mnaongezaongeza tu kama vile asilimia ya kuzaliwa na kadhalika, mimi nashangaa sana. Nina uhakika ng'ombe wako wengi, kondoo wako wengi, hata hao kuku ni wengi mno. Nafikiri hizi ni taarifa za mjini lakini siyo za kule ambako tunafuga mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tutakubaliana na Wizara hii maana yake sisi kila wakati tunasema jamani tuongeze bajeti halafu tukimaliza kuongea na kulalamika tukitoweka hapa ndani mkirudi mnasema hii bajeti ipite. Naomba kujua kuna matatizo gani, ni kwa nini tunashindwa kuelewana? Mawaziri ninyi mkishaacha Uwaziri mkija huku nanyi mnalia, sasa tunashindwa kuelewa, mtuambie kuna nini huko ili tusaidiane tuweze kupata manufaa kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kusifiana, mimi leo nitamsifia sana Mheshimiwa Rais Magufuli. Mheshimiwa

Rais Magufuli alipokuwa Shinyanga akasema kwamba afadhali mazao yapande bei ili wakulima tufaidike na sasa yamepanda bei mnalia nini? Wakulima tunafaidika nunueni debe kwa shilingi 30,000 ndiyo kazi hiyo maana yake yeye ndiyo kasema. Sasa tusipomsifia na yeye kwa kutupandisha sisi bei tutamsifia nani? Sasa na ninyi mnaanza kulalamika leteni mahindi bei ishuke, ishuke kwenda wapi? Mlikuwa mnatuumiza wakulima bei ya mahindi shilingi 5,000 kwa debe na shilingi 20,000 gunia sasa hivi tunapata shilingi 150,000, si raha yetu tumepata faida kuliko wafanyabiashara peke yao. Kwa hiyo, tunataka hiyo bei iendelee ili tuweze kupata manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/ Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Saumu Sakala na Mheshimiwa Juma Kombo dakika tano tano na Mheshimiwa Mary Muro na yeye dakika tano.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii mimi niweze uchangia katika Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Wizara ambayo binafsi naiona ni muhimu sana na imebeba kauli mbiu ya Rais ya Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kweli kabisa tusipoimarisha Wizara hii, Tanzania ya viwanda inakwenda ku-*fail.* Kilimo ndicho ambacho kimeibeba nchi yetu. Tangu enzi za Ukoloni tumekuwa tukisikia kwamba kilimo ni uti wa mgongo na mpaka sasa bado tunaendelea kuamini hivyo. Kilimo kimekumbwa na changamoto nyingi sana kiasi ambacho hata hiyo kauli ya kwamba kilimo ni uti wa mgongo ni kama vile inachezewa haileti maana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kusema kuwa kilimo kama ambavyo nimesema kimezungukwa na changamoto nyingi sana hasa ukizingatia wakulima walioko vijijini ambao ndiyo wanabeba kauli hii

ya kwamba kilimo ni uti wa mgongo bado wanalima kwa asili, kwa mazoea, tangu enzi za mababu wamekuwa wakirithi. Shamba ni lile lile ambalo mimi nalijua bibi yangu alikuwa akilima na ndiyo hilo hilo sasa hivi mama yangu analima na ndiyo hilo hilo najua mimi nitalima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalima sina mbolea, mbolea imezungukwa na urasimu mwingi tena mkubwa sana na hata nikiipata mbolea nyingi zinakuwa ni *fake* wakulima tunaathirika sana. Pia wakulima sisi tunalima kwa kutegemea mvua kitu ambacho sasa hivi kimepitwa na wakati. Mabadiliko ya tabianchi yameathiri kwa kiasi kikubwa Tanzania, mvua siyo za kutegemea tena tunatakiwa twende kwenye kilimo cha kisasa, lakini Serikali imekaa kimya hakuna elimu ya kutosha inayopelekwa vijijini kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Hakuna miundombinu inayopelekwa vijijini kwa ajili ya kilimo cha umwangiliaji tunategemea kilimo hili kitatubeba vipi? Kwa kweli Serikali kama kweli imedhamiria kumbeba Rais na kauli yake mbiu ya Tanzania ya viwanda ni lazima ihakikishe kilimo kinawekewa mazingira ambayo yatakuwa ni wezeshi kwa wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano Wabunge wa Mkoa wa Tanga hapa wamesimama hapa wakasema tulikuwa na zao la nazi katika Mkoa Tanga katika Wilaya ya Pangani na Wilaya ya Muheza, sasa hivi zao lile limekufa lakini wote tunafahamu zao la nazi jinsi lilivyo na faida katika nchi yetu. Licha tu ya kuuza nchi jirani Kenya na sehemu nyingine lakini pia ilikuwa ndiyo kitu ambacho kilikuwa kinatusaidia sisi katika kupika, kupaka, urembo na vitu vingine. Pia nazi sisi tunajengea, ni mbao kule kwetu Pangani, lakini zao hili limekufa na hakuna mtu ambaye anajali. Haya yote ni mazingira ambayo yanasababisha kilimo kiweze kurudi nyuma. Kwa hiyo, mimi nawasihi sana muangalie hali halisi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hata viwanda navyo vya mazao yetu ambayo yanapatikana kwa kudra ya Mwenyenzi Mungu. Nasema hivyo kwa sababu tunalima kwa kutengemea mvua, siku mvua ikiwa nzuri maana yake ndiyo

mazao yanapatikana sasa yakipatikana tunayapeleka wapi hata hilo soko nalo pia siku hizi hakuna. Hakuna soko la kuaminika, hakuna barabara za kuaminika ili mkulima aweze kutoa mazao yake pale na kuyafikisha sehemu inayohusika, naomba tuangalie sana sehemu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga tunalima matunda katika Wilaya ya Muheza, tuna matunda mengi sana pale, tuna machungwa sijui uende wapi usisikie chungwa la Muheza, nina imani hata huko Kusini kuna chugwa la Muheza pia, lakini Mkoa wa Tanga hatuna kiwanda cha kuchakata matunda yale. Wananchi wale wanalima machungwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sakala, muda wetu ndiyo huo, tunakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Juma Kombo kwa dakika tano.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mawili, matatu katika Wizara hii muhimu, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati tuko katika Bunge la Bajeti, Mheshimiwa Waziri aliyekuwa na dhamana muda huo au mwaka jana aliwaambia Wabunge wa Bunge hili Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba jembe la mkono litakuwa historia, lakini jembe la mkono litaonekana au litatumika katika maeneo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo jembe la mkono litatumika kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri wa kipindi hicho alisema jembe la mkono litaonekana kwenye majumba ya kumbukumbu (makumbusho), alisema jembe la mkono litatumika kwa ajili ya kuchimbia makaburi lakini alisema jembe la mkono litaonekana kwenye Nembo ya Chama cha Mapinduzi na kwamba jembe la mkono

halitatumika tena kwa shughuli za kilimo na alisema haya kwa sababu sasa Tanzania inaelekea kwenye uchumi wa kati na uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, kama tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda lazima tuboreshe kilimo na lazima tuwe na zana bora kwa ajili ya kuendeleza kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya *winding-up* ya hotuba yake atueleze hadi sasa shughuli hii au azma/dhamira hii tumefika katika eneo gani. Tumevuka pale ambapo tulikuwa tunahitaji kuvuka au bado Watanzania wanaendelea kuhenyeka na kuumia kwa kutumia jembe la mkono. Nadhani ni wakati sasa wa kupata angalau maelezo ya Serikali kupitia Wizara hii kuwaeleza Watanzania tumefikia katika hatua gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni la uvuvi. Tanzania tumebarikiwa kuwa na eneo kubwa la bahari lakini Tanzania ni pamoja na Zanzibar. Zanzibar ni visiwa ambavyo vimezungukwa na eneo lote la bahari, bahari kubwa ni bahari ya Hindi. Kiuhalisia ni kwamba hatujaitumia bahari ipasavyo katika masuala ya uvuvi wa samaki lakini katika kutumia *resource* zilizomo ndani ya bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu Waziri kama atakuwa hajui, lakini nina imani anajua kwa sababu naamini ni mlaji wa samaki. Hivi Waziri anajua kwamba hapa Dodoma tunakula vibua kutoka China?

**WABUNGE FULANI:** Eeeh.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Hivi Waziri anatambua kwamba tunakula vibua kutoka *South Africa?* Namwomba Mheshimiwa Waziri atambue hili, hivi sisi Watanzania tuna sababu gani kwa eneo kubwa la bahari ambalo limejaa *resource* ya samaki kwa nini hadi leo tunakula vibua vya *South Africa.* Mheshimiwa Waziri tunaomba na eneo hili atufafanulie kidogo tuone uhalisia na ukweli hasa wa matumizi ya bahari yetu ambayo tunayo katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho. Wachangiaji wengi wamezungumza hapa kwamba zao la korosho linastawi zaidi na sana pembezoni mwa Ukanda wa Bahari au Ukanda wa Pwani. Natambua kwamba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi si miongoni mwa Wizara za Muungano lakini kila siku hapa tunajivunia kwamba Wizara zilizoko katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wizara ambazo zinafanya kazi kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinafanya kazi kwa pamoja. Hebu tueleze hivi mmekaa lini kusaidiana na Wizara ambayo iko kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya utafiti na kuangalia labda kwa kiasi gani zao la Korosho tunaweza kuliimarisha kwa upande wa Zanzibar na likawa ni sehemu na mbadala wa zao la karafuu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary mmegawana au nikupe zote kumi? Ni haki yako.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki yangu dakika kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nina machache ya kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwanza ningependa kuungana na wengine wote waliosema Serikali iimarishe utafiti kwa sababu utafiti ndiyo utafanya zile tafiti zifike kwa wananchi waweze kulima kilimo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongolea kuhusu ushirika. Tunafahamu kabisa ushirika ulikuwa ndiyo Sera ya Mwalimu Nyerere ambayo iliwaunganisha wananchi kufikia malengo kwa pamoja. Ushirika huu kwa sasa hivi umeyumba baada ya wafanyakazi wengi kupunguzwa na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kuwa mgumu. Kwa hiyo, ningeishauri

Serikali iangalie kwa upya kuongeza wafanyakazi watakaokagua Vyama vya Ushirika kuanzia kwenye Vyama vya Msingi mpaka Vyama Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu mifugo. Wananchi wa Pwani wanaomba Waziri anapo-*wind up* awaeleze shamba letu la majani la Vikuge linayumba, lina shida, hakuna majani. Wananchi walikuwa wamezoea kununua majani kwa ajili ya mifugo, ile *zero grazing* lakini shamba la Vikuge halina majani, ukifika pale limeota miti, Waziri aeleze kuna nini hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wananchi wa Pwani wanauliza, je, Bonde la Rufiji kilimo kile kimeishia wapi na ile *RUBADA* imeishia wapi. Waziri tunaomba atueleze ili waweze kujua kwamba labda ipo siku watafikia yale malengo yaliyokuwa yametarajiwa na waanzilishi ya *RUBADA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia kwenye eneo la uvuvi. Kwenye uvuvi kuna matatizo ya nyavu na makokoro kama wanavyoita wavuvi. Hata hivyo, mara nyingi unakuta kwamba wananchi wanachomewa nyavu zao shida unaambiwa kwamba kwa sababu wanavua samaki wadogo lakini sijaona mkakakati wa makusudi wa kuzuia watengenezaji wa nyavu au waingizaji wanyavu bali wanawachomea wale ambao wananunua.

Mimi napenda Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha kwamba nyavu ambazo hazihitajiki haziingii hapa nchini kwa sababu sio kosa la mvuvi. Mnamuonea mvuvi ambaye anakwenda dukani ananunua zile nyavu kwa sababu yeye siyo muagizaji. Serikali inatakiwa iangalie suala hilo kwamba mvuvi apate haki yake, amenunua zile nyavu kwa sababu ziliingizwa na kuna watu ambao wapo kwa ajili kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba nyavu hizo haziingii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu kilimo na niungane na wale wote waliosema kwamba

Wagani wamekosa vitendea kazi. Ni kweli kabisa tusitarajie kwamba Mgani huyu yuko ofisini anatakiwa kuwafikia wananchi, aende kwa mshahara wake huo mdogo, hana posho wala kitu chochote akafanye kazi arudi na watoto wake wale nini? Hebu Serikali iangalie hapo kwamba tukitaka Mgani aweze kufanya kazi yake ni lazima tumjali kama tunavyojali wafanyakazi wengine. Hata sisi wenyewe leo hapa tungekuwa hakupati posho leo hakuna mtu angekuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia kuhusu mgogoro wa wakulima na wafugaji. Mgogoro huu ni wa siku nyingi na kila siku maelezo na majibu ni yale yale. Hivi kwa nini tusifanye *research* ili kujua ardhi ya Tanzania ni kiasi gani na matumizi ya ardhi ya hiyo ni yapi, tukayapanga kwa vipaumbele ili tujue kwamba mfugaji atakuwa na eneo lake la kufuga na mkulima atakuwa na eneo lake la kulima ili tusilete migongano. Nashauri Wizara mbili hizi zikae zikatathimini, ardhi ipi itumike kwa ajili ya ufugaji, kilimo na *reserve* kwa ajili ya wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika mifugo hiyo hiyo na napenda kuzungumzia kuhusu walaji wa nyama itokanayo na mifugo. Watanzania wengi au wenzetu anaokuja kutoka nchi za nje wanaogopa kula nyama ya Tanzania kwa sababu moja tu. Sababu ni kwamba nyama ya Tanzania ni hatari kwa sababu machinjio ni mabovu na machafu, hakuna machinjio ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali iliangalie hili kwamba kama tunaamua kuwalisha Watanzania nyama basi tuangalie hao ng'ombe wananchinjiwa wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika hapa Dodoma nimekuta kuna machinjio ya kisasa lakini kule kwangu nakotoka Kibaha, Pwani yote ile haina machinjio ya kisasa. Wizara hakikisheni kwamba mnaboresha machinjio ili wananchi Watanzania wasije wakapata maafa kwa kula nyama chafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo pia napenda kuzungunzia suala la uingizaji wa mazao ya mifugo kutoka nchi jirani. Ni kweli kabisa tuna nia ya dhati na mimi ni mfugaji vilevile, lakini kuna kitu ambacho wafugaji wa Tanzania wanapata shida ni pale ambapo unakuta tunashindana na Kenya au na Uganda kuingiza mazao ya mifugo au mazao ya kilimo bila Serikali kujali angalau wafugaji au wakulima wa ndani. Naishauri Serikali iangalie kwa sababu wananchi wanakuwa wame-*invest* fedha nyingi kwenye kilimo au kwenye mifugo, mtu anafuga kuku anaenda sokoni anakosa pa kuuza mayai kwa sababu mayai ya Kenya yamejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo tumeona sehemu nyingi sana wananchi wanalima kwa kujitegemea. Wanajitegemea kwa sababu yeye ndiyo atatafuta mbegu na kila kitu, lakini Serikali inataka kupanga bei au inamzuia kwamba asiuze mazao yake au auze kwa wakati fulani. Tunatakiwa tufahamu kwamba kama unamwambia mwananchi asiuze mazao yake na ana watoto wanatakiwa kwenda shule na anatakiwa kwenda kwenye matibabu bila kuuza mazao yake atategemea nini na yeye anategemea mazao yake ndio *ATM* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali itoe elimu kwamba mkulima atalima lakini auze kwa namna moja, mbili tatu lakini isizuie kabisa kwamba wakulima hakuna kusafirisha kwenda kuuza wapi kwa sababu *sometimes* anakwenda labda kuuza Uganda kwa sababu anajua kabisa Uganda kuna bei nzuri. Kama Serikali inanunua kwa bei ndogo, kwa nini asiuze sehemu nyingine ili aweze kurudisha gharama zake alizotumia wakati wa kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu maghala na ununuzi wa Serikali wa mazao ya wakulima. Mazao mengi yanabaki bila kununuliwa na Serikali inanunua mazao machache, kwa mfano tuchukulie mikoa ambayo ni *big five* unakuta mara nyingi wana mazao mengi kuliko uwezo wa Serikali wa kununua. Kwa nini Serikali isiongeze uwezo wa kununua mazao ili wananchi wasiweze kupoteza

mazao yao kwa sababu unakuta hakuna maghala ya kuhifadhia na hakuna ununuzi, watu wameweka mazao yao nje yananyeshewa na mvua, nguvu za wananchi zinapotea bure. Naishauri Serikali iliangalie hilo na ilitendee kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Desderius Mipata atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki na Mheshimiwa Oliver Semuguruka ajiandae.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Na mimi niungane na wenzangu kusema kwamba tozo zilizofutwa kwenye kilimo, mifugo pamoja uvuvi zinawafariji wadau zaidi wa maeneo hayo hasa wananchi wetu. Nipongeze Serikali kwa hatua hiyo. Lakini nitapongeza zaidi kama tabia ya kuchelewesha pembejeo itaachwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamepitia vizuri kwenye vitabu na wameeleza kwamba kama kilimo ni tegemeo letu kwa nini sasa pesa zinazotengwa kwenye kilimo zinakuwa chache. Nimeangalia na nimeona kila mwaka pesa tunazotenga kwenye kilimo ni kidogo, lakini hata utoaji wa fedha zenyewe zile za kwenye bajeti zinakuwa kidogo zaidi, zile za wafadhili zinakuwa zimeongezeka yaani kama sisi wenyewe hatujaona umuhimu wa kilimo licha ya takwimu kuonyesha kwamba kilimo kinategemewa na Watanzania wengi. Kilimo ni mhimili wa uchumi wa Taifa letu na ni mhimili wa chakula katika nchi yetu kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, ni vitu vya kuangalia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mpango wa Uendelezaji wa Kilimo Awamu ya Pili umelenga kuongeza thamani ya chakula na tija zaidi kwa wakulima. Naishauri Serikali mpango huu uelekezwe zaidi kwenye vijiji vya uzalishaji mali kwa kuangalia miundombinu ya barabara. Kuna vijiji vyangu pale kwenye Jimbo langu, kijiji cha Milundikwa kwenda Kisula kuna barabara ya uzalishaji na si nzuri sana.

Mkiiweka kwenye mpango huu wa kuboresha maeneo ya kilimo kwa utaratibu wa kuboresha barabara zao inaweza ikatusaidia. Ipo barabara pia ya kutoka Katani kwenda Myula, barabara ya kutoka Kasu kwenda Malongwe ni maeneo ambayo yanatusaidia sana katika suala zima la uzalishaji katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizungumzie pia juu ya Ranchi za Taifa. Kupitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri nimeona ni kama Ranchi ya Taifa *(NARCO)* ni kama haina mtaji wa kutosha kuwezesha kusaidia Ranchi zetu za Taifa. Nikitolea mfano juu ya Ranchi yetu ya Kalambo ambayo ina ukubwa wa hekta za eneo 23,000 yenye uwezo wa kuwa na ng'ombe zaidi ya 7,000; lakini leo hii Kalambo ina ng'ombe 700, sasa utaona kama ipo *under utilized.*

Kwa hiyo, ni vizuri Serikali itusaidie kuimarisha ranchi zetu hizi ili iwe ni mfano wa kuigwa kwa wafugaji wanaozizunguka. Kwa sasa mchango huo huuoni kwa wananchi wanaozunguka ranchi hizo, nadhani ndiyo ilikuwa maana kubwa ya Serikali ya kuweka ranchi hizi katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaohudumiwa na Kalambo hasa katika *blocks* zile zilizobinafsishwa sasa hivi wana mgogoro pia wa mpaka kati ya *Rwamfi Game Reserve* na Kalambo yenyewe. Wanapoendeleza shughuli zao na huku wanalipa kodi ya Serikali lakini Serikali bado inawafanyia fujo kwenye mipaka ile ya *Rwamfi Game Reserve.* Kwa hiyo, kuna sababu ya kupitia mipaka upya ili kutowasumbua wananchi hawa ambao wanalipa kodi. *(Makofi)*

Vilevile kwenye uzalishaji wa mifugo (ng'ombe), kuna shida ya kupata madume, madume ni machache. Tungetegemea madume yazalishwe kwa wingi ili wananchi walio katika *block* hizi waweze kunufaika na *breed* hizi mpya za kisasa zenye kuleta tija za ufugaji. Hii ingeweza kutusaidia kuliko ilivyo sasa hivi madume tunategemea uhaimilishaji ambao wananchi hawajauzoea na wakati mwingine wanaona kama ni gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuongelea chanjo na dawa za mifugo. Katika Mkoa wa Rukwa imetajwa Wilaya ya Nkasi hapa kwamba ni eneo ambalo mnataka mliendeleze liwe *free* kwa magonjwa lakini dawa tunapata kutoka Arusha, ni mbali. Hakuna *center* ya karibu ya kupata dawa na chanjo ili wakulima na wafugaji waweze kupata dawa katika maeneo ya karibu. Hii ingeweza kutusaidia kuboresha eneo la ufugaji kwa maeneo ya Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu soko, wafugaji wanafuga lakini hakuna soko la karibu la kuuza nyama kwa bei nzuri. Tuna kiwanda pale cha Mheshimiwa Mzindakaya, tungeweza kuona Serikali kama kuna changamoto yoyote kiweze kuboreshwa ili kiweze kuhudumia *center* ya eneo letu katika suala zima la mifugo yetu ambayo tunaizalisha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu suala zima la uvuvi. Katika eneo la uvuvi hatujafanya vizuri. Wakati tunaongeza uchangiaji wa ruzuku kwenye kilimo lakini wavuvi kidogo tumewaacha nyuma. Naomba Serikali tuongeze zaidi kuwachangia wavuvi katika vifaa ambavyo vinaasaidia na mikopo ambayo inaweza ikawasaidia. Hivi karibuni mlitueleza hapa kwamba wavuvi wangeweza kuweka utaratibu wa mfuko wao wa kuwakopesha lakini huo mfuko sijauona kama umetusaidia kwa kiwango chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika lile lina mwambao mkubwa sana na wavuvi wengi wanaokaa kule ni maskini lakini hatujasaidiwa vya kutosha na pesa yoyote iliyotoka Serikalini kwa ajili ya kusaidia vikundi vya wavuvi ili waweze kuboresha maisha yao. Wamezungukwa na rasilimali ambazo ni tajiri sana, lakini bado naona kama ni maskini. Naiomba Serikali ione uwezekano wa kutoa pesa za kutosha kusaidia wavuvi kama vile tunavyosaidia wakulima na wafugaji wakati mwingine wanasaidiwa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na timu yao yote ya Wizara kwa namna ambavyo wanafanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze sana kwa sababu ya kuja na mpango mzuri hasa unaohusiana na mbolea. Kuna mambo mengi yamesemwa kuhusiana na mbolea lakini mimi nataka tu kutahadharisha mambo mawili au matatu. Mpango wenyewe ni mzuri wa kununua mbolea kwa pamoja, ni mpango mzuri sana. Mambo matatu tu ninayotaka yaweze kufanyika kwa wakulima wangu waliopo Maswa na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla, moja ni bei. Najua mtatoa bei elekezi kwa sababu wale wauzaji wasije wakavuka pale, kwa hiyo, naomba bei iwe nafuu, kama itakuwa nafuu hakuna shida.

Pili, ni kufika kwa wakati, mbolea hiyo ifike kwa wakati kwa wakulima wetu, isipofika kwa wakati kama walivyochangia Wabunge wengine itakuwa haina maana sana.

Lakini la tatu kwenye mbolea, nataka tu kusema kwamba mbolea hii sasa ipatikane maeneo yote, siyo ukanda fulani tu upewe mbolea na ukanda mwingine usipate mbolea. Kwa sababu sasa tutakuwa na uhakika wa kuipata mbolea hii na inapatikana kwa wote basi ipatikane kwa wakulima wote nchi nzima. Hongereni sana kwa mpango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze kwa kutoa tozo hizo ambazo zilikuwa zimerundikwa kwenye kilimo. Waheshimiwa Wabunge tozo hizi zilikuwa zinakwamisha mambo mawili, moja ni bei za mazao kwa ajili ya wakulima wetu zilikuwa zinakuwa chini kwa sababu tozo nyingi zipo

pale. Pia zilikuwa zinakwamisha uwekezaji kwenye sekta hii ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze pia kwa kusimamia vizuri ushirika, ulishaanza kulegalega na kwenda tenge, lakini kwa ujio wenu naona sasa mambo yanaanza kurekebishwa kwa sababu wale walafi wa pesa mnaanza kuwachukulia hatua. Hongereni sana na endeleeni na maeneo mengine ambayo yamebakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nawapongeza ni la pembejeo, mmesimamia vizuri habari ya pambejeo, ule wizi uliokuwa ukifanyika mmeusimamia vizuri na mpo imara katika hilo. Nataka muendelee kusimamia namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sasa niishauri Serikali kwenye eneo la kilimo hasa kwenye uwekezaji. Uwekezaji kwenye kilimo umekuwa ni mdogo sana. Kwa muda wa miaka mitano iliyopita uwekezaji upande wa ukuaji wa kilimo ni mdogo sana. Kwa muda wa miaka mitano iliyopita kilimo kimekua kwa wastani wa asilimia 2.8, ni asilimia ndogo, lakini ukilinganisha ukuaji wa watu kwenye nchi yetu ni asilimia 2.7. Sasa ukijaribu kulinganisha ukuaji wa kilimo na ukuaji wa idadi ya watu karibu ni ule ule. Sasa ukikumbuka kwamba ukuaji wa kilimo ndiyo ukuaji wa kipato chetu maana yake ni kwamba kipato cha Watanzania wengi ambao wanaajiriwa kwenye kilimo hakijakua kwa kiasi kinachoweza kusemwa ni kikubwa, haujakua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mfululizo wa ukuaji wa kilimo umekuwa ukiendelea kushuka kila wakati, kila mwaka umekuwa ukishuka. Mwaka 2014 kilimo kilikua kwa asilimia 3.4, mwaka 2015 asilimia 2.3 na mwaka 2016 asilimia 2.1. Sasa ukuaji huu ni mdogo sana. Tunapoendelea na ukuaji wa kilimo ukiwa mdogo hivi ni hatari kwetu kwa sababu bado tunategemea kilimo lakini pia ni hatari kwa Sera ya Viwanda ambayo Serikali yetu inaiendesha sasa hivi maana yake malighafi kutoka viwandani itakuwa ni kidogo na matokeo

yake vile viwanda ambavyo Mheshimiwa Mwijage anaalika wawekezaji kila wakati na siku mbili zilizopita alikuwa akituelezea hapa kwamba ameweza kuanzisha viwanda vingi, vinaweza kuwa na hatari ya kufungwa baadaye kwa sababu ya vitakosa malighafi kwasababu ya ukuaji mdogo kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali iendelee kuwekeza kwenye kilimo kwa sehemu kubwa sana lakini pia Serikali hii iendelee kuhamasisha wawekezaji wengine hasa sekta binafsi ili iweze kuchangia kwa sehemu kubwa kwenye kuwekeza kwenye kilimo. Vinginevyo kama tukiitegemea Serikali yenyewe tu hatutafika kukamilisha kuwa na malighafi zitakazotosha kwa viwanda vile ambavyo tunategemea vianzishwe kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tukitembelea Mkoa wa Shinyanga na Mwanza tulikuta kiwanda cha nyuzi cha pale Shinyanga kinachotumia *raw materials* (malighafi), pamba kwa wingi kimesimamisha uzalishaji wake. Tatizo mojawapo ilikuwa ni kwamba wamepungukiwa na pamba kwenye kiwanda chao. Kwa hiyo, tuongeze uwekezaji kwenye kilimo ili tuhakikishe kwamba malighafi nyingi zitakazopatikana zinatumika kwenye viwanda vyetu ambavyo vimekwisha kuanzishwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni umuhimu wa umwagiliaji kwenye nchi yetu. Nimekuwa nikizungumza habari ya umwagiliaji sana, lakini ni muhimu sana kwa wakati huu kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi ambayo tunafahamu sasa hivi mazingira ya dunia yamebadilika, kumeongezeka joto na mambo mengine na ukame unaongezeka. Sasa tusipotia nguvu kwenye umwagiliaji tutakuwa bado tunarudi nyuma kwa sababu kilimo cha kutegemea mvua hakitoshelezi mahitaji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kina faida nyingi, moja mkulima atalima muda wote kwa hiyo atakuwa na ajira mwaka mzima. Vilevile wawekezaji

wanaokuja kuwekeza kwenye viwanda watakuwa na uhakika wa kupata malighafi wakati wote wa uzalishaji wa viwanda vyao. Pia umwagiliaji unatusaidia wakulima kwa sababu badala ya kulima mara moja utalima mara mbili ama mara tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fursa kubwa sana kwenye suala la umwagiliaji kwenye nchi yetu. Takwimu tulizonazo zinasema tuna hekta milioni 29 zinazofaa kwa umwagiliaji lakini eneo linalomwagiliwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipati nafasi niweze kuchangia katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayozidi kufanya katika Taifa letu. Mimi binafsi namuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumtia nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanazozidi kuzifanya kwa kulitumikia Taifa letu kwa moyo wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze moja kwa moja kutoa mchango wangu katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambayo ni Wizara nyeti inayotegemewa na Taifa letu. Mkoa wa Kagera tumebarikiwa kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba na hali ya hewa nzuri yenye mvua nyingi za kutosha. Mkoa wa Kagera kilimo kimekuwa cha kusuasua kutokana na changamoto mbalimbali. Kwanza kabisa kuwa na teknolojia duni na pembejeo kutokufika kwa wakati. Mkoa wa Kagera tuna ardhi nzuri sana na tunapata mazao ya kila aina lakini pembejeo zimekuwa za shida sana kutufikia kwa wakati na pia teknolojia duni, bado hatujapata teknolojia za kisasa kuweza kulima kwa kutumia teknolojia hizo. *(Makofi)*

Katika Mkoa wa Kagera kuna miundombinu mibovu ya kusafirisha mazao toka shambani hadi kwenye masoko. Wakulima wanapata shida sana kutoka shambani hadi kufikia masoko, miundombinu ni mibovu, barabara ni mbovu. Namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili waweze kutengeneza barabara wakulima wetu waweze kufika kwenye masoko bila tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kagera magonjwa ya mimea na mazao ya chakula kama zao la migomba linalolimwa na kutegemewa na wakazi wa Kagera linashambuliwa na ugonjwa wa mnyauko. Ugonjwa wa mnyauko umetushambulia sana katika Mkoa wetu wa Kagera ambapo migomba ndiyo tunayoitegemea kama chakula chetu kikuu. Naiomba Wizara ya Kilimo pamoja na Waziri waweze kutusaidia ili kuweza kupata tiba ya huu ugonjwa wa mnyauko kwa sababu ndilo zao kuu tunalolitegemea kwa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Kagera umebarikiwa kuwa na mazao ya biashara ya kahawa na miwa lakini kahawa imekuwa haipati soko zuri sana yaani hatupati bei nzuri hadi inapelekea wakulima kwenda nje ya nchi, kwa mfano, wanapeleka Uganda ili waweze kupata

bei nzuri. Naomba Serikali na Wizara husika waweze kuangalia zao letu la kahawa *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna zao la miwa, kwa upande wa zao hili napenda kuishauri Serikali kuweka mashamba darasa kwa wakulima wadogo wadogo ili waweze kuungana na wakulima wakubwa waweze kupata utaalamu wa kulima kwa kisasa zaidi. Naishauri Wizara ya Kilimo waweze kutuletea Maafisa Ugani, ikiwezekana kila kijiji, ili wakulima waweze kujifunza zaidi katika zao letu hili la miwa. Miwa ni zao kubwa sana ambalo linatupatia sukari, kwa mfano kwa sasa hivi sukari imekuwa tatizo katika nchi yetu, lakini tungekuwa na wakulima ambao wanaelewa vizuri hili tatizo lisingekuwepo, tungeweza ku-*supply* katika mikoa yote kutoka Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Kilimo iweze kufikiria kuweka mashamba darasa ili wakulima waweze kupata elimu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea kuhusu mawakala wa pembejeo za kilimo, mpaka sasa wameendelea kupigwa danadana kwa kutokulipwa fedha zao. Tukumbuke mawakala wengi walichukua fedha za mikopo katika benki, wengi wamepoteza hadi maisha yaani mtu akiwaza nyumba yake inapigwa mnada, hakuna mtu ambaye anaweza kumsaidia ili aweze kulipa lile deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameshasema kwamba wanafanya uhakiki wa mawakala wanaodai Wizara, mawakala wote nchi nzima wanadai Wizara ya Kilimo shilingi bilioni 64.4 ambapo Wizara inawapiga danadana na hawajui hatma ya deni lao, japo Wizara ya Kilimo inasema bado inafanya uhakiki wa deni hilo. Sasa itafanywa uhakiki mpaka lini na watu wanazidi kupoteza maisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hebu fikiria hivi tunavyokuja Bungeni, mtu usipopata posho yako, tunalalamika kutokupata posho, sasa endapo umechukua mkopo wa benki na ume-*supply* hizo mbegu sehemu yako na bado hujaweza kulipwa, kweli hii inaumiza sana kwa

sababu watu wanapoteza maisha, wanaacha familia zao zikihangaika. Naiomba sana Serikali na Wizara husika iweze kuwafikiria hawa watu ambao wali-*supply* hizi mbegu kwa wakulima. Basi ni vyema ikaanza kuwalipa wale iliyojiridhisha kuwa wanastahili kulipwa na wale ambao bado hawajiridhisha Wizara iangalie namna ya kuwasaidia watu hawa hata kwa mawazo. Kwa sababu mtu kama ameshatoa hela yake, inatakiwa kwa kweli apate *counseling* ili vifo visiendelee kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye uvuvi. Wavuvi hawako salama, kuna wavuvi wanakwenda kuvua usiku, wanatekwa na majambazi na wananyang'anywa samaki wao. Kwa hiyo, naomba angalau kuwepo na doria mle ziwani au baharini wanapokwenda kuvua samaki. Naomba Serikali waangalie kwa jicho la huruma suala hili. Pia leseni wasitoze zaidi ya mara moja, unaweza ukakuta mvuvi anatozwa leseni zaidi ya mara mbili, tunaomba Serikali iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea pia nyavu wanazotumia zinazosemekana kwamba ni mbovu. Hivi, hizo nyavu ambazo hazitakiwi mpaka zinaingia nchini Serikali inakuwa inaangalia wapi mpaka waweze kumuonea huyu anayekwenda kuvua samaki au hawa wavuvi wanawachomea nyavu zao. Kabla hawajafika hiyo hatua, naomba Serikali ifanye uchunguzi wa hizo nyavu zisiweze kuuzwa hata madukani kwa sababu wanawapa hasara wananchi wetu. Kwa kweli inatia uchungu sana katika upande wa uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee sekta ya mifugo. Mkoa wa Kagera wafugaji wamenyanyasika sana, wamehamishwa kupelekwa huku na huku na wengine wamepoteza ng'ombe wao wengi. Huku wanasema kwamba hakuna sehemu ya kufugia na wakulima vilevile wanasema hakuna sehemu ya kulima, lakini naomba Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma hawa wafugaji na wakulima pia, itenge sehemu ya kwamba hawa wafugaji wanatakiwa wafugie sehemu fulani na hawa wakulima wapate sehemu

ya kulima lakini imekuwa ni tatizo kubwa. Wafugaji wa Mkoa wa Kagera wanalia, wamenyang'anywa ng'ombe wao, wamepotea na kwa upande wa wakulima ng'ombe wanaenda kula mazao ya wakulima vilevile, yaani kote kote ni shida. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba uliangalie hili kwa uso wa huruma. Mimi mwenyewe ni mfugaji, hata wewe najua ni mfugaji, kwa hiyo, naomba uangalie jinsi ya kusaidia hawa wafugaji waweze kupata sehemu ya kufugia ng'ombe wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa, naunga mkono hoja ya Wizara yetu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo ni Mheshimiwa Zitto kwa dakika saba.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho leo katika Wizara hii.

Kwanza napenda kuwapongeza wachangiaji wote wa pande zote ambao wamechangia katika Wizara hii, wameonesha maeneo mbalimbali ambayo wanadhani kwamba yana haja ya kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeza kwa dhati kabisa Kamati ya Kilimo kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya uchambuzi wa bajeti hii na vilevile Waziri Kivuli wa Kilimo kwa maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu nyingi zimeelezwa hapa kuhusiana na Wizara hii na takwimu hizo zinaonesha ni namna gani ambavyo Wizara hii ni muhimu sana na ingehitaji kuwekewa nguvu za kutosha katika namna ambavyo inatekelezwa. Mwaka 2009 pato la Taifa la nchi yetu lilikuwa ni dola za Kimarekani bilioni 21.4. Mwaka 2016, miaka saba baadaye, pato la Taifa la nchi yetu lilifikia dola za Kimarekani bilioni 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba ndani ya kipindi cha miaka saba, tuliweza ku-*double* na zaidi pato la Taifa, lakini viwango vya umaskini wa Watanzania vimekuwa vikiongezeka kwa maana ya idadi ya watu maskini Tanzania imekuwa ikiongezeka licha ya pato la Taifa kuongeza zaidi ya mara mbili. Sababu ni nini? Sababu ni sekta ya kilimo. Hatuwekezi vya kutosha kwenye sekta ya kilimo na ndiyo maana malalamiko ya Wabunge yamekuwa ni mengi sana katika hili eneo. Kwa sababu kama una sekta ambayo watu asilimia 65.5 kwa mujibu wa takwimu za Serikali wanaitegemea, lakini sekta hii katika fedha zake za maendeleo inapelekewa asilimia tatu tu, ni dhahiri kabisa kwamba hatuwafanyii kazi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Wizara zote, tunaweza tukawa tunajadili na tukapitisha bajeti, lakini Wizara ambayo inawahusu Watanzania moja kwa moja ni Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi lakini mmeona dhahiri namna gani ambavyo Wizara hii bajeti yake, hata ile kidogo ambayo imetengwa, bado haiendi. Ukienda kuangalia vitabu vya maendeleo utaona kwamba katika kitabu cha maendeleo sehemu kubwa ya bajeti ambayo tuliitenga mwaka jana kwa ajili ya bajeti ya kilimo ilikuwa ni *Storoge Capacity Expansion Project* (Utunzaji wa Mazao yetu baada ya Uvuvi) mradi ambao ulikuwa ufadhiliwe *locally* na *foreigners* walikuwa ni Poland. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaposema kwamba ni bilioni tatu ambazo zimepelekwa kwenye Wizara hii maana yake ni kwamba mradi kama huu wote mwaka jana haukutekelezwa. Maana yake ni kwamba mwaka jana tumewalipa mishahara, tumewapa posho, tumewaweka ofisini wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo lakini hakuna kazi yoyote ya kimaendeleo ambayo ilifanyika. Hali kama hii kwa kweli inasikitisha sana na ni hali ambayo inabidi tuweze kuona ni namna gani ambavyo tutaweza kuirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuangalia maeneo hayo ya bajeti ndogo ambayo inapelekwa ya Wizara ya Kilimo, lakini pili naomba tuweze kuangalia ni namna gani

ambavyo mafanikio ambayo yamepatikana tunayalinda kivipi. Kwa mfano, napenda niwapongeze sana ndugu zangu wa Kusini kwa mavuno mazuri sana ya korosho na kwa fedha nyingi sana ambazo wamezipata kwenye korosho, lakini pamoja na ongezeko la mavuno ya korosho na ongezeko la bei ya korosho kwenye Soko la Dunia, sehemu kubwa ya mabadiliko haya ni ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwakani ikitokea kwamba bei ya korosho imeshuka, tutawafanya nini hawa wakulima na hapo ndipo inapokuja hoja ya msingi sana ya Hifadhi ya Jamii kwa Wakulima. Kuweka mfumo ambao utakuwa na fao la *price stabilization* ili pale ambapo bei za mazao ya kilimo zimekuwa kubwa sana, tuweze kuwa na sehemu ambayo itatunzwa, bei ikiporomoka chini ya gharama za uzalishaji kwa mkulima, mkulima yule atalipwa kumrudishia gharama za uzalishaji. Sasa hili ni eneo ambalo Waziri ameligusa, kuna *paragraph* moja amezungumza kuhusu *Wakulima Scheme* inaendeshwa na *NSSF,* lakini kuna haja kubwa ya kuweza kuangalia ni namna gani tutapanua hifadhi ya jamii kwa wakulima ili tuweze kuhakikisha kwamba wakulima wanakuwa na fao la bei. Siku bei zikiporomoka wakulima waweze kurudishwa katika zile bei ambazo angalau zitalinda hali yao ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naomba nirejee hoja ambayo Kambi ya Upinzani Bungeni imezungumza kuhusiana na tozo kwa wavuvi. Kuna malalamiko makubwa hasa kule kwetu upande wa Ziwa Tanganyika, *SUMATRA* inatoza leseni za usafiri kwa wavuvi na jana nimemsikia Waziri anasema kwamba kuna tozo ambazo zimeondolewa za kiwango fulani cha mitumbwi.

Naomba nipate ufafanuzi wa kutosha, kwa sababu *SUMATRA* hawatozi tozo ya leseni ya usafiri kwenye matreka, kwa sababu matrekta yanatumika kulima, lakini wanatoza tozo ya leseni ya wavuvi kwenye mitumbwi ya kuvulia. Sasa nataka nipate hapa haki inakuwa wapi, kwa sababu mvuvi hiki ndicho chombo chake cha kuzalisha, kwa nini atozwe, lakini mkulima chombo chake cha kuzalisha ambacho ni

trekta yeye asiweze kutozwa? Kwa hiyo, naomba nipate maelezo haya ambayo pia Kambi ya Upinzani Bungeni imeyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nawapongeza sana tena Kamati ya Kilimo na naomba ninukuu sehemu ya hotuba ya Kamati ya Kilimo ambayo nadhani inahitaji majibu ya Serikali, ambayo inasema kwamba; "Kwa mwenendo huu wa bajeti unaashiria kwamba, kilimo si moja ya vipaumbele vya Serikali; Serikali haitambui umuhimu wa sekta za kilimo katika ustawi wa sekta zingine na kilimo si sekta mama ya ustawi wa wananchi ambao wengi wanajihusisha na shughuli za kilimo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi hoja za Kamati ya Kilimo, naomba zipate majibu ya uhakika kutoka Serikalini kwa sababu ndiyo hoja ambazo zinawahusu wakulima na wananchi wetu kwa ujumla. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo, tumejitahidi kulinda uwiano wetu vizuri. La pili, sina matangazo ila kuwakumbushia yale niliyoyatangaza, mechi ya leo na semina ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru kwanza kwa sasa saa 8 mchana kwa kazi mliyoifanya, hoja hii tunayo mpaka kesho kutwa, siku ya Jumatatu ndiyo mtoa hoja atahitimisha. Kwa hiyo, wale ambao hatukufanikiwa kuchangia leo nadhani kwa taratibu zetu baadhi yenu mtapata nafasi ya kuchangia siku ya Jumatatu.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi keshokutwa, siku ya Jumatatu, tarehe 22 Mei, saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 22 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*